*Copyright © 2017 GMI Publications*

# WOKOVU

## Kazi Kuu ya Mungu

**Kimeandikwa na**

**Fred Vinton**

1011 Aldon Street, Wyoming, MI 49509, USA
www.vitabuvyakikristo.com

**WOKOVU KAZI KUU YA MUNGU**

Copyright © 2017 GMI Publications

GMI Publications ina haki zote za tafsiri ya kitabu hiki. Hairuhusiwi kuchapa na kuuza sehemu yo yote ya kitabu hiki bila ruhusa ya GMI Publications. Vilevile hairuhusiwi kuuza nakala za kikompyuta (digital copies) bila ruhusa ya GMI Publications.

Mfasiri – Steven Sherman
Wahariri – Mch. Fraison Ismail, Mch. Albert Juliano Simwanza, na Steven Sherman

Kama Biblia nyingine hazijatajwa, dondoo zote za kunukuu Biblia zinatumia Swahili Union Version (SUV): Haki miliki -1952, 1997: kwa: Chama cha Biblia cha Tanzania na Chama cha Biblia cha Kenya. Haki zote zimehifadhiwa.

**GMI Publications ni idara ya Grace Ministries International; misheni ifanyayo kazi na makanisa ya Neema duniani, pamoja na Wakristo wote wanaomwamini Yesu Kristo kuwa Mwokozi wao.**

## Yaliyomo

1. Habari ya Wokovu Ulianzaje? .................................................... 4
2. Kwa Nini Wanadamu Wanahitaji Kuokolewa? ........................... 5
3. Kwa Nini Wenye Dhambi Hawawezi Kujiokoa? ........................ 9
4. Kwa Nini Sheria Haiwezi Kutuokoa? ....................................... 11
5. Basi, Tuna Tumaini Lo lote la Kuokolewa? .............................. 15
6. Wokovu ni Nini? ........................................................................ 16
7. Msingi wa Wokovu ni Nini? ..................................................... 17
8. Kwa Nini Kifo cha Yesu ni Muhimu? ....................................... 18
9. Kwa Nini Kufufuka kwa Kristo ni Muhimu? ............................ 20
10. Je, Yesu Alizifia Dhambi Zote? ............................................... 21
11. Nifanye Nini Nipate Kuokoka? ............................................... 25
12. Toba Inahusikaje Katika Wokovu? .......................................... 28
13. Kunatokea Nini Mtu Anapookolewa? .................................... 32
14. Wokovu Unaleta Mabadiliko Gani Katika Uhusiano Wetu na Shetani na Dhambi? 33
15. Wokovu Unaleta Mabadiliko Gani Katika Uhusiano Wetu na Mungu? 34
16. Wokovu Unaleta Mabadiliko Gani Ndani Yetu? ...................... 43
17. Je, Mungu Aliwachagua Wote Watakaookoka? ....................... 44
18. Je, Mtu Anaweza Kujua kwa Uhakika Kwamba Ameokoka? .. 46
19. Uzima wa Milele Unadumu Muda Gani? ................................ 46
20. Kunamtokea nini Mtu Anapookolewa? ................................... 47

*Copyright © 2017 GMI Publications*

# UTANGULIZI

Kila anayetaka kwenda mbinguni na kujenga mahusiano mazuri na Mungu, lazima afahamu kwa usahihi yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu wokovu. Ufahamu sahihi wa elimu ya wokovu ni muhimu kwa kila anayetumaini kuokolewa kwa sababu ni msingi wa imani ya kweli. Mtu akiukosa ufahamu sahihi wa wokovu, anaweza kufikiri kwamba ameokolewa, kumbe si kweli, bali amejidanganya. Atajutia siku atakaposimama mbele ya Kristo na kuambiwa, "Sikukujua, ondoka kwangu". Pia, mbaya zaidi, anaweza kuwashuhudia watu Injili isiyo ya kweli hata na wao pia wakatupwa motoni pamoja naye. Shida nyingine inayosababishwa na kutoelewa wokovu kwa njia iliyo sahihi ni kwamba inaweza kusababisha mtu aliyeokoka kweli kuwa na mashaka juu ya wokovu wake na kukosa amani na raha ambazo ni matunda ya wokovu wa kweli.

Katika somo hili tutachunguza Biblia inavyofundisha kuhusu wokovu ili kila mmoja wetu awe na ufahamu sahihi wa wokovu. Ufahamu sahihi wa wokovu ni msingi muhimu wa maisha ya Kikristo. Ili Mkristo aweze kuishi kama anavyopaswa, anahitaji kuyajua yale yaliyofanyika alipookolewa na ajue uwezo alio nao katika kuishi maisha mapya. Tutajifunza jinsi wokovu unavyomletea Mkristo maisha haya mapya.

Lakini pia, kwa sababu watu wengine wameyachanganya mafundisho ya wokovu, tutayachunguza mafundisho ya uongo kuhusu wokovu pia. Kwa mfano hali ya kutegemea matendo mema kwa wokovu au utegemezi katika kifo cha Yesu pamoja na ubatizo. Tutaona kwa nini mafundisho haya ni ya uongo na kwa nini mafundisho haya hayawezi kumwokoa mtu ye yote.

Kitabu hiki kinagawanyika katika sehemu kuu mbili. Katika sehemu ya kwanza tutajifunza yale ambayo mwenye dhambi anapaswa kuyajua na kuyaamini ili aokolewe. Katika sehemu ya pili tutajifunza jinsi wokovu unavyokuwa msingi wa maisha ya Kikristo.

Kabla hatujaanza, tufafanue maneno na mawazo mengine yanayohusu wokovu. Ni muhimu kufanya zoezi hilo kwa sababu maneno mengine yana maana zaidi ya moja na hata uelewa wa watu kuhusu maana ya maneno mengine ni tofauti.

***Kwanza, wewe mwenyewe ufafanue jinsi unavyoelewa maneno haya:***

- Mkristo
- Muumini
- Mshirika wa Kanisa
- Mwenye kuhudhuria Kanisani
- Wokovu

***Jibu maswali yafuatayo kwa kuweka "x" kwenye nafasi ya jibu lililo sahihi.***

Kufuatana na ufafanuzi wako wa "Mkristo", Wakristo wangapi wameokolewa?
____Wote____Karibu Wote____Baadhi____Hakuna

Kufuatana na ufafanuzi wako wa "Muumini", Waumini wangapi wameokolewa?
____Wote____Karibu Wote____Baadhi____Hakuna

Kufuatana na ufafanuzi wako wa "Mshirika wa Kanisa", washirika wangapi wameokolewa?
____Wote____Karibu Wote____Baadhi____Hakuna

Kufuatana na ufafanuzi wako wa "Mwenye kuhudhuria kanisani", wangapi kati ya hawa wameokolewa?
____Wote____Karibu Wote____Baadhi____Hakuna

Kuna njia zaidi ya moja ya kufafanua maneno hayo. Lakini utakapoona maneno hayo katika kitabu hiki ujue ninatumia maana zifuatazo:

- Mkristo – Ni mtu aliyeokolewa kweli.

*Copyright © 2017 GMI Publications*

- Mwamini - Ni mtu aliyeokolewa kweli.
- Mshirika wa Kanisa – Ni mtu aliyepokelewa katika tawi la Kanisa ambaye labda ameokolewa au labda hajaokolewa.
- Mwenye kuhudhuria Kanisani – Ni mtu anayehudhuria tu. Pengine ameokoka, pengine hajaokoka. Pengine ni mshirika na pengine siyo mshirika.
- Wokovu – Ni kurejezwa na kupatanishwa na Mungu ili mtu awe na uhusiano na ushirikiano na Mungu.

Je, ufafanuzi au matumizi yako ya maneno haya yanaendana na maana ya maneno haya katika kitabu hiki? Utakapoendelea kusoma kitabu hiki, kumbuka maana ninayotumia wakati ninaandika ili uweze kuelewa ujumbe wa kitabu hicho.

Tuangalie zaidi neno “Wokovu”. Maneno muhimu katika ufafanuzi wangu ni “ushirikiano” na “kurejeza”. Watu wengine wanafikiri Mungu anataka kutuokoa kwa sababu ya thamani tuliyo nayo sisi. Lakini katika kitabu hiki tutaonesha jinsi wokovu unahusu zaidi jinsi Mungu anavyostahili kuabudiwa. Yaani wokovu unahusu thamani ya Mungu kuliko thamani ya wanadamu.

Maneno “ushirikiano na Mungu” yanaonesha kusudi la wokovu. Mungu aliumba wanadamu waishi wakiwa na uhusiano naye milele. Ndiyo sababu anaokoa watu. Kuwemo katika ushirika na Mungu kunaanza siku ya kwanza mtu anapookolewa, hakusubiri mtu afike mbinguni. Tutajifunza maana ya kuwa na ushirika na Mungu na jinsi tokeo moja la kuokoka ni hamu ya kuwa na ushirikiano huo.

Mwishoni, neno “kurejeza” linatuonesha kwamba kulikuwa wakati wanadamu walikuwa katika uhusiano mzuri na Mungu, lakini ushirikiano ule ulivunjwa. Tutaona jinsi uhusiano ule ulivyoharibiwa na jinsi Mungu alivyoshughulika ili aurejeze. Pia tutaona jinsi uhusiano huu uliorejezwa, utakavyodumu milele.

# 1. Habari ya Wokovu Ulianzaje?

Ujumbe wa wokovu unaanza na Mungu. Ni muhimu tuanze na Mungu kwa sababu wale wanaotaka kuokolewa lazima waamue kama wanataka kuwa na uhusiano na Mungu wakimwabudu au la.

Mstari wa kwanza wa Biblia unaanza kwa kusema, *“Hapo mwanzo…”* (Mwa 1:1). Tunajifunza kutoka maneno haya mawili kwamba kila kitu kina mwanzo wake. Vitu vinavyoonekana na hata vitu visivyoonekana vilikuwa na mwanzo. Kabla ya mwanzo huo hapakuwa mbingu, wala dunia, wala cho chote katika dunia. Watu wanahitaji vitu katika dunia hii ili waishi, kwa hiyo, hata watu hawakuwepo wakati hapakuwa dunia. Vizazi vilivyotutangulia havikuwepo wakati huo kabla ya mwanzo na hata malaika na pepo hawakuwepo.

Mwanzo 1:1 unaendelea ukisema, *“Hapo mwanzo Mungu…”* Hapo mwanzoni, wakati Mungu bado hajaumba kitu, wakati hapakuwa watu wala viumbe vya roho, kitu kimoja tu kilikuwepo. Yaani Mungu peke yake alikuwepo. Biblia ni wazi kwamba Mungu alikaa peke yake kabla ya mwanzo. Hapakuwapo hata miungu mingine. Biblia inafundisha kuhusu Mungu kwamba kuna Mungu mmoja tu (Kum 6:4). Mungu anasema katika Isaya 45:5, *“Mimi ni BWANA, wala hapana mwingine; zaidi yangu mimi hapana Mungu!”* Miungu yote mingine ya watu wengine ni sanamu tu na siyo miungu ya kweli (Zab 96:5).

Tukiendelea kusoma Mwanzo 1:1 tunaona yale Mungu aliyoyafanya hapo mwanzo: *“Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi.”* Jambo la pili tunalojifunza kuhusu Mungu ni kwamba yeye ndiye mwumbaji wa vitu vyote. Wakati Mungu alipoumba mbingu, aliumba vilevile vitu vyote vilivyomo mbinguni. Hapo mwanzo Mungu aliumba hata malaika. Pia Mungu aliumba dunia yetu na kila kitu ndani yake kama vile: wanadamu, wanyama, miti, mito, n.k. (Mwa 1:1-2:3).

Mungu ni mkuu kuliko viumbe vyake vyote (Zab 135:5). Anatawala juu ya vyote alivyoviumba (Zab 103:19), ikiwa ni pamoja na wanadamu, Shetani, malaika, na pepo (tazama mchoro #1).

Copyright © 2017 GMI Publications




***Mchoro #1.*** *Mungu anatawala viumbe vyote. Katika mchoro huu utawala wa Mungu ni juu ya vitu vyote vilivyo ndani ya mstatili.*


Mungu ni mwenye uweza wote. Ndiyo maana aliweza kuumba vitu vyote (Yer 32:17). Hakuna jambo lisilowezekana kwake Mungu. Aliumba yote aliyoyataka. Mungu ana uwezo na nguvu kuliko viumbe vyake vyote. Hakuna kitu kilichoumbwa chenye nguvu au mamlaka kuliko Mungu. Hata Shetani hana nguvu au mamlaka kuliko Mungu.

Kwa nini Mungu aliumba viumbe vyote? Mungu aliumba vitu vyote ili atukuzwe yeye (Isa 43:7a; Zab 148:1-13). Zaidi, Mungu aliwaumba wanadamu na malaika wamtumikie (Kut 20:3-5a; Heb 1:14). Makusudi makuu mawili ya Mungu kuumba wanadamu na malaika ni kumtukuza na kumtumikia Mungu.

Siku moja, malaika mmoja aliyeitwa "Nyota ya Alfajiri" (au Lucifer, yaani Shetani) alikuwa na kiburi na hamu ya kutawala kama Mungu atawalavyo; alitaka kuwa sawa na Mungu. Alifikiri ataweza kumshinda Mungu na kuingilia mamlaka yake. Malaika wengi walimwunga mkono Shetani na kwa pamoja walimwasi Mungu wakimpiga vita. Lakini hawakuweza kumshinda mwenyezi Mungu. Mungu aliwatoa mbinguni wakae sehemu za duniani (Eze 28:14-16). Na pia Mungu aliandaa mahali pa adhabu ya milele kwa ajili ya Shetani na wote watakaomfuata katika kutomtii Mungu; mahali panapoitwa jehanamu.

Kuanzia wakati "Nyota ya Alfajiri" alipomwasi Mungu ndipo alianza kuitwa Shetani. Maana ya jina hilo ni "adui". Shetani ni adui mkuu wa Mungu. Shetani hampendi Mungu na hapendi yote Mungu anayopenda. Ndiyo maana Shetani hapendi wanadamu kwa sababu Mungu anawapenda. Makusudi ya Shetani ni kupiga vita mapenzi yote ya Mungu hata kuangamiza wanadamu wote wanaopendwa na Mungu.

Tangu Shetani alipomwasi Mungu kumekuwa tawala mbili na falme mbili za kiroho. Mungu ndiye mtawala mkuu na mwenye haki kutawala mambo yote. Shetani ni mtawala mdogo anayetawala wale tu wanaomkubali na kumfuata (tazama mchoro #2). Malaika waliomfuata Shetani katika uasi wake wanaitwa pepo wachafu. Shetani hakuridhika kutawala pepo wake tu bali alitaka kutawala wanadamu pia. Tutaona jinsi alivyotaka kuwatawala katika sehemu inayofuata.





***Mchoro #2.*** *Mungu bado anatawala juu ya vitu vyote. Ndiyo maana vyote vimo ndani ya mstatili wa utawala wake. Shetani alipewa ruhusa kutawala juu ya wale wanaochagua kumfuata badala ya kumfuata Mungu. Mstatili mdogo ni mfano wa utawala wake ulio ndani ya utawala wa Mungu.*

## 2. Kwa Nini Wanadamu Wanahitaji Kuokolewa?

Kujibu swali hilo tutaanza kwa kumchunguza mwanadamu wa kwanza, Adamu, na jinsi alivyokuwa mwanzoni. Wakati Adamu alipoumbwa alikuwa na ushirikiano na Mungu, yaani uhusiano mzuri. Alikuwa mkamilifu; hakuwa na kosa lo lote. Alikuwa hai kiroho na alikuwa chini ya utawala wa Mungu (tazama mchoro #3). Mungu alidai utiifu wa Adamu ili Adamu aendelee katika uhusiano na Mungu. Mungu alimwonya Adamu kwamba kutotii kutaleta adhabu. Mwanzoni Adamu alimtii Mungu na al-

iendelea kuwa na ushirikiano na Mungu. Wakati huo Adamu alikuwa akitimiza makusudi mawili ya Mungu kumwumba Adamu; Adamu alimtukuza na kumtumikia Mungu.




***Mchoro #3.*** *Adamu aliumbwa kuishi katika ushirika na Mungu akiwa chini ya utawala na Mungu.*

Wakati huo, Shetani alitaka kuwa mtawala wa Adamu. Alijua kama atafaulu kumshawishi Adamu kumtii yeye badala ya kumtii Mungu, uhusiano wa Adamu na Mungu utavunjika na Adamu atahamia chini ya utawala wa Shetani. Hivyo siku moja Shetani alimwendea Hawa (mke wa Adamu) akiwa na kusudi la kumjaribu (Mwa 3:1-5). Adamu alichagua kumtii Shetani na kutomtii Mungu (Mwa 3:5-6). Uasi wa Adamu ulisababisha mabadiliko mabaya katika maisha yake. Alipata kuwa mwenye dhambi na matokeo yake alikufa kiroho, alitenganishwa na Mungu, na alihamia chini ya utawala wa Shetani (tazama mchoro #4). Aliacha kuishi kwa makusudi ya Mungu ya kuumbwa wake. Badala yake aliishi katika hali ya kujitukuza na kumtumikia Shetani akiendelea katika dhambi zake.




***Mchoro #4.*** *Mchoro huu ni mfano wa mabadiliko makubwa mawili katika maisha ya Adamu yaliyosababishwa na dhambi yake. Kwanza yeye ni mfu kiroho, jambo ambalo linaoneshwa na Adamu kulazwa. Pili yumo ndani ya mstatili wa utawala wa Shetani ambalo linaonesha kwamba yuko chini ya utawala wa Shetani.*

Baada ya Adamu kutenda dhambi, hitaji lake kuu lilikuwa nini? Hitaji lake kuu lilikuwa ushirikiano wake na Mungu urejezwe ili aweze kuishi tena katika makusudi ya Mungu kwa ajili ya maisha yake. Ili aweze kuhusiana tena na Mungu alihitaji kufanywa tena mkamilifu, alihitaji kufanywa hai kiroho, alihitaji kuokolewa kutoka katika utawala wa Shetani na kurudishwa chini ya utawala wa Mungu, na mwisho alihitaji mshahara au adhabu ya dhambi yake kushughulikiwa. Mahitaji hayo yote yanatimizwa katika wokovu.

Sisi sote ni wazao wa Adamu, na kwa sababu hiyo sisi sote tumerithi asili yake ya dhambi. Vilevile sisi ni watenda dhambi (Rum 5:12). Wote, tulizaliwa tukiwa tumetenganishwa na Mungu kiroho, tena tukiwa chini ya hukumu Yake na pia chini ya utawala wa Shetani. Sawa na hitaji la Adamu, hitaji kuu la kila mwanadamu ni nini? Hitaji letu kuu, sisi sote, ni kutengeneza uhusiano wetu na Mungu tukiingia tena katika ushirika naye ili tuweze kuishi kufuatana na makusudi Yake kwa ajili ya maisha yetu na kukwepa hukumu zake.

Sasa tuangalie kwa undani zaidi maana ya sisi kuwa wenye dhambi na uharibifu wake mkubwa katika maisha yetu.

Watu wengi wanadhani kuwa mwenye dhambi siyo jambo baya sana. Mara wanatamka, "Ndivyo tulivyo tu", au "Ni shida lakini siyo shida kubwa." Lakini watu hawa wanakosea. Biblia inasema kuwa mwenye dhambi ana shida kubwa sana iletayo adhabu milele na milele. Sasa tuangalie jinsi Biblia inavyoeleza hali ya wenye dhambi.

## A. Mwenye Dhambi ni Mfu Kiroho

*Waefeso 2:1-2 - "Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi"*

Copyright © 2017 GMI Publications

*Wakolosai 2:13 – "Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote"*

Tangu Adamu alipomwasi Mungu, yeye na wazao wake wote wamekufa kiroho; yaani wametengwa na Mungu. Kila mtu amerithi asili ya dhambi (Rum 5:12) na kuzaliwa mfu kiroho. Kwa nini Biblia inalitumia neno "wafu" kuielezea hali yetu mbele ya Mungu? Je, unaweza kuwa na uhusiano na maiti? Hapana! Je, unaweza kuwa na urafiki gani na maiti? Hamna! Je, maiti inaweza kufanya nini ili ikupendeze? Haiwezi! Je, kama mtu alikukosea alipokuwa hai, afanye nini ili asuluhishe kosa lake nawe akiwa maiti (baada ya kufa)? Hakuna cha kufanya! Hiyo ndiyo picha ambayo Mungu anataka kutupatia kuhusu hali yetu mbele yake. Kwa sababu sisi tumerithi asili ya dhambi na kuzaliwa tukiwa wafu kiroho, hatuwezi kufanya cho chote kumpendeza Mungu, wala kujipatanisha na Mungu, wala kuitafuta suluhu ya makosa yetu mbele ya Mungu.

Aliye mfu kiroho anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kuhuishwa, yaani, kufanywa tena hai kiroho.

Je, mtu aliye mfu kiroho anaweza kujihuisha awe hai kiroho? Hapana kwa kuwa hana uwezo huo kama maiti.



***Mchoro #5**. Kaburi hili ni mfano wa jinsi mwenye dhambi ni mfu kiroho asiyeweza kufanya cho chote kumpendeza Mungu wala kutengeneza uhusiano wake na Mungu.*

## B. Mwenye Dhambi ni Chini ya Utawala wa Shetani

*1 Yohana 5:19 – "Tunajua kwamba sisi ni wake Mungu ingawa ulimwengu wote unatawaliwa na yule Mwovu." (BHN)*

Adamu alipomwasi Mungu kwa kuufuata ushauri wa Shetani, alijiweka chini ya mamlaka ya Shetani (tazama mchoro #6). Shetani ni mtawala wa ulimwengu huu (Yoh 14:30; 16:11). Shetani ni mdanganyifu asiyependa wanadamu. Anawatakia mateso, hofu, hata kifo. Mara anatumia nguvu zake kuwalaani watu na kusababisha matatizo katika maisha yao. Mara anatumia uwezo wake kuwasaidia, kwa mfano katika kuponya magonjwa. Lakini Shetani hana nia ya kusaidia wanadamu. Anapomsaidia mwanadamu, daima ana kusudi la kutaka kumvuta mbali na Mungu ili amtegemee Shetani kuliko Mungu. Nia yake ni uharibifu wa mwanadamu huyu kwa kuwa mwisho wa kumtegemea Shetani ni kuangamia.

Mtu aliye chini ya utawala wa Shetani anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kuondolewa kutoka chini ya utawala wa Shetani.

Je, mtu aliye mfu kiroho anaweza kumshinda Shetani na kujiweka huru naye? Hapana kwa kuwa mfu hana uwezo.

***Mchoro #6**. Kama Adamu, wote wanaotenda dhambi ni wafu kiroho na wako chini ya mamlaka ya Shetani.*

## C. Mwenye Dhambi ni Adui wa Mungu

*Warumi 5:10 – "Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake."*

Shetani ni adui wa Mungu, na tunapokuwa katika ufalme wa Shetani, chini ya mamlaka yake, nasi pia tunakuwa maadui ya Mungu.

Adui wa Mungu anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kupatanishwa na Mungu.

Mtu aliye mfu kiroho, aliye chini ya utawala wa Shetani, aliye adui wa Mungu, anaweza kufanya nini ili ajipatanishe na Mungu? Hakuna analoweza kufanya.

## D. Mwenye Dhambi ni Mtumwa wa Dhambi


*Yohana 8:34 – "Yesu akawajibu, 'Kweli nawaambieni, kila mtu anayetenda dhambi ni mtumwa wa dhambi.'"*

*Warumi 6:6 – "Tunajua kwamba utu wetu wa kale ulisulubiwa pamoja na Kristo, ili hali ya dhambi iharibiwe, tusiwe tena watumwa wa dhambi."*

Sisi sote, wenye dhambi, tunakuwa chini ya utawala wa Shetani, na pia tunakuwa watumwa wa dhambi. Hivyo, hata dhambi inatutawala (tazama mchoro #7). Hatuwezi kufanya cho chote ila kuwatii watawala wetu Shetani na dhambi.

Mtu aliye mtumwa wa dhambi anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kuwekwa huru na utumwa wake.

Je, Mtu aliye mfu kiroho na adui wa Mungu ambaye naye ni mtumwa wa dhambi na Shetani, anaweza kujiweka huru? Hapana




***Mchoro #7.*** *Wafu kiroho wenye dhambi ni watumwa wa Shetani na wa dhambi, hali hii inaoneshwa na minyororo katika mchoro huu. Hawana uwezo kujiweka huru.*

## E. Mwenye Dhambi ni Mtumwa wa Utu wa Kale (yaani "Mwili" au tamaa za dhambi)

*Warumi 6:6 – "Mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."*

*Warumi 7:5 – "Kwa maana tulipokuwa katika hali ya mwili, tamaa za dhambi, zilizokuwako kwa sababu ya torati, zilitenda kazi katika viungo vyetu hata mkaizalia mauti mazao."*

*Warumi 8:5, 8, 9 – "Kwa maana wale waufuatao mwili huyafikiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho…Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu…Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."*

Wenye dhambi wanatawaliwa na udhaifu wa miili yao. Miili yao inawafanya wawe watumwa wa dhambi. Biblia inatumia maneno haya kutuonesha hali yetu halisi kabla hatujaokoka. Tulikuwa wafu kiroho. Tulitawaliwa na utu wa kale (au mwili) uliotufanya kuwa watumwa wa dhambi.

Mtu anayetawaliwa na mwili wake wa dhambi anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kuwekwa huru na utawala wa mwili wake (au utu wake wa dhambi).

Mtu aliye mfu kiroho, aliye adui wa Mungu, aliye mtumwa wa dhambi, Shetani, na hata mwili wake wa dhambi anaweza kujiweka huru? Haiwezekani.

## F. Mwenye Dhambi Yuko Chini ya Ghadhabu na Hukumu ya Mungu

*Yohana 3:18 – "Amwaminiye yeye hahukumiwi; asiyeamini amekwisha kuhukumiwa; kwa sababu hakuliamini jina la Mwana pekee wa Mungu."*

*Yohana 3:36 – "Amwaminiye Mwana yuna uzima wa milele; asiyemwamini Mwana hataona uzima, bali ghadhabu ya Mungu inamkalia."*

Kwa sababu tumemkosea Mungu, tuko chini ya ghababu na hukumu yake. Hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi ni nini? Hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi ni kifo, yaani kutenganishwa na Mungu milele (Rum 6:23). Hatuna njia ya kujitoa kutoka chini ya ghadhabu na hukumu ya Mungu.

Mtu aliye chini ya ghadhabu na hukumu ya Mungu anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kutuliza ghadhabu ya Mungu na kukwepa hukumu Yake.

Mtu aliye mfu kiroho, aliye adui wa Mungu, aliye mtumwa wa dhambi na wa Shetani, anaweza kufanya nini ili atulize ghadhabu ya Mungu na hukumu Yake? Hana uwezo wa kufanya cho chote.

## G. Mwenye Dhambi Yuko Chini ya Laana ya Sheria

*Wagalatia 3:10 – "Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye."*

Sheria ya Mungu inaonesha kiwango kikamilifu cha Mungu. Watu wote wamepungukiwa kulingana na kiwango hicho kwa kuivunja angalau amri moja ya Mungu. Kwa sababu hiyo wote wako chini ya laana ya sheria. Laana hiyo ni hukumu ya Mungu milele.

Mtu aliye chini ya laana ya kipimo na sheria za Mungu anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kukombolewa na laana ya sheria ya Mungu.

Je, mtu aliye mfu kiroho, aliye adui wa Mungu, aliye mwenye dhambi iletayo laana ya sheria anaweza kufanya nini ili ajikomboe na tatizo hilo? Hanacho cha kufanya.

**H. Mwenye Dhambi ni Mchafu Machoni pa Mungu**

*Isaya 64:6 – "Kwa maana sisi sote tumekuwa kama mtu aliye mchafu, na matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi; sisi sote twanyauka kama jani, na maovu yetu yatuondoa, kama upepo uondoavyo."* Dhambi zetu zimetuchafua mbele ya Mungu. Mungu mtakatifu hawezi kuwa na ushirikiano na kitu kichafu. Dhambi zetu zinatuchafua kabisa hadi matendo yetu mema yamechafuliwa na dhambi. Tena uchafu huo hutufanya tusiwe na uwezo wo wote wa kumkaribia Mungu na kuwa na ushirika naye. Ndiyo maana Isaya anasema matendo yetu mema yamekuwa kama nguo chafu.

Mtu aliye mchafu machoni pa Mungu anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kusafishwa au kutakaswa.

Je, mtu aliye mfu kiroho, aliye adui wa Mungu, aliye mtumwa wa dhambi, Shetani na Mwili wake wa dhambi, anaweza kujitakasa? Hawezi.

**I. Mwenye Dhambi Ametenganishwa na Kristo**

*Waefeso 2:12 – "Kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo, mmefarakana na jamii ya Israeli, wageni wasio wa maagano ya ahadi ile. Mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani"*

Kutenganishwa na Kristo ina maana kutokuwa na ushirika au uhusiano naye. Ina maana mtu huyu anakuwa chini ya hukumu ya Mungu. Wenye dhambi wote wametenganishwa na Kristo.

Mtu aliyetenganishwa na Kristo anahitaji nini ili aokolewe? Anahitaji kuunganishwa na Kristo.

**J. Mwenye Dhambi Hana Tumaini** (Efe 2:12)

Kwa sababu tulizaliwa wafu kiroho, chini ya utawala wa Shetani, tukiwa watumwa wa dhambi, na adui za Mungu, tena chini ya laana na ghadhabu Yake, kweli, hatuna tumaini hata kidogo la kujiokoa.

Mtu asiye na tumaini la kujiokoa anahitaji nini? Anahitaji tumaini litokalo kwa Mungu.

***Kwa nini wanadamu wanahitaji kuokolewa?***

Tunahitaji wokovu kwa sababu sisi sote tulizaliwa tukiwa wenye dhambi, wafu kiroho, na katika hali ya kutenganishwa na Mungu. Vilevile tunahitaji wokovu kwa sababu mwenye dhambi ni adui wa Mungu aliye chini ya ghadhabu na hukumu ya Mungu. Zaidi, mwenye dhambi yuko chini ya utawala wa Shetani, wa dhambi, na wa mwili wake wa dhambi. Yeye ni mchafu aliyetenganishwa na Kristo na wala hana uwezo wala tumaini la kuweza kujiokoa.

Haya ni matatizo makubwa sana. Wenye dhambi wanahitaji nini? Wanahitaji matatizo hayo yote yatatuliwe. Wanahitaji kuhuishwa kuwa hai kiroho, wanahitaji kupatanishwa na Mungu, wanahitaji kukombolewa na laana ya sheria za Mungu, na wanahitaji kukwepa hukumu ya Mungu. Zaidi wanahitaji kuokolewa na utumwa wao kwa Shetani, dhambi, na miili yao ya dhambi. Wanahitaji kutakaswa na kuunganishwa na Kristo. Tutaona katika kitabu hiki kwamba matatizo hayo yote yanatatuliwa na wokovu wa kweli unaopatikana katika Kristo.

# 3. Kwa Nini Wenye Dhambi Hawawezi Kujiokoa?

Katika mahusiano kati ya watu ni kawaida kwa mmoja kumkosea na kumwumiza mwenzake. Inapotokea, mahusiano yanapata shida, na mara nyingine yanavunjika. Kama aliyemwumiza mwenzake anataka kupatanishwa naye, kawaida atamwendea na kuomba msamaha na kama kuna kitu cha kufidia atatekeleza matakwa hayo.

Watu wengine wanafikiri wanaweza kutengeneza uhusiano wao na Mungu kwa njia hiyo hiyo. Kwa mfano, wakiona shida ni dhambi wanazozitenda, wataomba msamaha kwake Mungu na kujitahidi kutozitenda tena. Pengine wakiona wamevunja sehemu ya sheria ya Mungu, wataomba msamaha na kujitahidi katika kutii sheria hiyo. Yaani wakiona shida kati yao na Mungu ni matendo yao mabaya, wataomba msamaha na kujaribu kurekebisha matendo yao yawe matendo mema.

Je, tunaweza kutengeneza uhusiano wetu na Mungu kwa njia hii? Hapana. Hakuna tunachoweza kufanya kutengeneza uhusiano wetu na Mungu. Kwa maneno mengine – hatuwezi kujiokoa. Labda utau-

liza, "Ikiwa Mungu anatuagiza kusamehe wengine wanapoomba msamaha, je, kwa nini Mungu hatatusamehe sisi tunapomwomba msamaha?" Majibu yetu ni haya yafuatayo:

## A. Wenye Dhambi Hawawezi Kujiokoa kwa Sababu Wenyewe ni Wafu Kiroho.

Tulishaongea jambo hilo sana. Ukweli ni kwamba shida ya wenye dhambi ni shida ya kiroho ambayo inahitaji jibu la kiroho. Kwa sababu wenye dhambi ni wafu kiroho ina maana hawawezi kufanya cho chote kujisaidia kama vile maiti haiwezi kujisaidia. Mfu kiroho hana uwezo wa kujihuisha kuwa hai. Lazima aliye hai amsaidie.

## B. Wenye Dhambi Hawawezi Kujiokoa kwa Sababu Mungu ni Mtakatifu.

*Isaya 6:3 –" Wakaitana, kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, ni BWANA wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake."*

Tunamaanisha nini tunaposema kwamba Mungu ni mtakatifu? Katika Biblia, neno "utakatifu" lina maana mbili:

***Utakatifu wa Mungu ni jinsi anavyojitenga na vilivyo vichafu***

Maana ya kwanza ya utakatifu wa Mungu ni: "Kutengwa (kuwa mbali) na vyote vilivyo vichafu au najisi." Maana hii ni muhimu kwa kuwa inahusika katika wokovu. Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, hawezi kuwa na ushirikiano na kiumbe cho chote kilicho kichafu au kisicho kitakatifu kikamilifu.

***Mungu mtakatifu hawezi kushirikiana na mwanadamu mchafu***

Tukiiangalia hali ya wanadamu, wanadamu wanazaliwa wakiwa na asili ya dhambi. Dhambi imetuchafua kabisa mbele ya Mungu. Hata matendo yetu ya haki ambayo mtu anaweza kudhani ni safi, yamechafuliwa na dhambi zetu (Isa 64:6). Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, hawezi kuwa na ushirikiano na mtu ye yote mchafu wala kumkubali mtu mchafu. Inambidi mtu ye yote anayetaka kukubaliwa na Mungu awe mtakatifu. Mwanadamu asiye na utakatifu kamili mbele za Mungu hawezi kukubaliwa na Mungu wala kuwa na tumaini lo lote la kuwa na ushirikiano na Mungu.

***Matendo mema ya mtu asiye mtakatifu hayawezi kumpendeza Mungu***

Mtu fulani akisema, "Nadhani nitaokolewa kwa sababu nimejitahidi kumpendeza Mungu", anaonesha wazi kwamba haelewi maana ya utakatifu wa Mungu. Mwanadamu anayejitahidi kumpendeza Mungu, au anayetenda matendo mema ili ampendeze Mungu, au anayeziacha dhambi, bado ni mchafu mbele ya Mungu kwa sababu ya dhambi zake alizozitenda tayari pamoja na asili yake ya dhambi. Mungu mtakatifu hawezi kushirikiana na mtu kama huyo.

***Mfano wa chombo cha alizeti kilichotiwa petroli***

Mfano unaofuata unaeleza kwa nini Mungu anatuona kuwa wachafu. Mtu fulani alitafuta chombo cha kuwekea mafuta ya alizeti. Alipata chombo ambacho ndani yake kulikuwa nusu lita ya petroli. Akasema, "Kuna nusu lita ya petroli tu, na nina lita 20 ya mafuta ya alizeti. Petroli haitaharibu kitu." Ni kweli? Hapana! Ingawa mafuta ya alizeti yanazidi sana kiasi cha petroli, wote tunafahamu kiasi kile cha petroli kitaharibu kweli mafuta yale. Vivyo hivyo na dhambi. Matendo mema mengi hayawezi kufuta matendo mabaya machache au hata tendo baya moja. Lakini je, akimwaga nusu lita ile na kuweka mafuta ya alizeti bila kusafisha chombo kile? Tena, wote tutakubali hata kama chombo kile ni tupu, kama kiliwahi kutunza petroli, kitaharibu mafuta yale ya alizeti. Hakuna atakayetaka kula mafuta hayo. Ndivyo ilivyo katika maisha yetu. Dhambi, hata moja tu, inachafua kabisa matendo yetu mema na maisha yetu mbele ya Mungu.

***Utakatifu wa Mungu ni wema wake kamili***

Maana ya pili ya utakatifu wa Mungu ni "wema kamili". Mungu hana kosa wala kasoro. Ndiyo hali ya Mungu na hali inayotakiwa kwa wote wanaotaka kushirikiana naye Mungu. Kama mtu anataka kushirikiana na Mungu anatakiwa kuwa mtakatifu; anatakiwa kuwa mtu aliyekamilika katika wema wake, yaani asiwe na kosa wala kasoro yo yote.

Lakini ni wazi kwamba kila mwanadamu analo angalau kosa moja. Hivyo hawawezi kuitwa "wema kamili" wala hawawezi kuitwa watakatifu.

***Kwa nini hatuwezi kujiokoa? kwa sababu mwanadamu hawezi kujifanya kuwa mtakatifu na Mungu hashirikiani na asiye mtakatifu***

Mungu aliye mtakatifu hashirikiani wala hawezi kumkubali kamwe mwanadamu asiye mtakatifu. Sisi ni wenye dhambi na hatuwezi kujifanya kuwa watakatifu kwa sababu dhambi zetu zimetuchafua kabisa. Hata haki zetu na matendo yetu mema ni najisi mbele ya Mungu. Hatuna tumaini la kujifanya kuwa watakatifu ili tujipatanishe na Mungu na kushirikiana naye. Hatuwezi kujiokoa.

**C. Wenye Dhambi Hawawezi Kujiokoa kwa Sababu Mungu ni Hakimu Mwenye Haki.**

*Zaburi 7:11 – "Mungu ni mwamuzi mwenye haki, Naam, Mungu aghadhibikaye kila siku."*

***Mungu ni mwenye haki***

Tunamaanisha nini tunaposema kwamba Mungu ni mwenye haki? Tunamaanisha kwamba yote Mungu anayoyawaza na kuyatenda ni sahihi. Tena tunamaanisha kwamba Mungu hawezi kulivumilia wala kuliachilia kosa lo lote wala uovu wo wote kwa kuwa ni lazima atende kwa usahihi na kwa haki. Mungu ataziadhibu dhambi zote. Mungu, mwenye haki, hawezi kusamehe dhambi kabla hazijaadhibiwa. Adhabu kwa ajili ya dhambi yo yote ni moja - ni mauti (yaani kutengwa na Mungu milele.)

Watu wengi wanajaribu kuhonga, kudanganya, au hata kuelewana na pepo, roho za mababu, au hata mahakimu kupata yale wanayoyataka. Lakini Mungu, aliye mwenye haki, hayuko kama hawa. Mungu, kama hakimu mwenye haki, hawezi kupokea hongo wala kushawishika kufanya cho chote kisicho haki. Daima Mungu atatenda haki (Kum 10:17).

***Mfano wa hakimu mwenye haki***

Tunajua hakimu mwenye haki anatakiwa kuwaadhibu wote walio na hatia kwa kuwa wamevunja sheria. Kwa mfano, Petro na Esau walifika mbele ya hakimu kutetea misimamo yao. Petro alileta mashtaka kwamba Esau aliiba ng'ombe wake. Baada ya kuwasikiliza mashahidi wote, hakimu aliamua kwamba Esau ana hatia na adhabu yake ni kulipa shilingi 70,000/=. Esau alianza kulia na kumsihi hakimu amhurumie kwa sababu mke wake alihitaji matibabu na hakuwa na hela ya kuyalipia matibabu yake. Hakimu akimhurumia Esau na kusema kwa sababu ya shida yake, asilipe adhabu yake, je, atakuwa ametenda haki? Hapana! Ni lazima hakimu mwenye haki amwadhibu mwenye hatia. Ndiyo maana ya mfano huu, kama Esau ni mwenye hatia, hana budi ila kuhukumiwa na hakimu huyu ili haki itendeke.

***Haki ya Mungu inamlazimisha kuhukumu hata yule mwenye kosa moja tu***

Watu wengine wanadhani wanaweza kumwomba Mungu ayaangalie matendo yao mema na kuyasamehe makosa yao madogo madogo. Yaani wanataka wapimwe kwenye mizani wakiweka matendo mema upande mmoja na matendo mabaya upande wa pili. Wanadhani kama matendo mema yatazidi yaliyo mabaya, wanastahili kusamehewa. Mawazo haya hayalingani na haki ya Mungu. Mtu akimwomba Mungu kusamehe hata kosa moja bila adhabu, anaomba Mungu asitende haki. Mungu anaweza kukubali kutenda kisicho haki? Haiwezekani! Mawazo haya yatawafanya watu watupwe motoni kwa sababu Mungu ataiadhibu hata dhambi ndogo moja. Na je, adhabu ya dhambi moja ndogo ni nini? Jibu ni mauti; yaani kutengwa na Mungu milele kwenye adhabu.

Isitoshe, Mungu anasema katika Yakobo 2:10, *"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote."* Pengine wewe na mimi tungeweza kumsamehe mtu aliyekosea sheria moja tu (ingawa kufanya hivyo kusingekuwa haki). Lakini wote tungekubali kwamba mtu aliyevunja kila sheria anastahili adhabu. Ndivyo Mungu anavyoona makosa yetu hata moja. Kukosa mara moja tu, machoni pa Mungu, ni sawa na kuvunja sheria zake zote.

***Kwa nini hatuwezi kujiokoa?***

Kwa sababu Mungu mwenye haki ataziadhibu dhambi zote. Hatatuhurumia sisi wenye dhambi bila dhambi zetu zote kuadhibiwa. Sisi hatuwezi kufanya cho chote cha kujitetea mbele ya Mungu hata kama tumetenda matendo mengine mema. Sababu ni kwamba adhabu ya dhambi, hata moja ndogo, ni kutengwa na Mungu milele. Matendo mema hayafuti dhambi zetu wala adhabu yake. Hatuwezi kujiokoa!

# 4. Kwa Nini Sheria Haiwezi Kutuokoa?

Watu wengine wanadhani Mungu alitoa sheria yake ili watu waokolewe kwa kuitii. Lakini hii siyo sababu ya Mungu kutoa sheria yake. Sheria haina uwezo wa kuokoa. Tuone kwa nini sheria haiwezi kuokoa.

Copyright © 2017 GMI Publications

Sheria ya Mungu ni kipimo kamili ambacho Mungu atumia kupima wema wa watu. Sheria inaonesha mtu jinsi anavyopaswa kuishi ili akubaliwe na Mungu. Ili mtu akubaliwe na Mungu kupitia sheria, mtu huyu atalazimika kutimiza sheria zote za Mungu wakati wote. Lakini, hakuna mtu anayeweza kufanya hivyo. Kuanzia Adamu hadi leo, hakuna mwandamu, hata mmoja, aliyetimiza kikamili sheria ya Mungu isipokuwa Yesu Kristo tu.

## A. Sheria Ina Kusudi Gani Basi?

Kama wanadamu hawawezi kujiokoa kwa kutii sheria, je, kwa nini Mungu alitoa sheria yake? Tutaona kwa nini Mungu aliwafahamisha wanadamu sheria zake kwa kusoma maelezo ya Mungu katika Biblia.

***Kusudi la sheria ni kuonesha dhambi iwe wazi***

*Warumi 3:20 – "Kwa sababu hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki mbele zake kwa matendo ya sheria; kwa maana kutambua dhambi huja kwa njia ya sheria."*

*Warumi 7:7 – "Tusemeje, basi? Torati* (torati ni sheria) *ni dhambi? Hasha! Walakini singalitambua dhambi ila kwa sheria; kwa kuwa singalijua kutamani, kama torati isingalisema, Usitamani".*

Sheria haina kusudi la kuondoa dhambi, bali kuonesha dhambi ilipo. Kwa kawaida asiye Mkristo hajui yeye ni mwenye dhambi mbele za Mungu. Kazi ya sheria ni kumwonesha mtu kama huyu kwamba yeye kweli ni mwenye dhambi kwa kuwa matendo yake ni kinyume na mapenzi ya Mungu.

***Kusudi la sheria ni kunyamazisha watu mbele ya Mungu ili wasiweze kujitetea***

*Warumi 3:19 - "Basi twajua ya kuwa mambo yote inenayo torati huyanena kwa hao walio chini ya torati, ili kila kinywa kifumbwe, na ulimwengu wote uwe chini ya hukumu ya Mungu"*

Watu wengine wanadhani kwamba katika siku ya hukumu watamwomba Mungu awahurumie kwa sababu hawakufanya dhambi zilizo mbaya sana au kwa sababu matendo yao mema yalizidi matendo yao mabaya. Lakini watu hawa wamekosea katika mawazo yao kwa sababu Warumi 3:19 inadai hawataweza kujitetea; yaani hata kufungua kinywa chao hawatafanya. Sababu ni kwamba sheria itaonesha dhambi zao zote. Watajiona wenye hatia kweli kweli na wataona hakuna haja kujaribu kujitetea.

***Kusudi la sheria ni kuleta ghadhabu ya Mungu***

*Warumi 4:15 – "Kwa sababu sheria ndiyo ifanyayo hasira; maana pasipokuwapo sheria, hapana kosa."*

Zaidi ya kuwa chini ya hukumu tu, wote wanaovunja sheria za Mungu wako chini ya ghadhabu yake vilevile. Wote walio chini ya ghadhabu ya Mungu watatupwa katika ziwa la moto.

***Kusudi la sheria ni kuhukumu***

*Warumi 2:12 – "Kwa kuwa wote waliokosa pasipo sheria watapotea pasipo sheria, na wote waliokosa, wenye sheria, watahukumiwa kwa sheria."*

*Yakobo 2:10 – "Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja, amekosa juu ya yote."*

Ye yote atakayeweza kutimiza sheria zote za Mungu atahesabika kuwa haki mbele ya Mungu. Lakini wale wanaofanya hata kosa moja watahukumiwa na sheria hiyo. Hukumu ya kutotii sheria, hata moja, ni nini? Ni mauti ya milele. Sheria inatuhukumu sisi sote kwa sababu hakuna hata mwanadamu mmoja kati yetu anayeweza kutii kila sheria ya Mungu kila wakati.

***Sheria ya Mungu inalaani***

*Wagalatia 3:10 – "Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, Amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye."*

Sheria ya Mungu inaleta ghadhabu na hukumu, lakini pia inaleta laana kwa wote watakaoshindwa kutimiza sheria zote kikamili. Je, laana ya sheria ni nini? Laana ya sheria ni mauti.

***Sheria inaua***

Copyright © 2017 GMI Publications

*2 Wakorintho 3:6 – "Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko, bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha."*

Sheria inaua kwa kuwa ye yote atakayevunja hata sheria moja anahukumiwa na mauti ya milele. Ina maana sheria inatuhukumu sisi sote kufa kwa kuwa wote tumevunja angalau sheria moja (Rum 3:23).

***Sheria inatuongoza kwa Kristo***

*Wagalatia 3:23-24 – "Lakini kabla ya kuja ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa. Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani."*

Mungu anasema wazi katika Wagalatia 3:23-24 kwamba alitoa sheria yake ili itumike kama chombo cha kuleta watu kwa Kristo.

Tuseme, kwa mfano, una shida na anayeweza kukusaidia ni Mkuu wa Mkoa. Unafanya safari ya kwenda mkoani lakini hujui Mkuu wa Mkoa anakaa wapi. Ukipata mtu wa kukuongoza hadi ofisi ya Mkuu wa Mkoa, je, mtu huyu ana uwezo wa kutatua shida yako? Hapana. Kazi yake ni kukuonesha mahali pa yule anayeweza kukusaida. Baada ya kukuonesha mahali Mkuu wa Mkoa alipo, kazi yake imeisha.

Hii ndiyo kazi ya sheria ya Mungu. Sheria ya Mungu haiwezi kutusaidia na shida yetu ya dhambi. Yaani, haiwezi kutuokoa. Lakini kazi yake ni kutuongoza. Kwanza inatuongoza kuelewa na kukubali shida ya dhambi tuliyo nayo. Bila kutambua tunayo shida, hatuwezi kutafuta tiba ya shida hiyo. Pili inatuongoza kwa Yesu Kristo kwa kuwa yeye ndiye mwenye jibu la shida yetu. Tukishachoka katika kujaribu kujiokoa kupitia sheria, tutakuwa tayari kupokea zawadi ya Mungu kumpitia Yesu Kristo.

## B. Mambo Ambayo Sheria Haiwezi Kuyafanya

- Sheria ya Mungu haiwezi kutuhesabu haki mbele ya Mungu (Rum 3:21, 9:30-33, Gal 2:15-16).
- Sheria haiwezi kuondoa dhambi (Heb 10:1-4).
- Sheria haiwezi kumfanya mtu awe hai (Gal 3:21).
- Sheria haiwezi kuokoa (Rum 8:3).


Katika mistari hii pamoja na mingine, Biblia ni wazi kwamba hakuna anayeweza kuokolewa kwa njia ya kutii sheria ya Mungu.

***Kwa nini sheria haiwezi kutuokoa?***

Sheria inaweza kuokoa tu wale wanaoweza kutii sheria ya Mungu asilimia mia. Wote wanaovunja hata sheria moja wanahukumiwa na sheria hiyo. Kwa sababu tunazaliwa na asili ya dhambi hatuwezi kutii sheria zote za Mungu bila kukosea angalau mara kwa mara. Kwa sababu hiyo, sheria inatuhukumu tu. Haiwezi kutuhesabu haki wala kutuokoa kwa sababu inatangaza sisi ni wavunja sheria. Ndiyo maana Biblia inasema katika Warumi 8:2-3, *"Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili…"* Shida siyo sheria ya Mungu. Sheria ya Mungu ni *"haki"*, *"takatifu"*, na *"njema"* (Rum 7:12). Ila shida ni udhaifu wa wanadamu na jinsi wasivyoweza kutii sheria ya Mungu kikamilifu.

Kuna mifano miwili hapo chini. Mifano hii inaonesha kwa nini sheria haiwezi kutuokoa.

***Mfano #1 – Gereza la nchi fulani duniani***





Picha hii inaonesha mtu ambaye hajavunja sheria yo yote katika nchi yake. Hivyo ni mwenye haki na anakaa huru nje ya gereza.

Copyright © 2017 GMI Publications





Picha hii inaonesha jinsi mtu huyu alivyoiba mbuzi wa mwingine, akakamatwa, na hakimu alimhukumu akae gerezani mwezi mmoja kama adhabu yake.




Baada ya mwezi mmoja kutimia mtu huyu alimaliza adhabu yake. Kumaliza adhabu yake kunamfanya ahesabike tena kuwa mwenye haki; yaani hana hatia sasa. Hivyo anaachwa huru nje ya gereza tena.

***Mfano #2 – Gereza la Mungu la milele***




Katika picha hii, mtu huyu yuko huru kwa kuwa hajavunja sheria yo yote ya Mungu. Maana yake ana uhusiano mzuri na Mungu na anapokelewa na Mungu.




Katika picha hii, mtu huyu alitenda dhambi moja. Aliiba mbuzi wa mwingine na Mungu mwenye maarifa yote aliona na kujua kuhusu dhambi hiyo. Mwisho, Mungu kama hakimu alimhukumu mtu huyu kulingana na sheria na kanuni yake. Kutokana na dhambi yake, na kulingana na udhaifu wake kama mwanadamu mwenye dhambi, mtu huyu analazimika kukaa gerezani milele kwa kuwa adhabu yake ni kubwa mno. Hawezi kumaliza deni lake, hivyo ataendelea kukaa gerezani na kuendelea kulipa milele.

Mtu huyu atatoka gerezani lini? Kamwe – yaani, hatatoka tena. Kwa nini? Kwa sababu hawezi kumaliza adhabu yake. Kwa kuwa adhabu ya kuvunja hata sheria moja ndogo ya Mungu ni mauti ya milele, ni lazima mtu huyu aadhibiwe milele. Ndiyo maana sheria haiwezi kuokoa. Hakuna anayeweza kutii kila sheria ya Mungu kila wakati. Hivyo sheria inamhukumu kila mtu kwa kuwa inaonesha mahali alipokosea mapenzi ya Mungu.

Copyright © 2017 GMI Publications

# 5. Basi, Tuna Tumaini Lo lote la Kuokolewa?

Tumeona kwamba sisi ni wafu kiroho na hatuwezi kujisaidia mbele ya Mungu. Tumeona kwamba Mungu ni mtakatifu na mwenye haki na hivyo hatashirikiana na mtu asiye mtakatifu, bali ataziadhibu dhambi zake. Basi, tuna tumaini lo lote la kuokolewa? Ndiyo!

***Tumaini = Upendo, Rehema, na Neema ya Mungu***

Tuna tumaini kwa sababu Mungu ni mwema. Tunamaanisha nini tunaposema kwamba Mungu ni mwema? Wema wa Mungu unaonekana kwa njia tatu. Njia hizi ni kupitia upendo wake, rehema yake, na neema yake. Upendo ni kumtakia mwingine wema katika maisha yake. Rehema ni kutowaadhibu wanaostahili adhabu. Neema ni kumtendea mtu kwa wema wakati anastahili kuadhibiwa.

Tunaposema kwamba Mungu ni mwema, tunasema kwamba Mungu katika upendo wake anataka kututendea vizuri. Katika rehema yake, hataki kutuadhibu. Katika neema yake, anataka kutusaidia ingawa tunastahili kuadhibiwa.

***Upendo wa Mungu***

*Yohana 3:16 – "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*

Upendo ni kumtakia mtu mwingine wema katika maisha yake, yaani mambo mazuri. Kwa mfano, Linus alifika shuleni lakini alikuwa amesahau daftari lake na mwalimu wake alimlazimisha kurudi nyumbani. Lakini Yakobo, rafiki wa Linus, hakutaka Linus arudishwe nyumbani. Hivyo Yakobo alimpa Linus daftari lake la akiba. Nia ya Yakobo kumsaidia Linus ilitokana na upendo wake kwa Linus. Kama tunavyoona katika mfano huu, upendo huoneshwa kupitia matendo.

Tunaposema Mungu ni pendo, tunamaanisha Mungu ana nia njema kwetu na anatutakia wema katika maisha yetu. Kutokana na msimamo huo anatuonesha upendo wake kupitia matendo yake.

***Rehema ya Mungu***

Rehema ni kutoadhibu mtu anayestahili kuadhibiwa. Kwa mfano siku moja mtoto anayeitwa Antonio alivunja kikombe cha baba yake wakati baba yake alikuwa shambani. Wakubwa wa Antonio walimwambia, "Baba atakaporudi tutamwambia na yeye atakupiga!" Antonio aliogopa kupigwa na babaye. Baba yake aliporudi, Antonio hakuenda kumsalimia pamoja na wakubwa wake. Wakubwa wake walimwambia baba yao jinsi Antonio alivyovunja kikombe kile. Baba yake, kwa hasira, alimwita Antonio aje. Antonio alianza kulia na akamwendea baba yake akikiri na kueleza jinsi alivyokosea. Mwishoni, baba yake akamhurumia na hakumpiga ingawa alistahili kuadhibiwa.

Tunaposema Mungu ni mwenye rehema tunamaanisha jinsi Mungu hataki tuadhibiwe na jinsi anavyotafuta njia kutusaidia kukwepa adhabu yake iliyo ya lazima. Ukweli ni kwamba tunapofanya kosa lo lote, siku ile ile Mungu angeweza kutuhukumu milele. Lakini Biblia inasema kawaida Mungu hatoi adhabu siku ile ile, bali anatuvumilia kutokana na wema na rehema yake (Rum 2:4). Anataka tupewe nafasi ya kutubu na kukubali wokovu wake ulio njia pekee ya kukwepa adhabu tunayostahili.

***Neema ya Mungu***

*Waefeso 2:8 – "Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu"*

Neema ni kumtendea mema mtu mwingine asiyestahili kutendewa mema. Kwa mfano mgonjwa aliye na vidonda kwenye miguu yake alienda kumwona daktari ili atibiwe. Daktari huyu alitibu na kufunga miguu ya mgonjwa huyo. Mgonjwa alipoondoka, aliona kaptura za daktari huyu zimeanikwa nje, akaziiba na kuondoka nazo. Kwa bahati, daktari huyu akawa ameona tendo hilo dirishani. Kesho yake mgonjwa huyu alirudi kutibiwa tena. Je, alistahili msaada wa daktari huyu? Hapana. Lakini daktari huyu aliendelea kumtibu ingawa mgonjwa huyu hakustahili wema wake. Badala yake alistahili adhabu. Daktari yule alipoendelea kumtibu bila kuita polisi, alikuwa akimwonesha neema mgonjwa huyu.

Tunapoongea kuhusu neema ya Mungu tunaongea kuhusu hali yake ya kututendea mema wakati tunastahili adhabu.

Hali hizo zote za Mungu, wema, upendo, rehema, na neema, zinafanya kazi ili mtu aokolewe. Tunaona hali hizo zote katika Waefeso 2:1-9 inayoongea jinsi tulivyopotea, jinsi tulivyokuwa chini ya hasira ya Mungu, na jinsi wema, upendo, rehema, na neema ya Mungu zilivyotupa tumaini la kuokolewa.

*Waefeso 2:1-9 – "Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu; ambazo mliziendea zamani kwa kuifuata kawaida ya ulimwengu huu, na kwa kumfuata mfalme wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa kuasi; ambao zamani, sisi sote nasi tulienenda kati yao, katika tamaa za miili yetu, tulipoyatimiza mapenzi ya mwili na ya nia, tukawa kwa tabia yetu watoto wa hasira kama na hao wengine. Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa* ***REHEMA****, kwa mapenzi yake makuu aliyotu****PENDA****; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa* ***NEEMA****. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho, katika Kristo Yesu; ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa* ***NEEMA*** *yake upitao kiasi kwa* ***WEMA*** *wake kwetu sisi katika Kristo Yesu. Kwa maana mmeokolewa kwa* ***NEEMA****, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu."*

Kwa sababu Mungu ni mwema, pendo, mwenye neema na rehema, anatujali na anataka tusiadhibiwe kwa ajili ya dhambi zetu. Lakini Mungu ni hakimu mwenye haki vilevile. Kwa sababu hiyo analazimika kuhukumu na kutoa adhabu kwa mwenye dhambi. Akifuta adhabu yao tu, atakuwa hajatenda haki – hali isiyowezekana kwa Mungu.

***Mfano wa Petro, Esau, na Hakimu***

Unakumbuka hadithi ya Petro na Esau? Hadithi hiyo inaweza kutuonesha namna Mungu anavyoweza kutuhurumia, na wakati huo huo, aziadhibu dhambi zetu. Tukumbuke kwamba hakimu aliamua kwamba Esau aliiba ng'ombe na alipaswa kulipa 70,000/= kama adhabu yake. Esau aliomba ahurumiwe kwa sababu ya shida ya mkewe. Je, hakimu angeweza kumhurumia Esau asilipe adhabu hiyo na wakati huo huo atende haki? Jibu ni ndiyo. Tuone jinsi hakimu alivyoweza kumhurumia Esau na kuhakikisha adhabu yake ilipwe. Kwanza, Hakimu alijua hawezi kumwacha Esau aende zake bila adhabu yake kulipwa. Kwa sababu ya huruma yake, hakimu alikubali kumlipia adhabu yake. Alitoa pesa kwenye mfuko wake na akampa Esau ili Esau alipe deni la adhabu yake. Kwa njia hii, wizi wa Esau uliadhibiwa na Esau alihurumiwa. Esau aliondoka akiwa na shukrani na furaha sana kwa sababu alikubali kuupokea msaada wa hakimu huyu.

Je, hakimu angekubali Esau asilipe adhabu yake, angekuwa ametenda haki? Hapana, kwa sababu uovu wa Esau usingeadhibiwa. Je, hakimu alipoilipia adhabu ya wizi ya Esau, alitenda haki? Ndiyo, kwa sababu uovu wa Esau uliadhibiwa. Kupitia upendo, neema, na huruma ya hakimu, adhabu ya Esau ililipwa bila Esau binafsi kuadhibiwa.

Katika mfano huu, adhabu ya Esau ililipwaje bila Esau kuadhibiwa? Adhabu ya Esau ililipwa wakati mwingine alikubali kubeba gharama ya Esau – yaani kwa namna nyingine hakimu aliadhibiwa badala ya Esau.

Kuna njia peke gani ambayo Mungu anaweza kutuhurumia tusiadhibiwe na wakati huo huo gharama ya adhabu yetu ilipwe? Kwa njia ya Mungu kumwadhibu mwingine badala yetu. Wakati Mungu anamwadhibu mwingine kwa ajili ya dhambi zetu, adhabu inalipwa, haki inatendeka, na sisi wenyewe hatuhitaji kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu.

Wokovu wa kibiblia ni jibu la Mungu kuadhibu dhambi zetu bila sisi wenyewe kuadhibiwa kwa kuwa anaadhibu mwingine badala yetu.

***Kwa nini tuna tumaini la kuokolewa?***

Ingawa sisi ni wenye dhambi wasio na tumaini la kujiokoa, bado tuna tumaini la kuokolewa kwa sababu Mungu ni mwema na ametengeneza njia ya kuadhibu dhambi zetu bila kutuadhibu sisi wenyewe kwa kuadhibu mwingine badala yetu. Hili ndilo tumaini pekee tulilo nalo.

# 6. Wokovu ni Nini?


Katika mwanzo wa kitabu hiki tulieleza wokovu ni kurejezwa au kupatanishwa katika uhusiano wetu na Mungu. Sasa tufafanue zaidi maana yetu tukiunganisha yale tuliyojifunza hadi sasa:

**Wokovu ni kazi ya Mungu kumwokoa mwenye dhambi kutoka katika utawala wa Shetani na adhabu ya dhambi na kutengeneza uhusiano na ushirikiano kati ya mwenye dhambi na Mungu na kumweka chini ya utawala wa Mungu.**

Copyright © 2017 GMI Publications

Kwa ufafanuzi zaidi wokovu ni kuokolewa kutoka hali moja hadi hali nyingine mpya tunayopewa na Mungu.

| **KUTOKA** | **HADI** |
|---|---|
| Mfu Kiroho | Hai Kiroho |
| Utawala wa Shetani | Utawala wa Mungu |
| Utumwa wa dhambi | Utumwa wa Mungu |
| Utumwa wa Utu wa Kale | Kutawala Utu wa Kale |
| Ghadhabu ya Mungu | Upendo wa Mungu |
| Hukumu ya Mungu | Kibali cha Mungu |
| Laana ya Mungu | Baraka ya Mungu |
| Hali ya Uchafu | Hali ya Usafi |
| Kutenganishwa na Kristo | Kuunganishwa na Kristo |
| Kutokuwa na Tumaini | Kuwa na Tumaini |
| Kuwa mwenye Hatia | Kuwa Mwenye Haki |
| Adui ya Mungu | Rafiki ya Mungu |




***Mchoro #8*** *– Mtu wa kushoto bado hajaokolewa. Bado yuko chini ya utawala wa Shetani na dhambi. Mtu wa kulia ameokolewa na yuko katika uhusiano mzuri na Mungu.*

**Tunaona katika mchoro #8 kwamba:**

- Wokovu siyo kujitahidi kumpendeza Mungu
- Wokovu siyo kuokoa mtu kutoka utawala wa Shetani na dhambi tu ili ajitawale
- Wokovu siyo kukoa mtu asiadhibiwe tu

Yaani, wokovu ni kutoka katika hali fulani ili tupewe hali nyingine mpya. Jambo muhimu katika hali mpya ile ni uhusiano wetu na Mungu. Uhusiano wa kuwa chini yake na uhusiano wa kushirikiana naye katika upendo, imani, na ibada. Katika sehemu ya pili ya kitabu hiki tunaangalia zaidi maana ya kuwa katika uhusiano na Mungu.

# 7. Msingi wa Wokovu ni Nini?

***Msingi wa wokovu ni neema***

*Waefeso 2:8 – "Kwa maana mmeokolewa kwa neema,..."*

Tangu mwanzo hadi leo msingi wa wokovu ni neema ya Mungu. Kila aliyeokolewa tangu Adamu hadi leo ameokolewa kwa sababu ya neema ya Mungu. Bila neema ya Mungu hakuna anayeweza kuokolewa. Kwa nini? Kumbuka tulisema maana ya neema ni wema kwa wale wasiostahili kutendewa wema bali wanastahili kuadhibiwa. Kwa sababu sisi ni wenye dhambi, sisi sote tunastahili hukumu ya

Copyright © 2017 GMI Publications

milele. Bila neema ya Mungu kila mtu angepata yale anayostahili mbele ya Mungu. Anastahili nini? Hukumu ya adhabu ya milele.

Ingawa Biblia inafundisha kwamba msingi wa wokovu ni neema ya Mungu, watu wengi wanajaribu kujipatanisha na Mungu kulingana na mawazo yao. Wanataka kufanya jambo fulani ili wastahili kuokolewa. Wengine wanajaribu matendo mema, wengine wanajaribu kuachana na dhambi, baadhi wanajiunga na makanisa, na wengine wanatafuta nafasi za uongozi katika makanisa. Njia hizi zote hazifai kwa sababu bado dhambi zao zinawafanya kustahili adhabu ya milele. Ni kupitia neema ya Mungu tu, mtu anaweza kuokolewa.

Yule anayedhani msingi wa wokovu ni matendo mema, kutii sheria, kuacha dhambi, au kutubu, amekosa kufahamu namna Mungu anavyowaokoa watu, na bado yuko chini ya hukumu ya Mungu.

***Neema inapatikana kwa njia ya imani***

*Waefeso 2:8 –"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani;,..."*

Tangu mwanzo wa dunia, wokovu umekuwa kwa neema kupitia imani. Kwa mfano, Abeli alionesha imani yake alipotoa sadaka yake kwa Mungu kufuatana na mapenzi ya Mungu (Heb 11:4). Mungu alimkubali Abeli kwa sababu ya neema ya Mungu na imani ya Abeli. Kabla Yesu hajafa msalabani, Mungu alikuwa ameamuru watu wake kutoa sadaka za kuteketezwa (dhabihu) ili wapewe msamaha wa dhambi zao. Wale waliotoa sadaka hizo *kwa njia ya imani* walionesha jinsi walivyoamini Mungu alikuwa anasamehe dhambi zao kupitia kifo cha mnyama aliyeuawa badala yao wenyewe kuadhibiwa. Sadaka hizo za kuchinja wanyama zilikuwa mifano ya jinsi Yesu atakavyokuja kuadhibiwa na kufa badala ya wanadamu wote. Lakini kwa kipindi kile hawakujua kwa uwazi kuhusu kuja kwa Yesu bali walijua tu kwamba Mungu ameagiza sadaka hizo na hivyo katika imani wakazitoa.

Siku hizi tunaagizwa na Mungu kuiweka imani yetu katika nini? Siku hizi tunaagizwa kuiweka imani yetu katika Bwana Yesu Kristo. Tunatakiwa kuamini nini kuhusu Bwana Yesu? Siyo tu kuamini kwamba alikuwa nabii wa Mungu, kwamba alikuwa mtu mwema, wala ukweli wa yeye kuwa Mwana wa Mungu. Mambo hayo yote ni kweli, lakini imani katika mambo hayo haiokoi. Imani katika Bwana Yesu inayookoa ni kuamini kwamba aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu ili atupatanishe na Mungu kupitia kifo na ufufuo wake. Tutachunguza maana ya imani katika Bwana Yesu kwa makini baadaye.

***Njia yo yote iliyo tofauti na imani haifai katika kuokoa***

Kumwamini Kristo na kazi yake msalabani ni njia pekee ya kuipokea neema ya Mungu. Mtu hataipokea neema ya Mungu kwa njia ya toba, kwa njia ya matendo mema, kwa njia ya kujitahidi kuifuata sheria, kwa njia ya kubatizwa, wala kwa njia ya kuwa mshirika wa kanisa fulani. Njia pekee ya kuipokea neema ya Mungu inayoleta wokovu ni kwa njia ya imani katika Bwana Yesu.

# 8. Kwa Nini Kifo cha Yesu ni Muhimu?

Kwa sababu mwanadamu hawezi kujiokoa mwenyewe, ni Mungu tu anayeweza kuutengeneza wokovu kwa ajili ya mwanadamu. Tumeona kwamba tunaokolewa kwa sababu ya neema ya Mungu, kwa njia ya imani katika kifo na ufufuo wa Bwana Yesu kama malipo ya dhambi zetu zote. Bwana Yesu alifanya kazi kubwa kwa ajili yetu alipokufa msalabani. Tutaona hapo chini jinsi kifo chake kilivyoutengeneza wokovu wetu. Ni kwa sababu hiyo kifo cha Yesu ni muhimu.

## A. Kifo Cha Yesu ni Muhimu kwa Sababu Yesu Asiye na Dhambi Aliweza Kufa Badala ya Wanadamu Akiadhibiwa kwa Ajili ya Dhambi Zao Zote.

***Ni lazima mwanadamu asiye na dhambi afe kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi.***

Tulishaona kwamba Mungu aliye mwenye haki analazimika kuadhibu dhambi zote. Ili tuweze kuokolewa tunahitaji kukwepa adhabu ya dhambi zetu. Tuliona hali hii inawezekana tu ikiwa mwingine ataadhibiwa badala yetu. Kama mwingine anaweza kulipa deni letu Mungu ataacha hasira yake na tutakuwa tumepatanishwa na kurejezwa katika ushirika wetu naye. Yaani, tutakuwa tumeokolewa.

Nani anaweza kuadhibiwa badala yetu? Biblia inasema ni lazima mwanadamu aadhibiwe kwa ajili ya dhambi za wanadamu (Ebr 2:14-17). Mungu hatapokea kifo cha mnyama kama malipo ya dhambi za wanadamu (Ebr 10:4) na hata malaika hawawezi kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi za wanadamu.

Pili, yule atakayeadhibiwa badala ya wanadamu wenyewe, lazima asiwe na dhambi. Mwanadamu mwenye dhambi hawezi kuadhibiwa kwa ajili ya mwingine. Mwenye dhambi ni lazima aadhibiwe kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe. Tumeshaona adhabu ya dhambi, hata moja, ni adhabu ya milele. Kutokana na hali hii, mwenye dhambi hawezi kumaliza adhabu yake ili aadhibiwe kwa ajili ya mtu mwingine mwenye dhambi. Hivyo, ili mtu mwingine aadhibiwe kwa ajili ya dhambi zetu, inabidi yule mwingine awe mwanadamu asiye na dhambi; yaani mtu ambaye amemtii Mungu asilimia mia bila kuvunja hata amri au agizo moja.

***Yesu aliweza kufa kwa ajili yetu kwa sababu alikuwa mwanadamu 100% asiye na dhambi***

Ni mtu gani anayeweza kufanya hivyo? Mwenye sifa hiyo? Hakuna! Biblia inasema *"wote wametenda dhambi"* (Rum 3:23).

Hapo tunaona ukuu wa neema ya Mungu na sababu tunaweza kuokolewa kwa neema yake tu. Kwa kuwa hakuna mtu anayeweza kuadhibiwa kwa ajili ya mwandamu mwenzake kutokana na hali ya wote kuwa wenye dhambi wanaostahili hukumu, Mungu alimtuma Mwana wake azaliwe hapa duniani. Mwana wa Mungu alizaliwa kama mwanadamu (Gal 4:4) na aliitwa Yesu. Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu pia, aliweza kuishi bila kutenda dhambi hata moja (2 Kor 5:21). Pia kwa sababu Yesu hakuwa na dhambi yo yote (Ebr 4:15), yeye pekee aliweza kuzichukua dhambi za ulimwengu na kuadhibiwa badala yetu. Kristo alipokufa, alizichukua dhambi zetu zote. Aliadhibiwa badala yetu sisi ili tusiadhibiwe kamwe (Isa 53:5,6; 2 Kor 5:21; 1 Pet 2:24).

***Kwa kuwa Yesu ni 100% Mungu aliweza kufa kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote.***

Lakini tukumbuke kwamba wakati Yesu alipokufa alikuwa asilimia mia moja mwanadamu na asilimia mia moja Mungu wakati mmoja. Kwa kuwa alikuwa mwanadamu aliweza kufa kwa ajili ya wanadamu wenzake. Lakini ni muhimu pia kwamba Yesu alikuwa Mungu wakati alipofia dhambi za wanadamu wote. Kifo cha mwanadamu mmoja wa kawaida kisingeweza kubeba dhambi za wanadamu wote. Mwanadamu wa kawaida asiye na dhambi angeweza kuadhibiwa kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi mmoja tu. Tukumbuke mshahara au adhabu ya dhambi ni mauti ya milele. Hivyo mtu mmoja huyu wa kawaida angehitaji kuadhibiwa milele kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja, ili mwenye dhambi asiadhibiwe. Na kwa njia hii huyu asiye na dhambi asingeweza kumaliza adhabu hiyo ili aadhibiwe kwa ajili ya wengine pia.

Lakini, kwa sababu Yesu alikuwa asilimia mia Mungu, umungu wake ulimwezesha kufia dhambi za watu wote. Uwezo huo unatokana na thamani ya kifo chake; yaani kifo cha Mungu.

Tena umungu wa Yesu ulimwezesha Yesu kuadhibiwa kwa muda mfupi badala ya hitaji la kuadhibiwa milele.

## B. Kifo cha Yesu ni Muhimu kwa Sababu Ghadhabu ya Mungu Juu ya Wenye Dhambi Ilitulizwa Wakati Yesu Aliadhibiwa Badala ya Wenye Dhambi Wenyewe

***Mungu aliitoa ghadhabu yake juu ya Yesu***

Sisi wenye dhambi tulikuwa chini ya ghadhabu ya Mungu. Kristo alipoipokea adhabu ambayo sisi tulistahili kuipokea, ghadhabu ya Mungu ilimwagika juu ya Yesu. Ndiyo sababu wale wanaomwamini Kristo hawatapokea ghadhabu ya Mungu tena. Kwa sababu ghadhabu ya Mungu imetulizwa msalabani, njia ya sisi kupatanishwa na Mungu ilifunguliwa.

## C. Kifo Cha Yesu ni Muhimu kwa Sababu Kupitia Kifo Hicho Kristo Alimshinda Shetani Ili Aweze Kutukomboa Tusiwe Chini ya Mamlaka ya Shetani Tena.

Copyright © 2017 GMI Publications

Sisi wenye dhambi tulikuwa chini ya mamlaka ya Shetani. Yesu alimshinda Shetani ili tuwe huru kutoka chini ya mamlaka ya Shetani (Ebr 2:14-15). Sasa, tuko chini ya utawala wa Mungu; Muumba wetu anayetupenda (Kol 1:13).

**D. Kifo cha Yesu ni Muhimu kwa Kuwa Katika Kifo Chake Utu Wetu wa Kale Ulikufa Ili Tukombolewe na Utumwa wa Dhambi.**

Sisi wenye dhambi tulikuwa tunatawaliwa na utu wa kale na tulikuwa watumwa wa dhambi. Ndiyo kusema kielelezo cha maisha yetu kilikuwa kutenda dhambi kwa kuwa kama mtumwa wa dhambi hatukuweza kutotenda dhambi. Yesu aliposulubishwa, utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye. Maana ya kufa kwa utu wa kale ni kusema tuliondolewa kutoka kuwa chini ya utawala wa utu wa kale au dhambi katika maisha yetu (Rum 6:6-7). Mabadiliko hayo yana maana aliyemwamini Yesu siyo mtumwa wa dhambi tena na nguvu za Shetani zimevunjwa. Kama wakristo, bado tuna uwezo wa kutenda dhambi, lakini kuna uchaguzi sasa. Tunaweza kuchagua kutenda dhambi au kutotenda kwa kuwa sisi hatujawa watumwa tena wa dhambi.

Tumeona ni kweli Yesu aliifanya kazi kubwa kwa ajili yetu alipokufa msalabani. Aliipokea adhabu ya dhambi zetu ili atupatanishe na Mungu na kutukomboa kutoka kwa Shetani, na dhambi. Kifo chake kilitosha kutuokoa. Tusichoke kumshukuru Mungu kwa kazi yake kuu!

# 9. Kwa Nini Kufufuka kwa Kristo ni Muhimu?

***Yesu asingefufuka Wakristo wasingepata wokovu***

Bwana Yesu alijidai kuwa Mungu (Mk 14:61-64), alidai kwamba atakufa kwa ajili ya dhambi za walimwengu (Mk 10:45), na alidai atafufuka (Mk 9:31). Kama Yesu angekufa na kubaki kaburini ingekuwa na maana ya kwamba hajashinda mauti na sisi tusingekuwa na uwezo wa kuzaliwa upya katika maisha yetu ya kiroho wala kufufuka kwenda mbinguni pamoja na Yesu.

***Kufufuka kwa Yesu kunathibitisha yeye ni Mungu***

Lakini, kufufuka kwake kunathibitisha ukweli wa madai yake. Kufufuka kwake kunathibitisha kwamba Yesu ni Mungu (Rum 1:4) na kwamba aliweza, kama Mungu, kufia dhambi za walimwengu wote.

***Kufufuka kwa Yesu kunathibitisha Mungu ameikubali sadaka yake***

Pia, kufufuka kwake kunathibitisha kwamba Mungu alikubali kifo chake kama malipo kamili kwa ajili ya dhambi zote (Rum 4:25). Kufufuka kwake ni tangazo la Mungu kwa watu wote kwamba Mungu amekikubali kifo cha Yesu badala ya kifo cha mwenye dhambi kwa ajili ya dhambi zake. Yesu ameimaliza kazi hiyo na Mungu amependezwa naye. Hakuna sababu kwa Yesu kubaki mautini kwa sababu kazi yake ilikamilika na Mungu hakuwa na sababu ya kuendelea kumhukumu mautini.

***Kufufuka kwetu ni hakika kwa kuwa yeye alifufuka kwanza***

Kufufuka kwa Yesu baada ya kufa kwa ajili ya dhambi zetu ndiyo sababu sisi tunapata kufufuka kwa njia mbili. Kwanza tukiweka imani yetu katika kifo cha Yesu, Biblia inasema tunazaliwa upya ambayo ni kufufuka katika maisha yetu ya kiroho (1 Pet 1:3). Pili tukizaliwa upya katika maisha yetu ya kiroho tuna ahadi ya Mungu ya kwamba atatufufua kimwili siku ya mwisho akiitumia nguvu ile ile aliyoitumia kumfufua Yesu (2 Kor 4:14, 1 Kor 15:20). Kama Mungu aliweza kumfufua Yesu, tuna tumaini kwamba ataweza kutufufua na sisi pia.

***Kufufuka kwa Yesu ni msingi wa Ukristo***

Kwa sababu zilizotajwa hapo juu, tunaweza kusema kufufuka kwa Yesu ni msingi mkuu wa ukristo wetu. Bila msingi huo, hakuna wokovu. Ndiyo sababu mtume Paulo anasema kwamba, ikiwa Kristo hakufufuka, imani yetu ni bure (1 Kor 15:17) na wanaohubiri ufufuo wake ni mashahidi wa uongo juu ya Mungu (1 Kor 15:15).

Copyright © 2017 GMI Publications

# 10. Je, Yesu Alizifia Dhambi Zote?

Kabla hatujaendelea, tuhakikishe tunaelewa faida ya kifo cha Yesu kwa wote waliookolewa. Tuangalie tukio moja katika maisha ya mtu *aliyeokolewa.*

***Mfano wa Benyamini aliyekufa kabla hajaungama***

Benyamini alikuwa Mkristo aliyeokoka kweli lakini aliiba kalamu ya mtu. Kwa bahati mbaya alikufa mara moja baada ya tendo hilo na hakuweza kuungama dhambi hiyo kwa Mungu. Je, jambo gani litatokea atakaposimama mbele ya Mungu? Atahukumiwa na kutupwa katika ziwa la moto, au atapokelewa mbinguni?

Andika jibu lako:________________________________________

Jibu lako litaonesha kama umeelewa vizuri kazi ambayo Yesu alimaliza msalabani kwa ajili ya wote waliookolewa naye. Ikiwa jibu lako ni kwamba atapokelewa mbinguni, ina maana umeelewa kazi ya Yesu msalabani. Lakini, kama umejibu kwamba atahukumiwa na kutupwa jehanamu, ina maana hujaelewa maana ya kifo cha Yesu.

***Tunapookoka Yesu anachukua dhambi zote na kuzisafisha***

Kumbuka Biblia inafundisha wakati Yesu alipokufa msalabani, Bwana Yesu alichukua au kusafisha dhambi *zote* na Mungu alimwadhibu Yesu kwa ajili ya dhambi zetu *zote.*

*1 Yohana 1:7 – "Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote."*

*1 Petro 2:24 – "Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa."*

*Isaya 53:5-6 – "Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe; na BWANA ameweka juu yake maovu yetu sisi sote."*

***Tunapookoka Mungu anasamehe dhambi zetu zote***

Matokeo ya Bwana Yesu kuchukua juu yake mwenyewe makosa yetu *yote* na kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi hizo zote ni kwamba Mungu amesamehe makosa yetu *yote*.

*Wakolosai 2:13 – "Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akiisha kutusamehe makosa yote"*

***Tunapookoka Mungu anatangaza kuwa hatuwezi kuhukumiwa tena***

Matokeo ya Mungu kusamehe dhambi zetu zote ni kwamba ye yote anayesamehewa dhambi zake zote hawezi kuadhibiwa tena kwa ajili ya dhambi zake. Kutokana na kazi ya Yesu msalabani, na imani ya mtu katika Yesu, Mungu anasamehe dhambi za mtu huyu na kutanganza hataadhibiwa tena. Tangazo hilo linatangazwa mara anapookoka. Mungu hasubiri mtu amalize maisha yake ili aweze kuona kama baadaye atafanya dhambi ambayo haitasamehewa. Mungu anatangaza mara moja akijua adhabu ya Yesu imelipia dhambi zote.

*Warumi 8:1 – "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu."*

***Mawazo ya uongo kuhusu kiasi cha dhambi Yesu alicholipia***

Sasa tuangalie mawazo mengine yanayotaka kukanusha au kubishia mafundisho haya. Pia tuangalie mifano ambayo itatusaidia kuelewa kwamba Biblia inafundisha kwa uwazi kwamba wote waliookolewa hawataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao kwa kuwa Yesu alishasamehe dhambi zao zote hata kabla hawajazitenda zingine.

***Wazo la uongo #1 – Yesu anasamehe tu dhambi zile zilizotendeka kabla mtu hajaokoka***

Watu wengine wanasema wakati mtu anapookolewa, dhambi zile alizozitenda tayari zinasamehewa, lakini dhambi ambazo hajatenda bado haziwezi kusamehewa kwa kuwa bado hajazitenda.

Mfano unaofuata unaonesha kwamba inawezekana kwa dhambi kulipiwa na kusamehewa hata kabla dhambi hiyo yenyewe haijatendeka. Matokeo yake ni kwamba dhambi hiyo itakapokuja kutendeka, hakuna adhabu itakayotolewa.

Mfano: Uongozi wa kijiji ulitangaza kwamba kila mwanakijiji lazima awe na choo cha kuchimba kabla mwisho wa mwezi haujaisha. Tena walisema mwanzo wa mwezi unaofuata, viongozi watapitia kila nyumba na kukagua. Ye yote ambaye hana choo atawekwa ndani mpaka faini ya 10,000 tsh imelipwa. Mwisho wa mwezi ulipokaribia Petro alijikuta bado hajaanza kuchimba choo chake na ikaonekana atafeli kumaliza. Rafiki wa Petro, Mathayo, akaamua kwenda kwa uongozi wa kijiji na kuwataarifu kwamba Petro atashindwa kumaliza. Kwa sababu Mathayo hakutaka Petro kufungwa akaamua kumlipia faini yake hata kabla mwezi haujaisha; yaani kabla Petro hajakosea amri ya kijiji. Wakati uongozi wa kijiji ulipitia nyumba ya Petro mwishoni mwa mwezi wakakuta hajamaliza choo chake. Je, waliweza kumfunga Petro ndani? Hapana. Kwa nini? Kwa sababu Mathayo alikuwa ameshamlipia Petro faini yake hata kabla hajaingia kwenye kosa.

Vivyo hivyo Bwana wetu Yesu Kristo aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu msalabani hata kabla hatujazaliwa na kutenda hata dhambi moja. Dhambi zetu zote bado zilikuwa katika siku zijazo wakati Yesu alisulubishwa, yaani dhambi zetu ambazo tulitenda kabla hatujaokolewa na dhambi zetu tulizotenda baada ya kuokolewa. Dhambi zote hizo zilisamehewa zaidi ya miaka 2000 iliyopita wakati Yesu aliadhibiwa msalabani.

Kwa sababu dhambi zote ziliadhibiwa msalabani, Mungu hataadhibu ye yote anayemwamini Yesu na kuokolewa. Hataadhibu dhambi zilizotendeka kabla mtu hajaokoka na hataadhibu dhambi za mtu zilizotendeka baada ya kuokoka kwa kuwa alishaziadhibu zote katika Yesu.

***Wazo la uongo #2 – Lazima mtu aungame dhambi zake baada ya kuokoka au hatasamehewa na atalazimika kuadhibiwa baada ya kufa kwake.***

Watu wengine wanasema, ingawa Yesu alifia dhambi zote, hatasamehe dhambi ambazo mtu aliyeokolewa hajaziungama. Na mtu akikosa kuungama dhambi fulani atahukumiwa milele kwa ajili ya dhambi hizo.

Mfano unaofuata unaonesha wakati dhambi au kosa limeshaadhibiwa, isingekuwa haki mtu huyu aadhibiwe tena kwa kosa lile lile.

Patriki aliiba kuku wa jirani yake. Tendo hilo lilikuwa kinyume na sheria na alilazimika kuadhibiwa alipokamatwa. Uongozi wa kijiji chake uliamua Patriki alipe faini ya 10,000 tsh kwa ajili ya kosa la kuiba kuku huyo. Lakini Petro hakuwa na 10,000 tsh kwa ajili ya kulipa. Hivyo kesho yake Samweli, rafiki wa Petro, aliamua kwenda kumlipia Petro deni lake lote. Lakini siku iliyofuata viongozi wa kijiji walirudi kwa Petro na kumdai 10,000 tsh kwa ajili ya kuiba kuku yule. Je, viongozi wana haki kumdai Petro kwa mara ya pili wakati deni lake lilishalipiwa kwa kosa hilo hilo? Hapana. Baada ya faini ya Petro kulipiwa mara ya kwanza, Petro alikuwa hana hatia tena. Kumlazimisha kulipa kwa mara ya pili kungekuwa kutomtendea haki.

Bwana Yesu Kristo alilipia deni la dhambi zote la watu wote waliomwamini na kuokolewa. Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zote na Mungu aliridhika na malipo yake. Je, Mungu mwenye haki anaweza kumwadhibu mtu kwa ajili ya dhambi ambazo zimeshaadhibiwa kupitia Yesu Kristo? Hapana. Kumwadhibu mtu kwa dhambi ambazo Yesu alishaadhibiwa kungekuwa kuadhibu dhambi zile zile mara mbili. Kufanya hivyo kusingekuwa sahihi na Mungu mwenye haki hawezi kufanya hivyo. Kwa kuwa dhambi inaweza kulipiwa mara moja tu, na kwa kuwa Biblia inafundisha dhambi zetu zililipiwa na Yesu msalabani, mtu aliyeokoka hawezi kuadhibiwa tena kwa kuwa dhambi zake zilishalipiwa. Ndiyo maana tunasoma katika Warumi 8:1, "*Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu.*"

Isitoshe, haiwezekani mtu kukumbuka na kuungama dhambi zake zote kwa maana ya kutaja kila dhambi. Watu wengine wanaokoka katika uzee wao. Je, kweli wanaweza kukumbuka kila dhambi waliyoitenda ndani ya maisha yao yote ili waziungame? Haiwezekani. Dhambi zetu ni nyingi mno na Mungu hategemei tuweze kukumbuka kila moja. Hata hivyo ni kawaida ya wanadamu kutotambua kila dhambi wanayotenda. Mtu atawezaje kukumbuka dhambi ambayo hajui aliitenda? Hawezi. Ni kweli Mungu anataka tuungame kila dhambi tunayotambua na kukumbuka lakini kutoadhibiwa kwetu hakutegemei uwezo wetu wa kukumbuka kila dhambi na kuiungama. Mtu anapookoka anakiri dhambi zake kwa ujumla na Mungu anazisamehe kwa ujumla. Tena anamsamehe hata dhambi ambazo hajazitenda bado, yaani dhambi ambazo atazitenda baadaye katika maisha yake ya kikristo. Ingekuwa ni kweli tunapaswa kuungama kila dhambi kwa kuitaja, wote tungeadhibiwa na kuhukumiwa kwa sababu wote tungesahau angalau dhambi moja na hukumu ya dhambi moja tu ni mauti ya milele.

***Kutafakari zaidi kuhusu mawazo haya ya uongo***

Copyright © 2017 GMI Publications

Mchoro unaofuata unaonesha mifano mbalimbali ya jinsi Mungu anavyoweza kufikiria msamaha wa dhambi. Mifano mingine ni sahihi kulingana na mafundisho ya Neno la Mungu na mifano mingine ni ya uongo. Katika michoro hii mstari wa chini ni mfano wa maisha ya mtu, “x” ni mfano wa dhambi zake ambazo hazijasamehewa, na mchoro wa msalaba unaonesha wakati ambao mtu huyu aliokolewa katika maisha yake.




*Mchoro #9 – Huu ni mfano wa jinsi ambavyo maisha ya mtu yangeonekana machoni pa Mungu kama Mungu hajasamehe dhambi zake hata moja.*




*Mchoro #10 – Huu ni mfano wa mtu ambaye Mungu alisamehe dhambi zake zilizotendeka kabla hajaokoka (wazo la uongo).*




*Mchoro #11 – Huu ni mfano wa mtu aliyeokoka na Mungu alisamehe dhambi zake zote kasoro moja mwishoni mwa maisha yake ambayo hakupata nafasi ya kuungama (wazo la uongo).*



*Mchoro #12 – Huu ni mfano wa mtu aliyeokoka na Mungu alisamehe dhambi zake zote.*

Mchoro #10 hapo juu unaonesha maisha ya mtu ambaye Yesu aliadhibiwa kwa ajili yake na Yesu aliondoa dhambi zote zilizotendeka na mtu huyu kabla hajaokoka. Tumaini la mtu huyu ni kwamba dhambi anazozitenda baada ya kuokoka zitasamehewa wakati anapoungama dhambi zake kwa Mungu njiani. Lakini tunahitaji kuuliza swali moja: Kama Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zilizotendwa na mtu huyu kabla hajaokoka, je, nani ataadhibiwa kwa ajili ya dhambi alizotenda baada ya kuokoka?

Watu wengine wanasema mtu akiungama dhambi zake kwa Mungu, Mungu atafuta dhambi zake na kumsamehe. Je, kuungama kunaweza kuondoa dhambi za mtu? Biblia inasema nini? Katika Waebrenia 9:22 tunasoma *pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi.* Maana yake nini “kumwaga damu”? Yesu angekata mguu au mkono wake na kumwaga damu, je, damu ile ingeweza kuleta msamaha wa dhambi? Hapana. Maana ya kumwaga damu ni mauti. Mauti ndiyo malipo ya dhambi (Rum 6:23). Wakati mtu anaungama dhambi zake, nani anakufa? Hakuna mtu. Yesu asingeondoa dhambi zote wakati alipokufa msalabani, kitu gani kingine kingeweza kuondoa dhambi? Hakuna.

Kama Yesu hakuondoa dhambi zote msalabani, basi Yesu hakumaliza malipo ya dhambi zote. Atakuwa amelipa sehemu ya malipo tu. Na kama hali hii ni kweli nani atamaliza malipo yale ya dhambi ambayo Yesu hakumaliza? Jibu ni yule aliyezitenda. Atahitaji kuadhibiwa milele katika ziwa la moto ingawa katika wazo hilo la uongo Yesu aliadhibiwa kwa baadhi ya dhambi zake.

Tunajua kwa hakika kwamba Mungu ataadhibu dhambi zote. Kama Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi za watu zilizotendeka kabla hawajaokoka, nani ataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao zilizotendeka baada ya kuokoka? Jibu tena ni yule aliyezitenda, tena atahitaji kuadhibiwa milele kwa kuwa ndiyo malipo ya dhambi hata moja.

Kama Yesu hakuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zote na kama hakuondoa dhambi zote msalabani, watu wote wataadhibiwa kwa dhambi zao ambazo Yesu aliziachilia. Na kama hali hii ni kweli, kumbe hatuna tumaini la kuokolewa.

Mchoro #11 hapo juu unaonesha maisha ya mtu ambaye Yesu aliadhibiwa kwa ajili yake na Yesu aliondoa dhambi zake zote kasoro moja aliyotenda katika dakika zake za mwisho duniani. Kwa sababu alikufa ghafula, hakupata nafasi ya kuungama dhambi hiyo ya mwisho. Tuulize swali letu tena: Ikiwa Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake zote kasoro moja, nani ataadhibiwa kwa ajili ya dhambi hiyo moja iliyobaki? Jibu tena ni yule aliyeitenda. Lakini mfano huu ni wa uongo kwa sababu ukweli ni kwamba Yesu aliadhibiwa tayari kwa ajili ya dhambi zote za kila mtu anayemwamini Yesu.

*Copyright © 2017 GMI Publications*

Mchoro #12 hapo juu unaonesha maisha ya mtu ambaye Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake zote. Mtu huyu amesamehewa dhambi zake zote. Kwa sababu dhambi zake zote zimesamehewa, mtu huyu hawezi kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zake. Mtu huyu kweli ameokolewa.

Kama huamini kwamba Yesu alikufa na kuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zako zote wakati ukweli ni kwamba ameondoa na kusamehe dhambi zako zote, inakubidi kuchimba zaidi katika kitabu hiki na Neno la Mungu mpaka wakati utakapoelewa na kuamni ukweli huo unaofundishwa na Biblia. Kama Yesu hakuadhibiwa kwa ajili ya dhambi zako zote wakati alipokufa msalabani, Mungu atalazimika kukuhukumu na kukuadhibu kwa dhambi zile ambazo Yesu hajakulipia (Kumbuka Mungu ni mwenye haki na ni lazima aadhibu dhambi zote). Hivyo kama Yesu alipokea adhabu yako ya dhambi zote kasoro moja, basi wewe utaadhibiwa milele kwa dhambi ile moja iliyobaki. Je, adhabu ya hata dhambi moja ni nini? Ni mauti ya milele; ni hali ya kutenganishwa na Mungu milele na milele katika ziwa la moto. Kwa hiyo, kama Yesu hajakulipia dhambi zako zote na kuziondoa, basi hakuna wokovu na utaangamizwa kwa ajili ya dhambi zako.

Lakini usihangaike! Biblia inafundisha kweli kwamba Yesu alikuja duniani ili aokoe wenye dhambi wasiadhibiwe kwa ajili ya dhambi zao. Mtu akisema Yesu alisamehe baadhi ya dhambi tu, mtu huyu ni mwongo na haelewi mafundisho ya Neno la Mungu. Ingemaanisha kwamba Yesu hakutimiza kusudi lake la kuja duniani. Zaidi mtu akisema hivyo ina maana kifo cha Yesu hakina kazi kwa sababu watu wote bado wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao ambazo hazikulipiwa. Mawazo kama hayo hupuuza kazi kubwa ambayo Yesu alifanya msalabani. Mawazo kama hayo siyo sahihi, tena ni ya uongo.

### *Hoja ya uongo kwamba mafundisho haya yataruhusu Wakristo kutenda dhambi*

Lakini wengine wanaogopa kufundisha mawazo ya kibiblia kwamba mtu aliyeokoka amesamehewa dhambi zake zote, ikiwa ni pamoja na zile alizotenda tayari na hata zile ambazo atatenda baadaye. Wanaogopa Mkristo huyu atazidi kutenda dhambi bila kujali akifundishwa hivyo. Mtume Paulo anasema, *"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?"* (Rum 6:12). Yaani, Mkristo wa kweli hawezi kuwa na tabia ya namna hiyo. Kumbuka mwanzoni mwa kitabu hicho tulisema kwamba kila mtu lazima achague yule atakayemtumikia. Mkristo ni mtu aliyeamua kumtumikia Mungu na kuachana na dhambi. Kuendelea katika dhambi bila kujali kusingeonesha shukrani yo yote kwa ajili ya wokovu huu wa ajabu unaopatikana katika Yesu. Tubaki katika mafundisho ya kweli ya Neno la Mungu na tubaki katika hali ya kumwabudu, kumtumikia, na kumshukuru Mungu tukiachana na dhambi.

### *Kwa nini wengine wataadhibiwa ikiwa Yesu alifia dhambi zote?*

Pengine mafundisho haya yatakuwa yamezalisha swali kwako. Labda utauliza, "Je, kama Yesu aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi za walimwengu wote, kwa nini wengine wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, hasa kama siyo haki kuadhibu dhambi zile mara mbili?" Hilo ni swali zuri linaloonesha unafuata kwa ukaribu somo letu.

Jibu letu la kwanza ni kusema tunaamini hivyo kwa sababu Biblia inafundisha hivyo. Lazima tubaki katika mafundisho ya Biblia. Biblia inafundisha kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya kila mwanadamu na zaidi alikufa kwa ajili ya dhambi zote za kila mwanadamu. Mistari ya Biblia ni mingi sana inayofundisha mafundisho hayo (kwa mfano: Yn 3:16, Ebr 2:9, 1 Tim 2:4-6, 4:10, 1 Yoh 2:2 n.k.). Vilevile Biblia inafundisha wengine watahukumiwa kwenye ziwa la moto. Hivyo tunaamini hali zote mbili ni kweli.

Inawezekanaje? Jibu ni kwamba wengine wanakataa malipo ya Yesu na wanataka walipe wenyewe. Unaweza kumlipia mtu deni lake, lakini akikataa na kutaka kulipa mara ya pili mwenyewe huwezi kumzuia. Maana yake ni kwamba Mungu aliandaa njia kwa ajili ya watu kuondolewa dhambi zao na kusamehewa. Njia ile ni kumwamini Yesu Kristo na kazi yake msalabani. Mungu alimwadhibu Yesu kwa ajili ya wote. Lakini ni lazima kila mtu apokee neema hiyo kutoka kwa Mungu kwa njia ya kumwamini Yesu. Kila asiyeamini anatangaza hataki Yesu kubeba dhambi zake na pia anatangaza anataka abebe mwenyewe. Kwa mfano baba wa nyumba anaweza kufanya kazi nyingi ili chakula kipatikane kwa familia yake. Kazi imetendeka na chakula kimepatikana. Lakini mwingine katika familia anaweza kukataa kula chakula kile. Hivyo, ingawa chakula kiliandaliwa, anayekataa chakula hicho atahitaji kutafuta chakula chake mwenyewe.

Vivyo hivyo Mungu aliandaa njia ya msamaha kwa kumwadhibu mwana wake Yesu Kristo. Lakini kuna sharti kwa kila mtu ili afaidike na msamaha ule; sharti lile ni imani katika Yesu.

Copyright © 2017 GMI Publications

# 11. Nifanye Nini Nipate Kuokoka?

Mtu akitaka kuokolewa, afanye nini? Watu wengine wanasema lazima mtu huyu aache kutenda dhambi, wengine wanasema afanye matendo mema au atii mafundisho ya Yesu. Tumeshaona katika kitabu hiki kwamba hakuna atakayeokolewa kwa njia ya kuacha dhambi wala kwa kutenda matendo mema.

Biblia inatoa jibu moja tu kwa ajili ya swali hilo: Mwamini Bwana Yesu Kristo (Mdo 16:31; Yn 3:15, 16, 36; 5:24; 6:40, 47; 20:31; Mdo 10:43; Rum 1:10; 4:23-34; 10:9; 1 Tim 1:16; 1 Yn 5:1, 13).

*Matendo 16:31 - "Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako."*

*Yohana 3:16 "Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele."*

*1 Timotheo 1:16 - "Lakini kwa ajili hii nalipata rehema, ili katika mimi wa kwanza, Yesu Kristo audhihirishe uvumilivu wake wote; niwe kielelezo kwa wale watakaomwamini baadaye, wapate uzima wa milele."*

Kumwanini Yesu kuna maana gani? Ukimwambia mtu kumwamini Yesu, ni mambo gani ambayo unataka aamini? Andika jibu lako hapo chini (Lakini usitumie jibu la "kumpokea Yesu," "kumkubali Yesu," au maneno mengine yanayofanana na "kuamini").

Maana ya kumwamini Yesu ni:

________________________________________________________________________________

________________________________________________________________________________

Baadaye katika sura hii tutafafanua maana ya kumwamini Yesu lakini kwanza tuangalie mawazo mabaya au ya uongo.

Je, kila anayemwamini Yesu ataokolewa? Labda utashangaa jibu letu; jibu letu ni hapana. Biblia inafundisha kwamba watakuwepo watu wengi wanaosema wamemwamini Yesu lakini wengine kati ya hawa watakuwa hawajaokoka. Wenyewe ni Wakristo kwa jina tu, siyo Wakristo wa kweli. Siku ya mwisho, hawa watatambulishwa na wataadhibiwa (Mt 7:21-23).

Inawezekanaje mtu amwamini Yesu na asiokoke? Tuangalie njia tatu.

***Watu wanaweza kumwamini Yesu bila kuokolewa wakiamini bila kuelewa maana ya kweli ya kumwanini Yesu***

Watu wakiambiwa kumwamini Yesu bila kuelezwa ni mambo gani ambayo wanapaswa kuamini kuhusu Yesu, pengine wataamini mambo mengine yasiyoweza kuwaokoa. Labda yale watakayoamini yatakuwa habari iliyo kweli au ya uongo. Hata kama ni kweli, haitawasaidia kuokoka kama siyo habari husika. Kwa mfano, ikiwa mtu atafikiri maana ya kumwamini Yesu ni kutii mafundisho yake, je, imani hiyo itamwokoa? Hapana. Mwingine akifikiri maana ya kumwanini Yesu ni kuhudhuria kanisani, je, imani hiyo itamwokoa? Hapana. Ikiwa mtu atafikiri maana ya kumwamini Yesu ni kuacha kutenda dhambi, je, imani hiyo itamwokoa? Hapana. Ili mtu aokolewe, lazima aelewe maana halisi ya kumwanini Yesu inayookoa.

***Watu wanaweza kumwamini Yesu bila kuokolewa wakimwamini lakini pia wanategemea kitu kingine kuchangia wokovu wao pia***

Mtu akimwamini Yesu na wakati huo huo anaamini kitu kingine cha pili kama matendo mema, ubatizo, kutii amri kumi n.k. mtu huyu hajaokolewa. Vilevile kama mtu atamwamini Yesu ili apate msamaha kwa ajili ya dhambi alizozitenda kabla hajamwanini Yesu lakini anategemea kuungama njiani kwa ajili ya dhambi zote atakazozitenda baada ya kumwamini Yesu, huyu naye hajaokolewa. Kwa nini? Kwa sababu Biblia inafundisha imani inayookoa ni imani inayomlenga Yesu peke yake. Kwa maneno mengine, ni lazima mtu aweke imani yake yote katika Yesu ili asamehewe dhambi zake. Mtu anayemwanini Yesu lakini pia anaamini kitu kingine kiasi fulani, hajaweka imani yake yote katika Yesu. Akimwamini Yesu na pia sehemu fulani ubatizo, akimwamini Yesu na pia matendo mema, akimwamini Yesu na pia kutii amri za Mungu, ina maana hajamwanini Yesu asilimia yote peke yake.

Kwa mfano, Mtu akiomba kikombe cha maji kwako na unamletea kikombe cha chai ukisema, "haya ni maji yakichanganywa na majani ya chai kidogo." Je, mtu huyu atakubali ni maji? Hapana. Maji yaliyochanganywa na majani ya chai bado ni maji? Hapana, sasa yanaitwa chai.

*Copyright © 2017 GMI Publications*

Vivyo hivyo na imani. Tukichanganya imani katika Kristo pamoja na imani katika kitu kingine kama matendo mema au mahudhurio kanisani, imani hiyo siyo imani inayookoa tena kwa kuwa siyo imani katika Kristo tu. Maji halisi ni maji safi au maji tupu. Imani halisi inayookoa ni imani katika Kristo peke yake isiyochanganywa na cho chote kingine.

Yesu alipokuwa msalabani alisema, "Imekwisha!" (Yn 19:30). Alikuwa na maana gani alipotamka hivyo? Alikuwa na maana kwamba kifo chake msalabani kilitosha katika kulipia adhabu ya dhambi zote na hakuna kitu kingine kilichohitajika ili watu wapate kuokolewa. Malipo ya mshahara wa dhambi yaliisha. Watu wakisema ni lazima kumwamini Yesu pamoja na kitu kingine ili tuokolewe, ina maana kifo cha Yesu hakikutosha na hakikumaliza deni la dhambi. Kusema hivyo ni kupuuza kazi kubwa ambayo Yesu alifanya msalabani kwa kuwa kweli kweli kifo chake kilitosha na hakuna haja ya kuongeza cho chote kingine.

Mtu anaposema njia ya kuokolewa ni kumwamini Yesu na pia kuongeza kitu kingine, mtu huyu anabadilisha Injili ya Yesu. Katika Wagalatia, mtume Paulo aliwaonya wasibadilishe Injili ya Yesu.

*Wagalatia 1:6-9 – "Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe. Kama tulivyotangulia kusema, na sasa, nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe."*

Katika kanisa la Galatia wengine walianza kuhubiri kwamba Injili ya Yesu haitoshi. Walitaka kulazimisha Wakristo kuongeza utiifu wa sheria ya Musa pamoja na tendo la kutahiriwa. Lakini Paulo anahoji kuongeza cho chote kingine ni kufanya kifo cha Yesu kuwa bure, tena anasema ni ishara ya kukataa neema ya Mungu inayopatikana katika kumwamini Yesu.

*Wagalatia 2:18-21 – "Lakini ikiwa ninajenga tena kile nilichokwisha bomoa, basi nahakikisha kwamba mimi ni mhalifu. Maana, kuhusu sheria hiyo, mimi nimekufa; sheria yenyewe iliniua, nipate kuishi kwa ajili ya Mungu. Mimi nimeuawa pamoja na Kristo msalabani, na sasa naishi, lakini si mimi tena, bali Kristo anaishi ndani yangu. Maisha haya ninayoishi sasa naishi kwa imani, imani katika Mwana wa Mungu aliyenipenda hata akayatoa maisha yake kwa ajili yangu. Sipendi kuikataa neema ya Mungu. Kama mtu hufanywa mwadilifu kwa njia ya sheria, basi, Kristo alikufa bure!"*

### ***Watu wanaweza kumwamini Yesu bila kuokolewa wakiamini bila kutubu***

Kutubu ni lazima katika kumwamini Yesu kwa sababu Mungu aliagiza watu wote kutubu (Mdo 17:30). Ikiwa mtu atasema amemwamini Yesu lakini hajatubu, kumbe hajatimiza maana kamili ya kumwamini Yesu ili aokolewe. Tendo la kutubu linalohusika katika kumwamini Yesu linafafanuliwa katika Neno la Mungu. Kwa kuwa mawazo ya namna ya kufafanua neno hilo ni mengi, lazima tulitegemee Neno la Mungu ili tuelewe vizuri jinsi toba inavyohusika katika wokovu. Baadaye katika kitabu hiki tutafundisha kuhusu maana ya toba katika Neno la Mungu.

### ***Kumwamini Yesu Kristo kuna maana gani?***

Biblia ni wazi kwamba wokovu unapatikana katika kumwamini Yesu Kristo tu. Yesu mwenyewe alisema:

*Yohana 14:6 - "Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi."*

Lakini kumwamini Yesu ina maana gani? Kuamini ni hali ya kuwa na imani. Kumwamini Yesu ni kumtegemea. Ni kukubali hujiwezi na ni kukubali kumtegemea Yesu kwa kuwa unaamini yeye anaweza. Ni kuamini mambo fulani kuhusu jinsi Yesu alivyo na pia mambo fulani kuhusu kazi aliyofanya, anayofanya, na atakayofanya kwa ajili yetu. Ingawa kuna mambo mengi, yaliyo muhimu zaidi ni kwamba Yesu ni Mungu, Mwokozi, na Bwana.

### ***Kumwamini Yesu ni kuamini Yesu ni Mungu***

Kwanza, ni lazima mtu anayetaka kuokoka ajue na kuamini kwamba Yesu ni Mungu (Mk 14:61-62). Biblia inasema imani ya kweli inatakiwa kuamini kwamba Yesu ni Mungu.

*Yohana 20:21- "Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake."*

Yesu siyo Nabii tu, Yesu ni Mungu wa milele aliyezaliwa kama mwanadamu. Asingekuwa Mungu asingeweza kuishi maisha bila dhambi ili aweze kufa kwa ajili ya dhambi za wengine.

***Kumwamini Yesu ni kuamini yeye ni Mwokozi***

Pili, ni lazima mtu anayetaka kuokoka ajue na kuamini kwamba Yesu ni mwokozi.

*2 Petro 3:18 - "Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele."*

Ina maana gani kuwa mwokozi? Mwokozi ni yule anayeokoa mwingine kutoka uovu au hatari. Tuangalie mifano miwili ili tuelewe vizuri maana ya Yesu kuwa mwokozi. Katika mfano wa kwanza, Danieli yumo gerezani na lazima alipe faini ya 50,000 tsh ili atoke gerezani. Rafiki wa Danieli, Isaka, anakubali kulipa 25,000 tsh ili Danieli atoke gerezani. Je, 25,000 tsh zinatosha ili Danieli atoke? Hapana. Je, Danieli angemwita Isaka kuwa mwokozi wake? Hapana. Kulipa sehemu ya faini kusingemfanya Isaka kuwa mwokozi kwa sababu kwa njia hiyo Danieli hataokolewa na hali ya kufungwa.

Katika mfano wa pili Danieli bado yumo gerezani mpaka alipe 50,000 tsh. Mjomba wake anakubli kumlipia zote 50,000 tsh na hivyo Danieli anatoka gerezani. Je, Danieli angemwita mjomba wake mwokozi? Ndiyo, kwa sababu mjomba wake alimwokoa na hali ya kifungo.

Watu wengi wanamwita Yesu mwokozi bila kuamini Yesu aliwaokoa na adhabu ya dhambi zao. Ingawa wanamwita mwokozi, ukweli ni kwamba hawamwamini kama mwokozi. Kama Yesu hakutuokoa na dhambi zetu zote—tulizotenda, tunazotenda, na tutakazotenda—basi Yesu siyo mwokozi wetu.

Lakini ukweli ni kwamba Yesu ni mwokozi wetu. Kwa nini tunaweza kumwita mwokozi? Kwa sababu wakati alipokufa msalabani alibeba dhambi zetu zote na Mungu alimwadhibu kwa ajili ya dhambi zetu zote. Kwa kuwa aliadhibiwa kwa ajili yetu, ametuokoa sisi na matokeo yake ni kwamba hatutaadhibiwa sisi wenyewe.

Ili mtu amwamini Yesu kama mwokozi wa maisha yake ni lazima aweke imani yake yote katika Yesu na kazi aliyoifanya msalabani. Ni lazima aamini kifo cha Yesu kilimaliza deni au mshahara wa dhambi unaodaiwa na Mungu kwa ajili ya dhambi zake. Kuamini Yesu alikufa kwa ajili ya baadhi ya dhambi zake ina maana bado mtu huyu ataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zilizobaki. Lakini anayeamini kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zake zote ataokolewa kwa kuwa ataamini kweli kweli Yesu ni mwokozi wake.

***Kumwamini Yesu ni kuamini Yesu ni Bwana***

Tatu ni lazima mtu anayetaka kuokoka ajue na kuamini Yesu ni Bwana:

*Warumi 10:9 - "Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka." (angalia pia Mdo 2:36)*

Neno "Bwana" lina maana gani? Maana yake ni kuwa mtawala. Biblia inasema ni lazima mtu aamini Yesu ni Bwana wa maisha yake ili aokoke (Rum 10). Maana yake nini? Mtu anayeokolewa na Yesu, lazima aamini kwamba Yesu ni Bwana na mtawala wa maisha yake. Ni kusema mtu huyu anaamini anapaswa kumpa Yesu nafasi ya kwanza katika maisha yake na kwamba anapaswa kumtumikia Yesu na moyo wake wote akiishi kutimiza mapenzi ya Yesu.

Ni suala la imani na siyo matendo wala utiifu. Wakati mtu anapookoka anamwamini Yesu kuwa Bwana. Ndiyo kusema anakubali ukuu wa Yesu na haki ya Yesu kutawala maisha yake. Mtu akiamini hivyo pamoja na kumwamini Yesu kama mwokozi, mtu huyu ataokolewa. Baada ya kuokoka, imani hiyo ya kwamba Yesu ni Bwana, italeta mabadiliko katika maisha ya mtu huyo. Kabla hatujaokolewa, tuliishi kwa kufuata mapenzi yetu sisi wenyewe. Baada ya kuokolewa tunapaswa kuacha kufuata mapenzi yetu na badala yake tunapaswa kufuata mapenzi ya Yesu na kuishi kwa ajili yake. Ni hali itakayoonekana kwa wote, tena ni ishara ya kwamba mtu ameokoka. Kufanya mabadiliko katika maisa yetu ili tuwe watiifu wa Yesu hakutuokoi bali ni matokeo ya kawaida ndani ya maisha ya mtu aliyeokoka na kuamini Yesu ni Bwana.

***Kumwamini Yesu ni kumtegemea***

Tunamaanisha nini tunaposema kwamba anayeiamini Injili au kumwamini Kristo anapata wokovu? Mtu akikubali kwamba Injili ni kweli, je, tayari ameokoka? Hapana. Akikubali Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu na kufufuka tena, je, amepata wokovu? Hapana. Kukubali kwamba Yesu ni Mungu kunatosha kumfanya mtu aokoke? Hapana. Hizo zote ni habari zinazomhusu Yesu. Kuna habari nyingi za Yesu ambazo mtu anaweza kujua, na kukubali ni kweli, bila mtu huyu kuokoka. Kwa mfano, Yesu alifanya miujiza, Yesu alipaa kwenda mbinguni, Yesu alizaliwa duniani, n.k. Kukubali siyo imani kamili.

Copyright © 2017 GMI Publications
Kitu gani kinakosekana katika kukubali habari kuwa kweli? Kumtegemea Kristo. Kuamini siyo kukubali maarifa katika akili zetu bali ni kuyaamini maarifa yale katika mioyo yetu hadi tunapokuwa tayari kumtegemea Yesu kama mwokozi wetu.

***Kumwamini Yesu ni kumtegemea Yesu akiwa Mungu.***

Ni kutegemea Yesu ana uwezo wa kutuokoa kwa sababu yeye ni Mungu. Ni kutegemea Yesu ni mwenye nguvu zote na ana uwezo kutuokoa kwa sababu yeye ni Mungu. Ni kutegemea Yesu ni mwenye maarifa yote na anajua namna gani ya kutuokoa kwa sababu yeye ni Mungu. Ni kutegemea Yesu ni mwenye maarifa yote na hivyo anajua siku zetu zijazo na anajua ni wakati gani atatupeleka mbinguni. Ni kutegemea Yesu aliye Mungu habadiliki na kwa sababu hiyo ahadi zake hazitabadilika. Ni kutegemea Yesu anaposema ametuokoa ni jambo linaloaminika leo na kesho na milele.

***Kumwamini Yesu ni kutegemea Yesu ni Mwokozi.***

Ni kuacha kujaribu kujiokoa. Ni kuacha kutafuta njia nyingine ya kuokolewa. Ni kuamini wokovu tunao kwa sababu tunaamini maneno ya Yesu na pia tunaamini kazi aliyotufanyia, anayotufanyia, na atakayotufanyia. Kazi zake ni nyingi kwa niaba yetu katika kuwa mwokozi wetu. Tunategemea kazi hizo zote. Tunategemea alilipa mshahara wa dhambi zetu na hivyo tunapumzika katika yeye bila kuhangaika. Tunategemea alishinda mauti alipofanya kazi ya kufufuka na hivyo sisi hatutakufa mauti ya pili. Ni kutegemea yu hai na bado anafanya kazi katika maisha yetu ya kutubadilisha na kututakasa kama sehemu ya wokovu wetu (Flp 1:6, 2:12-13). Ni kutegemea kuna siku atakamilisha wokovu wetu wakati atakaporudi na kubadilisha miili yetu kuwa miili ya utukufu na kutupeleka mbinguni.

***Kujumlisha mawazo hayo ya namna ya kuokolewa***

Ni muhimu wewe kujikagua na kujiuliza ni aina gani ya imani uliyo nayo.

- Unasema unamwamini Yesu. Je, unaamini Yesu ni Mungu?
- Unasema unamwamini Yesu. Je, umeweka imani yako yote katika yeye bila kuongeza kitu kingine cha pili kama matendo mema n.k.?
- Unasema unamwamini Yesu. Umetubu kweli na kubadilisha mawazo yako kuhusu hali yako ya dhambi na kuhusu Yesu, jinsi alivyo na kazi aliyokufanyia?
- Unasema unamwamini Yesu. Je, unategemea kifo chake kililipa deni la dhambi zako zote, hata zile ambazo bado hujazitenda?
- Unasema unamwamini Yesu. Je, unakubali Yesu ni Bwana na je, imani hiyo imeleta mabadiliko yo yote katika maisha yako kiutendaji?

Kama umejibu hapana katika moja la maswali haya, inawezekana bado hujaokolewa na bado uko chini ya hukumu ya Mungu. Kama unataka kuokolewa leo, yaani kuokolewa na adhabu ya dhambi zako na kurudishwa katika uhusiano mzuri na Mungu chini ya utawala wake, na kupewa uzima wa milele – Mungu anasema lazima utubu kuhusu dhambi zako na umwamini Yesu kuwa mwokozi na Bwana wako. Ukiamini hivyo, Biblia inasema umeokolewa!

# 12. Toba Inahusikaje Katika Wokovu?

***Kutubu hakuleti wokovu***

Mtu akipenda kuokolewa, anatakiwa kufanya nini? Watu wengi watajibu kwamba anatakiwa **kutubu**. Lakini Biblia inafundisha kwamba kuna sharti moja tu ili aupokee wokovu. Sharti hilo ni **kuiweka imani katika Bwana Yesu**: *"Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka"* (Mdo 16:31).

Toba siyo njia ya kuokoka. Kama tulivyokwishajifunza, imani ni njia peke ya kuokoka. Lakini imani ya kweli, inayoleta wokovu, inatakiwa ijengwe juu ya msingi wa toba. Mtu akikosa kutubu, anaweza kuamini bure. Basi, tuchunguze kwanza maana ya toba au kutubu.

Wengi wanachanganyikiwa siku hizi kuhusu maana ya "kutubu" kwa jinsi inavyohusika katika wokovu. Wakristo wengine wanasema kwamba kutubu ni kuacha dhambi. Wengine wanasema kutubu ni majuto.

Copyright © 2017 GMI Publications

Tutaanza kwa kuyachunguza mawazo haya kuhusu toba na kuona kwa nini mawazo haya siyo sahihi. Baada ya hayo, tutajifunza yale Biblia inayofundisha kuhusu toba.

***Kutubu si kuacha dhambi***

Wengine wanasema kutubu ni kuacha kutenda dhambi. Wanadai kabla mtu hajaja kwa Kristo na kumwamini ni lazima aachane na dhambi ndani ya maisha yake kwanza. Yaani, wanaamini ni lazima mtu abadilike kabla hajaokoka. Lakini tutaona ufafanuzi huo siyo sahihi kwa sababu wanadamu, peke yao, hawawezi kuacha kutenda dhambi asilimia mia katika maisha yao.

Ingekuwa kweli kwamba maana ya kutubu ni kuacha kutenda dhambi, matokeo yake ni kwamba hakuna ambaye angeweza kuokoka. Kwa nini? Kwa sababu Biblia inasema wote wasioamini wamekufa kiroho na wako chini ya utawala wa Shetani. Ni lazima wasiomwamini Yesu wamtii mtawala wao, yaani, ni lazima watende dhambi. Hivyo, wasioamini hawawezi kuacha kutenda dhambi kwa kuwa wanatawaliwa na Shetani na hali yao ya kuwa watumwa wa dhambi. Hakuna kati yetu, hata Mkristo mmoja, ambaye ameacha kutenda dhambi asilimia mia. Ikiwa sisi Wakristo, tulio na Roho Mtakatifu ndani yetu, hatuwezi kuacha kutenda dhambi, je, atawezaje asiyeamini ambaye ni mtumwa wa Shetani? Jibu ni kwamba hawezi kuacha kutenda dhambi. Hivyo, maana ya kutubu haiwezi kuwa kuacha kutenda dhambi. Mungu hawezi kumdai mwanadamu kitu asichokiweza.

***Kutubu si majuto wala huzuni***

Mara nyingi huzuni au majuto yanasindikiza toba. Lakini huzuni au majuto siyo toba yenyewe. 2 Wakorintho 7:10 inasema: *"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto; bali huzuni ya dunia hufanya mauti."* Hapa Biblia inataja aina mbili za huzuni. Aina moja ya huzuni ni *"huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu."* Huzuni hii inatangulia na kuleta toba, lakini siyo toba yenyewe. Huzuni ya pili inaitwa *"huzuni ya dunia."* Huzuni hii siyo toba wala haileti toba. Inaleta mauti. Maana yake, huzuni hii ni huzuni ya mtu anayehuzunika bila kutubu.

Katika Mathayo 19:16-26, kijana tajiri alimwuliza Yesu afanye kitu gani chema ili apate uzima wa milele. Alikuwa anayategemea matendo mema ili aokolewe. Yesu alitumia sheria kumwonesha matakwa makamilifu ya Mungu. Baada ya kusikia yale aliyotakiwa kuyafanya, hakupenda kuyatimiza. Kijana huyu aliendа zake kwa huzuni. Huzuni ya kijana tajiri ilileta toba? Hapana. Alikuwa na huzuni ya aina gani? Huzuni ya kidunia. Tumeona kwamba huzuni au majuto siyo toba. Huzuni inaweza kuleta toba au kuisindikiza toba, lakini pia mara nyingine huzuni haifuatani na toba.

***Kutubu ni kuyabadilisha mawazo***

Tumeona kwamba kutubu siyo kuacha dhambi wala kuwa na hisia za huzuni. Sasa, tuone yale Biblia inayofundisha kuhusu toba. Maana ya neno "kutubu" katika Agano Jipya ni "kubadili mawazo". Toba ni mabadiliko ya mawazo kuhusu tendo, neno, au uamuzi fulani. Kwa mfano, mtu fulani anaweza kutenda tendo ambalo halioni kuwa baya, kusema neno ambalo halioni kuwa baya, kuamua jambo ambalo halioni kuwa baya, au kuishi maisha ambayo hayaoni kuwa mabaya. Lakini, baadaye anaweza kufika mahali pa kugundua kwamba tendo, au neno, au uamuzi, au maisha yake, kweli yalikuwa mabaya. Mabadiliko yake katika mawazo haya ni toba. Kwa mfano mwingine, mtu anaweza kuamua kufanya kitu fulani lakini baadaye anabadili uamuzi wake. Tunasema kwamba mtu yule ametubu. Mabadiliko ya mawazo yake ni toba. Tazama kwamba toba ni mabadiliko ya ndani; ni mabadiliko ya mawazo au mtazamo na siyo mabadiliko ya matendo.

***Mifano ya toba katika Biblia***

Tutaangalia sasa mifano ya matumizi ya neno "toba" au "kutubu" katika Biblia. Mifano hii itatusaidia kufahamu kwamba kutubu ni kuyabadili mawazo.

***Mfano wa toba katika maisha ya Sulemani***

Tunapata mfano mzuri wa maana ya toba katika 1 Wafalme 8:46-49. Mfalme Sulemani alikuwa amemaliza kujenga hekalu. Aliwaita Waisraeli wote kusherehekea kuliweka wakfu hekalu. Mfalme Sulemani alisali na akamwomba Mungu hivi:

"*Ikiwa wamekutenda dhambi, (maana hakuna mtu asiyetenda dhambi), hata ukawaghadhibikia, ukawatia katika mikono ya adui zao, wawachukue mateka mpaka nchi ya adui zao, iliyo mbali au iliyo karibu; basi,* ***wakijirudia nafsi zao*** *katika nchi ile watakayochukuliwa mateka,* ***wakitubu****, na kukusihi*

Copyright © 2017 GMI Publications
*katika nchi ya hao waliwachukua mateka, wakisema, **Tumekosa, tumefanya ukaidi, tumetenda maovu**; watakaporejea kwako kwa mioyo yao yote, na kwa nia zao zote, katika nchi ya adui zao, waliowachukua mateka, wakikuomba, kwa kuikabili nchi yao, uliyowapa baba zao, na mji huu uliouchagua, na nyumba hii niliyoijenga kwa jina lako; basi, uyasikie maombi yao na dua yao, huko mbinguni, makao yako, ukaitetee haki yao*."

Katika sala yake, Mfalme Sulemani anataja uwezekano wa Waisraeli kuacha kumfuata Mungu na kuziabudu sanamu. Ikiwa watafanya hivyo na ikiwa Mungu atawaadhibu, alisema kwamba inawezekana *"watajirudia nafsi zao".* Maana ya *"kujirudia nafsi zao"* ni nini? Ni kubadilisha mawazo yao kuhusu uovu wao. Ndiyo kutubu. Kutubu kwao kutahitajika wakimkosea Mungu kwa kuabudu miungu ya uongo bila kujali. Wanapofika mahali pa kugundua kwamba walikuwa wamefanya vibaya, ndipo wangetubu na kusema, *"Tumekosa, tumefanya ukaidi, tumetenda maovu."* Toba yao inatoka ndani yao. Ikiwa ni toba ya kweli, Mfalme Sulemani alisema itaoneshwa kwa jinsi watakavyomrejea Mungu. Kurejea kwa Mungu siyo toba, lakini ni matunda ya toba yao ya kweli.

***Mfano wa toba katika mifano ya Yesu***

Bwana Yesu alitoa mfano wa kijana aliyetubu (Mt 21:28-32). Kijana huyo alikuwa amesema kwamba hatatumika shambani mwa baba yake, lakini baadaye alitubu, na akaenda shambani. Maana yake, aliyabadili mawazo yake na alikubali kufanya kazi shambani. Hapa tunaona kwamba kutubu kunamaanisha kuyabadili mawazo. Je, kijana aliachana na dhambi? Hapana. Je, alijutia dhambi zake? Hapana. Kijana alibadili mawazo yake kuhusu jibu ambalo alikuwa amempa baba yake na baada ya kuyabadili mawazo akafanya kazi.

***Mfano wa toba katika Luka***

Mfano mwingine wa toba ni katika Luka 17:3-4:

*"Jilindeni; kama ndugu yako akikosa, mwonye; akitubu msamehe. Na kama akikukosa mara saba katika siku moja, na kurudi kwako mara saba, akisema, Nimetubu, msamehe."*

Hapa anayetubu anatubu kwa ajili ya nini? Anatubu kuhusu kosa alilomtendea mwingine. Anayabadili mawazo na kuona kwamba tendo alilomtendea mwenzake lilikuwa baya; kwa hiyo anautafuta msamaha.

***Jumla ya fundisho la mifano hii***

Mifano hii inathibitisha kwamba maana ya kutubu ni kuyabadili mawazo. Mifano hii inaonesha pia kwamba toba ni mabadiliko yanayofanyika ndani ya mtu, siyo mabadiliko ya nje. Ni mabadiliko ya mawazo, siyo mabadiliko ya matendo. Mabadiliko ya matendo ni tokeo la toba, lakini siyo toba yenyewe.

***Toba iliyo msingi wa imani***

Katika mifano ya hapo juu, watu wanatubu kwa ajili ya mambo mbalimbali (kuabudu sanamu, kutofanya kazi shambani, kumkosea mwingine). Katika mifano hii, toba yao siyo toba inayohusiana na wokovu. Sasa tunataka kuangalia toba inayohusiana na wokovu. Tunajua kwamba toba inatangulia imani inayoleta wokovu, na tunajua kwamba toba ni mabadiliko ya mawazo. Basi, toba hiyo inayotangulia imani iletayo wokovu ni mabadiliko ya mawazo gani? Ni kubadili mawazo kuhusu nini?

***Toba ni kuyabadili mawazo kuhusu upekee wa Mungu***

Watu wanaweza kuwa na mawazo mengi ya uongo kuhusu Mungu. Lakini anayependa kuokolewa anatakiwa kuyabadili mawazo yake kuhusu Mungu ili yafuatane na ukweli wa Biblia. Kwanza mtu anatakiwa kukubali kwamba Mungu ni mmoja na hakuna mwingine. Kama mtu anaamini Mungu wa Biblia ni mmojwapo miongoni mwa miungu mingi, kweli hajui jambo hilo la msingi kuhusu Mungu.

Waisraeli walizungukwa na watu walioiabudu miungu ya uongo. Kabla hawajaingia nchi ya ahadi, Mungu alisisitiza kwamba yeye pekee ni Mungu katika Kumbukumbu la Torati 6:4. Kifungu hiki ni msingi wa imani ya Kiyahudi. Kinasema, *"Sikiliza, Ee Israeli; BWANA, Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja."* Wengine hawaoni umuhimu wa kuwashuhudia watu kwamba Mungu ni mmoja. Tukichunguza huduma na mahubiri ya Bwana Yesu, tunaona kwamba yeye hakuwafundisha Wayahudi kwamba Mungu ni mmoja. Kwa nini? Kwa sababu Wayahudi tayari waliamini kwamba Mungu ni mmoja. Mtume Paulo alizoea kuwahubiria watu waliokusanyika kwenye masinagogi. Alipowahubiria Injili, je, alianza na

mafundisho kwamba Mungu ni mmoja? Hapana. Kwa nini? Kwa sababu wale waliohudhuria katika masinagogi tayari walijua kwamba Mungu ni mmoja. Lakini, wakati mtume Paulo alipowashuhudia wapagani wa Athene, watu ambao waliabudu miungu mbalimbali bila kumjua Mungu wa kweli, alianza kwa kuwashuhudia nini (Mdo 17:22-34)? Je, alianza kwa kushuhudia kwamba walikuwa wenye dhambi na kwamba Kristo alikufa kwa ajili yao? Hapana. Hakulitaja jina la Yesu. Alianza kwa kuwafundisha kuhusu Mungu wa kweli.

Hii ina maana kwetu sisi kwa sababu watu wengine hapa Tanzania wanaabudu miungu ya uongo. Sisi wainjilisti tunatakiwa kugundua kwanza kama yule tunayemshuhudia anaamini kwamba Mungu ni wa pekee. Mtu akiunganisha imani katika Yesu na imani yake katika miungu mingine, je, Mungu atamfurahia na kumkubali? Hapana, mtu yule atakuwa anaamini bure. Hivyo lazima mtu anayekuja kwa Kristo atubu na kubadili mawazo yake kuhusu ummoja na upekee wa Mungu wa kweli.

***Toba ni kuyabadili mawazo kuhusu utakatifu wa Mungu***

Jambo la pili ambalo mtu anapaswa kuyabadili mawazo yake ni utakatifu wa Mungu. Watu wengi hawaufahamu ukweli wa kwamba Mungu ni mtakatifu. Wanafikiri kwamba Mungu atawakubali ingawa wametenda dhambi. Wanatakiwa kuyabadili mawazo yao na kukubali kwamba Mungu mtakatifu hawezi kushirikiana na mwenye dhambi. Inabidi mtu aelewe ni lazima awe mtakatifu ili aweze kushirikiana na Mungu. Hata kama anajitahidi kumpendeza Mungu, jitihada zake ni bure kwa sababu yeye bado ni mwenye dhambi na mchafu mbele za Mungu. Mungu hatamkubali hata kidogo asipokuwa mtakatifu. Katika kuyabadili mawazo yake kuhusu utakatifu wa Mungu, badala ya kujitegemea kujifanya sawa mbele ya Mungu, mtu anatakiwa amtegemee Mungu kumfanya mtakatifu.

***Toba ni kuyabadili mawazo kuhusu haki ya Mungu***

Jambo la tatu ambalo mtu anatakiwa kuyabadili mawazo yake ni haki ya Mungu. Wengine wanafikiri kwamba Mungu ataachilia dhambi zao wakizichanganya na matendo mema. Wanapaswa kuyabadili mawazo haya na kukubali kwamba Mungu ni mwenye haki, yaani Mungu anadai dhambi zote ziadhibiwe. Adhabu ya dhambi ni mauti; yaani kutengwa na Mungu milele motoni. Kwa sababu Mungu anadai kila dhambi iadhibiwe, mtu hawezi kujitetea mbele ya Mungu. Mtu asidhani kwamba ataweza kujifanya akubaliwe na Mungu kwa sababu ya matendo yake mema. Yule anayeyategemea matendo yake mema kumwokoa, anahitaji kuulizwa namna gani matendo yake yataifuta adhabu ya dhambi zake. Mwisho anapaswa kutubu mawazo haya na kuyabadilisha ili mawazo yake yaendane na ukweli kuhusu haki ya Mungu.

***Toba ni kuyabadili mawazo kuhusu dhambi.***

Toba iliyo msingi wa imani ya kweli pia ni mabadiliko ya mawazo ya mtu kuhusu dhambi zake. Mpagani anaweza kuona dhambi zake (au maisha yake ya dhambi) siyo mbaya. Anaweza hata kuzipenda na kuzifurahia dhambi zake. Au anaweza kukubali kwamba dhambi zake nyingine ni mbaya, lakini siyo mbaya sana. Kama mtu huyo atatubu, anatakiwa kuwa na mabadiliko gani katika mawazo yake yahusuyo dhambi zake? Badala ya kuona dhambi zake kama kitu cha kuleta furaha au kitu kisicho kibaya sana, anatakiwa kuziona dhambi zake kama Mungu anavyoziona.

Mungu anaziona dhambi zake namna gani? Dhambi ni kitu kilichomtenganisha mwanadamu na Mungu. Dhambi zake zinamfanya kuwa adui wa Mungu. Dhambi zake zinamchafua kabisa na hana jinsi ya kujisafisha. Dhambi zake zinamfanya asiwe na njia ya kujipatanisha na Mungu. Dhambi zake zinamchukiza Mungu sana na kuileta ghadhabu ya Mungu na hukumu ya milele motoni. Mtu anayetubu kweli atayabadili mawazo yake kuhusu dhambi na kukubali kwamba mambo haya ni ya kweli.

***Tokeo la toba***

Mtu akitubu, yaani, akiyabadili mawazo yake kuhusu Mungu na kuhusu dhambi zake, basi, tokeo gani litafuata? Mtu akiona kwamba: 1) Ametengwa na Mungu mtakatifu; 2) Yeye ni adui wa Mungu; 3) Dhambi zake zimemchafua kabisa mbele ya Mungu mtakatifu; 4) Dhambi zake zinamfanya asiwe na njia ya kumkaribia Mungu wala kujipatanisha naye; 5) Dhambi zake zinamletea ghadhabu ya Mungu; 6) Mungu mwenye haki atamhukumu na kumwadhibu katika moto wa milele, jibu lake linatakiwa kuwa nini? Jibu linalohitajika litafanana na jibu la Isaya alipomwona Mungu na kugundua uchafu wa dhambi zake.

***Tokeo la toba ni kuwa tayari kumwamini Yesu***

*Isaya 6:5 – "Ole wangu! Kwa maana nimepotea."*

Copyright © 2017 GMI Publications

Mtu asipojibu hivyo ina maana hajamwelewa Mungu jinsi alivyo na hajaziona dhambi zake kama Mungu anavyoziona. Ina maana hajatubu kweli kwa kuwa hajabadilisha mawazo yake kuhusu mambo hayo.

Mtu anayetubu, anayeyabadili mawazo yake kuhusu Mungu na kuhusu dhambi zake ili yapatane na ukweli wa Neno la Mungu, huyo sasa yu TAYARI kuisikia Injili na kuiweka imani yake katika Kristo. Mtu huyu aliyetubu kweli, je, ameokoka? Hapana. **Hajaokolewa bado** kwa sababu bado hajalitimiza sharti lile moja la wokovu la kumwamini Kristo! Lakini sasa mtu huyu ni TAYARI kuipokea Habari Njema ya Yesu na kuokolewa. Ndiyo maana tunasema kwamba toba si njia ya wokovu, lakini ni msingi wa imani inayookoa.

***Tokeo la toba ni kukusudia kutotenda dhambi tena***

Baada ya mtu kubadili mawazo yake kuhusu dhambi na kugundua ubaya na matokeo ya dhambi zake, mtu huyu hupaswa kufanya uamuzi moyoni. Kwa kawaida anatakiwa kukusudia moyoni mwake kutotenda dhambi tena. Kwa mfano, mtu anapotubu (yaani anabadili mawazo yake) kwamba kusema uongo kunamkasirisha Mungu, baada ya hapo anapaswa aamue asiendelee kusema uongo.

Tuangalie tofauti kati ya kukusudia kuacha kutenda dhambi na hali halisi ya kuacha kutenda dhambi. Ni muhimu tuone tofauti hiyo. Kuacha kutenda dhambi ina maana kweli kweli mtu huyu hatatenda dhambi tena katika maisha yake. Lakini, mtu akitubu na kubadili mawazo yake kuhusu kusema uongo, hivi kweli ataishi miaka mingi iliyobaki katika maisha yake bila kusema uongo tena? Hapana. Bila shaka atarudia dhambi hiyo ingawa amekusudia kutosema uongo tena. Tokeo moja la kutubu ni kukusudia kutorudia dhambi tena. Mtu anaweza kujaribiwa na kuanguka katika dhambi tena lakini kwa kuwa alitubu, ina maana, hataki kufanya dhambi tena. Kwa sababu mtu aliyetubu na kuelewa ubaya wa dhambi hataki kuendelea katika dhambi, akianguka, ataungama dhambi yake kwa Mungu na kuendelea na uamuzi ule ule wa kukusudia kutotenda dhambi.

Kwa mfano wakati mtu anatembea shambani, akiona panya kwenye njia, je, atageuka na kukimbia? Hapana. Kwa nini? Kwa sababu anajua panya huyu siyo hatari kwake. Lakini mtu huyu akiona nyoka kwenye njia atafanya nini? Atajitahadharisha. Aidha atageuka na kukimbia au atatumia kifaa fulani kumwua nyoka huyu. Kwa nini akimbie? Kwa sababu anajua nyoka ni hatari kwake na anamtambulisha kuwa adui wake. Kwa sababu hiyo, wanadamu hawataki hata kuwa karibu na nyoka.

Kwa mfano mwanamke akiingia katika nyumba yake na kuona nyoka mdogo, je, atasema, "nitamwacha nyoka huyu kwa kuwa ni mdogo"? Hapana. Hata nyoka mdogo ni hatari na ni adui wa mwanadamu. Hawezi kumwacha nyumbani, lazima amwue.

Jinsi tunavyojisikia kuhusu nyoka ni sawa na jinsi mtu aliyetubu anavyojisikia kuhusu dhambi. Tunapaswa kuchukia dhambi zote, ziwe ndogo au ziwe kubwa. Tunapaswa kutambua dhambi kuwa adui yetu. Hatupaswi kuvumilia dhambi katika maisha yetu kwa kuwa tulishabadilisha mawazo yetu kuhusu ubaya na uharibifu wa dhambi. Yaani, tumegundua dhambi ni mbaya sana hadi inaleta kifo cha milele.

***Kutubu ni hali endelevu***

Jambo la mwisho tunalohitaji kujifunza ni kwamba toba ya kweli haiishi baada ya muda mfupi. Anayebadilisha mawazo yake kuhusu Mungu na dhambi anabaki na mawazo haya kwa maisha yake yote kama ametubu kweli. Kutubu ni uamuzi unaompeleka kwenye kumwamini Yesu lakini pia ni uamuzi wa kuendelea nao kila siku ya maisha yake. Ni vizuri kwa Wakristo kujikumbusha kila siku jinsi dhambi ilivyo mbaya na jinsi dhambi inavyomhuzunisha Mungu. Kama vile nyoka ni adui wetu maisha yetu yote, vilevile anayetubu kuhusu dhambi ajue dhambi ni adui wake kila siku ya maisha yake. Kwa sababu hiyo aliyetubu kweli kweli hawezi kuzoea dhambi kuwa jambo la kawaida katika maisha yake. Anaweza kutenda dhambi lakini atakusudia kutotenda dhambi tena kwa sababu alishabadilisha mawazo yake kuhusu ukweli wa dhambi. Na kwa msaada wa Roho Mtakatifu atafaulu zaidi na zaidi anapokua katika Kristo.

# 13. Kunatokea Nini Mtu Anapookolewa?

***Mtu anatendewa mengi anapookoka***

Copyright © 2017 GMI Publications

Wokovu ni tendo la Mungu kumkomboa mwanadamu kutoka katika utawala wa Shetani na dhambi, na kutoka chini ya ghadhabu na hukumu ya Mungu, kumpa uhai kiroho, na kumrudisha mwanadamu chini ya utawala wa Mungu ili awe na ushirikiano na Mungu.

Wokovu siyo kusamehewa dhambi tu, bali ni zaidi ya kusamehewa dhambi. Pia, wokovu ni zaidi ya kuhesabiwa haki. Wokovu unaleta mabadiliko katika uhusiano wetu na Shetani na dhambi, unaleta mabadiliko katika uhusiano wetu na Mungu, na unaleta mabadiliko ndani yetu. Mungu anatutendea mambo mengi mazuri na ya ajabu anapotuokoa!

***Mungu peke yake anahusika kila upande wa wokovu***

Tutaona ukweli hapo chini wa kwamba wokovu ni kazi ya Mungu. Wokovu unaanzishwa na Mungu, unatimizwa na Mungu na unatunzwa na Mungu.

## 14. Wokovu Unaleta Mabadiliko Gani Katika Uhusiano Wetu na Shetani na Dhambi?

***Kila mtu anazaliwa akiwa chini ya mamlaka ya Shetani na dhambi***

Tunapookolewa, tunakombolewa kutoka katika mamlaka ya Shetani na dhambi. Kwa sababu Adamu aliamua kumfuata Shetani na kumwasi Mungu, alikuwa mwenye dhambi.

*Warumi 5:12 - "Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi."*

Adamu alipokea asili ya dhambi inayoitwa "utu wa kale" au "mwili" katika Biblia. Dhambi ilianza kumtawala na alikuwa mtumwa wa dhambi. Pia, Adamu alipomfuata Shetani, alijiweka chini ya mamlaka yake, hivyo Shetani alikuwa mtawala wake. Kwa sababu ya dhambi ya Adamu, wazao wake wote wanazaliwa wakiwa na asili ya dhambi, wakiwa chini ya utawala wa Shetani, na watumwa wa dhambi.

***Kutawaliwa na Shetani na dhambi ni kuwatumikia***

Inamaanisha nini kuwa chini ya utawala wa Shetani na kuwa mtumwa wa dhambi? Inamaanisha kwamba sisi tunaishi maisha ya kuyafuata mapenzi ya Shetani na dhambi na pia tunatii Shetani na dhambi. Tunafanya dhambi na kuifurahia. Kwa nini? Kwa sababu ndivyo watawala wetu wanavyotaka kwetu.

***Aliyeokoka hatawaliwi na Shetani tena***

Tunapookolewa, Mungu anatukomboa kutoka katika mamlaka ya Shetani na utumwa wa dhambi.

*Warumi 6:6-7 – "utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi."*

Hii inamaanisha nini? Kwanza, Shetani siyo mtawala wetu tena. Kristo alimshinda Shetani na pepo wote msalabani (Kol 2:15; Ebr 2:14-15). Hivyo, kama Wakristo, hatupaswi kuwatii, kuwatumikia, wala kuwaogopa Shetani na pepo tena. Tuko huru na mamlaka yao.

Mfano huu utatusaidia kuelewa ni mabadiliko gani yanayotokea kwenye uhusiano wa Mkristo na Shetani wakati Mkristo anapookolewa. Nimetunga mfano huu mwenyewe kuhusu mtoza ushuru anayeitwa Anatory.

Anatory alikuwa mtoza ushuru vijijini mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika mwaka 1990 na kuendelea. Alikuwa mtu mwovu na mara nyingi alidai kodi kuliko watu walivyopaswa kulipa kulingana na sheria. Hata wale ambao hawakutakiwa kulipa kodi, aliwatoza kwa nguvu. Watu hawakumpenda kabisa lakini hawakuweza kumfanya cho chote kwa kuwa alikuwa mtumishi wa serikali aliyekubaliwa na wakubwa wake.

Katika mwaka 1996 vita ilianza katika nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo yenye kusudi la kumfukuza rais wao. Wakati wapinzani walipokaribia mji mkuu, Anatory alijua siku zake za kufanya kazi serikalini zilikuwa zinaisha. Tarehe 17 ya mwezi Mei wapinzani walishinda jeshi la serikali.

Wakati Anatory alipoamka tarehe 17 ya mwezi Mei, alijua amepoteza kazi yake. Lakini kwa kuwa habari zilifika vijijini polepole alifanya safari ya mwisho kukusanya kodi kabla habari zile hazijafika.

Copyright © 2017 GMI Publications

Alifika katika kijiji cha kwanza asubuhi na mapema. Mtu wa kwanza aliyekutana naye akamdai kuku. Kwa sababu hakujua Anatory hakuwa na mamlaka, mtu huyu alimpa kuku. Anatory alipanga kupitia vijiji vingi siku ile akidai pesa na chakula kama malipo ya kodi za watu ili abaki nazo mwenyewe.

Alipofika katika kijiji cha pili watu walikuwa wameshasikia habari za kuanguka kwa serikali. Lakini Anatory aliamua kuwadai ingawa alijua wanafahamu habari hizo. Pamoja na kwamba watu walijua Anatory hakuwa na mamlaka juu yao tena mmoja alikuwa amezoea kumwogopa na hivyo kutokana na hofu yake alikubali kumlipa.

Lakini wengine waliitika tofauti. Wakati Anatory alipowaendea waliwaita majirani wao waje kusaidia kumpiga Anatory na kumfukuza kijijini. Anatory alikuwa amepoteza mamlaka yake na hawakuweza kumkubali tena. Anatory alikimbia akijua wanaweza hata kumwua.

Katika hadithi hii Anatory ni mfano wa Shetani na wanakijiji ni Wakristo. Wakristo wote wamewekwa huru na Shetani, hawako chini ya mamlaka yake tena. Lakini Wakristo wengine wanamwitikia Shetani kama wanakijiji wa kijiji cha kwanza. Hawajui kwamba wamewekwa huru na Shetani na hivyo wanaendelea kumruhusu Shetani kuwatawala na kuwashawishi kutenda dhambi, yaani wenyewe wanakubali kumtii. Wakristo wengine ni kama yule mmoja katika kijiji cha pili. Wanajua kwamba Shetani hana mamlaka juu yao tena lakini kwa sababu mbalimbali wanaamua kumtii Shetani badala ya kumtii Mungu, yaani, wanampa Shetani utawala wakati hanao. Lakini Mungu anataka Wakristo wote kuwa kama wale wengine katika kijiji cha pili. Wajue Shetani hana mamlaka juu yao na hivyo wamfukuze katika maisha yao kwa kukataa kumtii. Yakobo 4:7-8 inasema,

*"Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia. Mkaribieni Mungu, naye atawakaribia ninyi. Itakaseni mikono yenu, enyi wenye dhambi, na kuisafisha mioyo yenu."*

Pili, tunapookolewa sisi si watumwa wa dhambi tena. Yesu alipokufa, utu wa kale ulisulubishwa pamoja naye (Rum 6:6-7; Gal 5:24). Kusulubiwa kwa utu wa kale kuliuvunja utawala wa dhambi juu yetu. Tunakuwa huru na dhambi. Hivyo hatupaswi tena kufanya dhambi kwa kuwa dhambi au utu wa kale hauwezi kutulazimisha kufanya dhambi.

***Aliyekombolewa yuko huru***

Kukombolewa kutoka katika mamlaka ya Shetani na dhambi ni kuwekwa HURU na mamlaka ya Shetani na dhambi katika maisha yetu. Inawezekana sasa kuishi tukiwa huru bila kutenda dhambi!

*Warumi 6:22 – "Lakini sasa mkiisha kuwekwa huru, na kuwa mbali na dhambi, na kufanywa watumwa wa Mungu, mnayo faida yenu, ndiyo kutakaswa, na mwisho wake ni uzima wa milele."*

**Maana ya kukombolewa kutoka katika mamlaka ya Shetani na dhambi:** Tendo la Mungu la kumfanya yule anayemwamini Kristo kuwa huru na mamlaka ya Shetani na dhambi katika maisha yake.

**Matokeo ya kukombolewa kutoka katika mamlaka ya Shetani na dhambi katika maisha ya Mkristo:** Mkristo ataweza kuishi maisha huru bila kulazimishwa kutenda dhambi kwa sababu hatawaliwi na Shetani wala dhambi tena.

**Swali la Kutafakari:** Maisha yako yanaoneshaje kwamba uko huru na utawala wa Shetani na dhambi?

# 15. Wokovu Unaleta Mabadiliko Gani Katika Uhusiano Wetu na Mungu?

Tunapookolewa, uhusiano wetu na Mungu unabadilishwa katika sehemu mbalimbali. Tutaona jinsi tunavyorudishwa chini ya utawala wa Mungu, jinsi tunavyobatizwa katika Mwili wa Kristo, jinsi tunavyounganishwa na Kristo, jinsi tunavyopokea Roho Mtakatifu, tunavyohesabiwa haki, tunavyotakaswa, tunavyofanywa watoto wa Mungu, tunavyosamehewa, na tunavyopokea uzima wa milele.

## A. Tunapookolewa, Tunarudishwa Chini ya Utawala wa Mungu.

***Kuwa huru na dhambi ni kurudishwa chini ya utawala wa Mungu***

Kabla Adamu hajafanya dhambi, alikuwa chini ya utawala wa Mungu. Lakini, alipofanya dhambi, alijiweka chini ya mamlaka ya Shetani. Mungu alipotukomboa kutoka katika mamlaka ya Shetani na dhambi, hakutuacha kujitawala wenyewe. Aliturudisha chini ya utawala wake ili awe mtawala wetu tena.

*Wakolosai 1:13 – "Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake."*

Kuwa huru na utawala wa dhambi siyo kuwa huru kufanya dhambi! Kuwa huru na utawala wa dhambi ni kutokuwa mtumwa wa dhambi tena na kuwa mtumwa wa Mungu (Rum 6:22). Mkristo aliye mtumwa wa Mungu anapaswa kumtii nani? Mungu. Anaweza kuishi vile anavyotaka tu? Hapana. Mtumwa anapaswa kumtii na kuyafanya mapenzi ya mtawala wake. Kwa kuwa Mungu ni mtawala wetu, tunatakiwa kuyafanya mapenzi yake.

**Maana ya kurudishwa chini ya utawala wa Mungu**: Tendo la Mungu kumweka katika ufalme wake yule anayemwamini Kristo.

**Matokeo ya kurudishwa chini ya utawala wa Mungu katika maisha ya Mkristo:** Mkristo atamtii Mungu na kuishi maisha yanayolingana na mapenzi ya Mungu kwa sababu anafahamu kwamba anatawaliwa na Mungu.

**Swali la Kutafakari:** Unaoneshaje kwamba wewe ni mtumwa wa Mungu?

## B. Tunapookolewa, Tunabatizwa Katika Mwili wa Kristo.

Mungu anatumia mifano mingi kuonesha hali au mahali pa kila Mkristo. Mfano wa kwanza tuliouona ni kwamba Mkristo ni mtumwa katika ufalme wa Mungu. Mfano mwingine, tutakaoangalia sasa, ni kumwelewa Mkristo kuwa ndani ya "Mwili" wa Kristo. Biblia inafundisha kwamba Bwana Yesu Kristo ni kichwa cha mwili huo (Efe 4:15; 5:23; Kol 1:18). Ndiyo maana mwili huo unaitwa Mwili wa "Kristo". Kila Mkristo ni sehemu au mshiriki wa Mwili wa Kristo. Hivyo, Mwili wa Kristo ni Wakristo wote kwa pamoja (Rum 12:4-5; 1 Kor 12:12-27; Efe 3:6; 4:25; 5:30).

### *Kazi za kichwa na mwili*

Katika somo hilo kuhusu maana ya Mwili wa Kristo tutaangalia kazi za kichwa na pia kazi za mwili. Sisi Wakristo tunapaswa kufahamu wajibu wetu kama wajumbe wa Mwili wa Kristo kwa kuwa ndiyo sababu moja ya Mungu kutuokoa.

Kazi ya kichwa cha mwili huo ni nini? Kazi ya kichwa ni kuongoza na kuamuru mwili. Kila tendo na kila neno ambalo mwili unafanya na kusema unaongozwa na kichwa. Mkono ukishika kitu, unafanya hivyo kwa sababu umeagizwa na kichwa kufanya hivyo. Yesu Kristo anaitwa Bwana, Mfalme, na Kichwa. Maana ya maneno hayo yote ni kwamba Yesu ni mtawala wa Wakristo wote.

Kazi ya mwili ni nini? Kazi ya mwili ni kutimiza mawazo, mapenzi, na maagizo ya kichwa.

### *Mwili usioshughulika hauna afya*

Jambo moja tunalojua kuhusu miili yetu ni kwamba hatuna raha kama miili yetu haina shughuli za kushughulika nazo. Nani angekuwa na raha kubaki kitandani wiki zima? Mtu akibaki kitandani kwa muda huo tungesema nini kuhusu mtu huyu? Tungesema mtu huyu anaumwa. Mtu mwenye afya hawezi kulala muda wote huo bila kuamka na kufanya shughuli fulani. Ndivyo ilivyo kwa kila Mkristo aliye katika Mwili wa Kristo. Wote wanatakiwa kushughulika wakitii maagizo ya kichwa. Wasipofanya, mwili unakosa afya.

### *Kila kiungo cha mwili ni muhimu*

Tunajua kila sehemu ya mwili lazima ifanye kazi yake ili mwili uwe na afya na maendeleo. Hata sehemu ndogo za mwili ni muhimu na za lazima. Mtu akiumiza kidole chake, mkono wake utashindwa kutimiza kazi yake ipasavyo. Kila kiungo cha mwili kina kazi yake iliyo muhimu. Mungu amepanga mapenzi yake yatimie kupitia mwili wake hapa duniani. Lakini ili mapenzi yake yafanyike ni lazima kila Mkristo atimize wajibu wake.

### *Mwili unafaulu kazi wakati viungo vinashughulika kwa pamoja*

Mwili unafanyaje kazi? Mwili unafanya kazi pale ambapo viungo vyote vya mwili vinafanya kazi kwa pamoja. Kidole hakiwezi kufanya kitu peke yake. Vivyo hivyo na Mkristo hapaswi kuishi peke yake bila Wakristo wengine. Kila Mkristo ameunganishwa na Wakristo wengine katika Mwili wa Kristo ili kwa pamoja watimize mapenzi ya Kristo. Ni katika hali ya ushirikiano Mwili wa Kristo una uwezo mkubwa zaidi. Kwa sababu ni mwili mmoja, Wakristo wanategemeana. Ndiyo sababu Biblia inatoa maagizo kwa Wakristo: kusaidiana, kufundishana, kuonyana, kupendana, kuheshimiana, kuhimizana, kujengana, n.k. Wakifanya hivyo kwa pamoja watafaulu kutimiza mapenzi ya kichwa aliye Yesu Kristo.

***Tawi la mahali ni mfano wa Mwili wa Kristo***

Kama mshiriki wa Mwili wa Kristo, kila mjumbe ni sehemu ya kundi lile na Yesu anataka kazi zake zitendeke kwa pamoja na katika ummoja. Lakini haiwezekani kila Mkristo ajue na afanye kazi akiwa karibu na kila Mkristo duniani. Kwa sababu hiyo Mungu ameagiza yawepo matawi ya mahali. Wakristo wanapoungana katika matawi ya mahali, wanaweza kutimiza mapenzi ya Mungu kwa njia bora kuliko wanavyoweza kila mtu peke yake. Kusudi la tawi la mahali siyo kukutana na kumwabudu Mungu tu, wala kufundisha Neno la Mungu tu. Kusudi la tawi la mahali ni kutimiza mapenzi yote ya Yesu Kristo. Ni kuabudu, kufundisha Neno la Mungu, na zaidi, likilenga kuhudumia washirika, jamii ya karibu na hata jamii wanaokaa mbali.

***Matawi yanaungana kwa baadhi ya kazi***

Pia kuna kazi zingine ambazo ni kubwa kiasi ambacho matawi mbalimbali yanahitaji kuungana ili waweze kutimiza mpango wa Mungu kwa ajili ya Mwili wa Kristo.

***Mara nyingine Mkristo atatumika peke yake lakini siyo wakati wote***

Mfano huu wa Mwili wa Kristo hauna maana kwamba kila wakati Mkristo atakapofanya huduma atakuwa pamoja na Wakristo wenzake. Kwa kuwa Mkristo ni mtumwa wa Kristo masaa yote, ni wazi mara nyingine atahitaji kufanya huduma peke yake. Lakini hawezi kukaa peke yake kila wakati wala kufanya huduma peke yake kila wakati. Mkristo anayekaa peke yake bila ushirikiano wo wote na Wakristo wenzake atapoteza nguvu na kuanguka njiani. Anahitaji msaada wa Wakristo wenzake ili ajengwe na ili huduma zake zipate kufaulu. Ndiyo maana Mungu ameunda Mwili wa Kristo akiwapa karama zilizo mbalimbali na akiwapa uwezo wa kusaidiana na kutegemeana katika kutimiza mapenzi yake.

***Maana ya kubatizwa katika Mwili wa Kristo***

Tumeona kwamba kila Mkristo ni kiungo au mjumbe wa Mwili wa Kristo. Lakini, Mkristo anapataje kuwa mjumbe? Biblia inasema ni kazi ya Roho Mtakatifu kubatiza Wakristo katika Mwili wa Kristo wakati wanapookolewa

*1 Wakorintho 12:13 – "Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru"*

Maana ya neno "kubatiza" ni kuchovya au kuweka ndani ya kitu kingine. Roho Mtakatifu anaweka au kubatiza Wakristo ndani ya Mwili wa Kristo wakati wanapookolewa. Ubatizo huo siyo ubatizo wa maji. Wayahudi walipewa agizo la kufanya ubatizo wa maji kama tendo linaloendana na toba wakati walikuwa wakiandaliwa kumpokea masihi wao. Wakati mtu alipobatizwa na maji aliwekwa au kuchovywa katika maji. Lakini wakati mtu anabatizwa na Roho Mtakatifu katika Mwili wa Kristo, mtu huyu anawekwa katika Mwili wa Kristo.

**Maana ya kubatizwa katika Mwili wa Kristo:** Kazi ya Roho Mtakatifu ya kuweka Mkristo katika Mwili wa Kristo na kumfanya kuwa kiungo au mjumbe wa mwili huo.

**Matokeo katika maisha ya Mkristo ya kubatizwa katika Mwili wa Kristo:** Mkristo ataelewa ana kazi muhimu ya kutekeleza na atashughulika na kazi hiyo ili mapenzi ya Yesu Kristo, aliye kichwa cha mwili, yapate kutimizwa.

**Maswali ya kutafakari:** Je, maisha yako yanaoneshaje wewe ni mjumbe wa Mwili wa Kristo anayeshughulika? Una huduma au nafasi gani katika Kanisa?

## C. Tunapookolewa Tunaunganishwa Na Kristo

Kabla hatujaokolewa tulikuwa bila Kristo. Tunapookolewa tunaunganishwa na Kristo. Muungano wetu na Kristo ni jambo la ajabu. Inamaanisha kwamba sisi ni ndani ya Kristo (Rum 8:1; 2 Kor 5:17), Kristo ni ndani yetu (Yn 14:20; Gal 2:20), na Mungu Baba na Mwana wanakaa ndani yetu! (Yn 14:23; 1 Yn 4:15, 1 Kor 6:19). Tukifikiria maana ya mambo haya, tutaona kwamba muungano wetu na Kristo ni mkubwa sana.

*2 Wakorintho 5:17 – "Hata imekuwa, mtu akiwa* ***ndani ya Kristo*** *amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."*

*Wagalatia 2:20 – "Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali **Kristo yu hai ndani yangu**; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu."*

*Yohana 14:23 – "Yesu akajibu, akamwambia, Mtu akinipenda, atalishika neno langu; na Baba yangu atampenda; **nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake.**"*

***Matokeo ya sisi kuwa ndani ya Kristo ni nini?***

Kwa sababu tumo ndani yake, kamwe hatutahukumiwa.

*Warumi 8:1 – "Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu."*

Kwa sababu tuko ndani yake kamwe hatutatengwa na Mungu.

*Warumi 8:35-39 – "Ni nani atakayetutenga na upendo wa Kristo?... Lakini katika mambo hayo yote tunashinda, na zaidi ya kushinda, kwa yeye aliyetupenda… Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba… wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu."*

Muungano wetu unatupa amani katika maisha yetu kwa sababu hatutakuwa na hofu kwamba tunaweza kupotea.

Kwa sababu tumo ndani ya Kristo, tunabarikiwa na baraka zote za rohoni.

*Waefeso 1:3 – "Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika ulimwengu wa roho, ndani yake Kristo."*

Baraka za rohoni haziko kama baraka za kimwili. Baraka za kimwili zinadumu kwa muda tu. Baadhi ya baraka za kimwili ni afya nzuri, akili, watoto, mvua n.k. Lakini baraka za rohoni zinadumu milele. Tukiwa ndani ya Kristo, tuna hakika kwamba baraka za rohoni hazitaondolewa. Tunaweza kuzitegemea na kuzifurahia baraka hizo hata milele. Baadhi ya baraka hizo zinatajwa katika Waefeso sura 1:

- Tumechaguliwa naye (1:4)
- Tumefanywa kuwa watakatifu (1:4)
- Tumefanywa kutokuwa na hatia (1:4)
- Tumefanywa kuwa wana (1:5)
- Tumepewa ukombozi (1:7)
- Tumepewa msamaha wa dhambi (1:7)
- Tumefanywa warithi (1:11)
- Tumefanywa sifa ya utukufu wa Kristo (1:12)
- Tumeokolewa (1:13)
- Tumepewa Roho Mtakatifu kama arabuni ya urithi wetu (1:14)
- n.k.

Kwa sababu tumo ndani ya Kristo, tunapata uwezo wa kuzaa matunda ya kiroho na kuishi maisha yanayompendeza Mungu. Katika Yohana 15:1-17 Yesu anajifananisha na mzabibu na anatufananisha na matawi. Kama mzabibu unavyoliwezesha tawi kuzaa matunda, vivyo hivyo, Yesu anatuwezesha sisi kuzaa matunda ya kiroho. Yesu alisema kwamba hatuwezi kuzaa matunda ya kiroho isipokuwa tukikaa ndani yake. Matunda ambayo tutayazaa tukiwa ndani ya Yesu ni: upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, na upole (Gal 5:22,23).

**Maana ya kuungwa na Kristo:** Tendo la Mungu la kumweka katika Kristo yule anayemwamini Kristo.

**Matokeo ya kuungwa na Kristo katika maisha ya Mkristo:** Mkristo atakuwa na amani kwa sababu hawezi kutengwa na Mungu, tena atawezeshwa kuzaa matunda ya kiroho.

**Maswali ya kutafakari:** Je, una amani na Mungu? Je, matunda gani ya kiroho yanaonekana katika maisha yako?

## D. Tunapookolewa, Tunampokea Roho Mtakatifu.

***Kila Mkristo anaye Roho Mtakatifu ndani yake***

Copyright © 2017 GMI Publications

Tunapookolewa, Mungu anatupa Roho Mtakatifu akae ndani yetu. Roho Mtakatifu ni zawadi itokayo kwa Mungu kwa waumini wote. Mungu hawapi baadhi ya Wakristo Roho Mtakatifu, bali kila mmoja anayemwamini Yesu Kristo anapewa Roho Mtakatifu siku hiyo hiyo. Kama mtu hana Roho Mtakatifu, mtu huyu siyo Mkristo (Rum 8:9).

*1 Wakorintho 3:16 – "Hamjui ya kuwa ninyi mmekuwa hekalu la Mungu, na ya kuwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?"*

*Wagalatia 4:6 – "Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba."*

***Roho Mtakatifu akiingia kwa Mkristo hatoki tena milele***

Tuna ahadi ya Yesu kwamba Roho Mtakatifu atakuwa nasi milele.

*Yohana 14:16 – "Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele."*

Baada ya kuja na kukaa ndani yetu, hatatoka tena. Hata kama Mkristo anatenda dhambi, Roho Mtakatifu bado anakaa ndani yake. Mtume Paulo alipowaandikia Wakorintho, aliwauliza kama walijua kwamba miili yao ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye **ndani yao** (1 Kor 6:19). Katikati yao kulikuwa watu waliofanya uovu, hata uzinzi. Swali la mtume Paulo lilionesha kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ndani ya wote, hata waliotenda dhambi hizo. Habari hii inaleta amani mioyoni mwetu kwamba Roho Mtakatifu hatatuacha, hata tukifanya dhambi.

***Uthibitisho wa kuwa na Roho Mtakatifu***

Tunawezaje kuwa na uhakika kwamba tunaye Roho Mtakatifu ndani yetu? Watu wengine wanasema kwamba uthibitisho wa kuwa naye Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha. Lakini Biblia haifundishi kwamba kunena kwa lugha ni uthibitisho wa Roho Mtakatifu kukaa ndani ya Mkristo. Bali Biblia inasema ikiwa mtu hana Roho Mtakatifu ina maana huyu siyo wa Kristo.

*Warumi 8:9 – "Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake."*

Hivyo, kila anayemwamini Kristo kweli kweli ni lazima anaye Roho Mtakatifu. Kwa hiyo tuna uhakika tunaye Roho Mtakatifu kama tumemwamini Kristo. Tunao uhakika huo kwa sababu tunaamini ukweli wa Neno la Mungu linaloahidi kwamba wote wanaomwamini Kristo wanaokolewa na kupewa Roho Mtakatifu.

Jambo la pili linalotuhakikishia kwamba tunaye Roho Mtakatifu ni matunda ya Roho Mtakatifu katika maisha yetu. Wakati mtu anamwamini Yesu Kristo, Roho Mtakatifu anakuja kukaa ndani ya mtu huyu na anaanza kufanya kazi katika maisha yake. Kazi mojawapo ya Roho Mtakatifu ni kuzalisha matunda ya Roho ndani ya maisha ya Mkristo. Matunda kama vile upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, na kiasi (Gal 5:22-23). Matunda ya Roho yataonekana zaidi na zaidi katika maisha ya Mkristo aliye na Roho Mtakatifu ndani yake. Matunda hayo ni uthibitisho wa kuwepo kwa Roho Mtakatifu ndani yake.

***Roho Mtakatifu ni muhuri***

*Waefeso 1:13 – "Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu; tena mmekwisha kumwamini yeye, na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu."*

Kila Mkristo anapookolewa anapewa Roho Mtakatifu kuwa muhuri na arabuni (Efe 1:13-14; 2 Kor 1:22). Tuangalie kwanza maana ya "muhuri". Wakati Rais, mwenyekiti, au katibu anaandika barua, anaitia muhuri wake kama uthibitisho wa kwamba barua hii inatoka kwake. Muhuri unahakikisha kwamba kitu fulani ni cha mtu fulani. Tunapookolewa, tunapewa Roho Mtakatifu kama muhuri wa Mungu kama uthibitisho wa kwamba sisi ni wa Mungu. Mungu anatuahidi kwamba Roho Mtakatifu ni muhuri hata siku ya ukombozi.

*Waefeso 4:30- "Wala msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu; ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata siku ya ukombozi."*

Maana yake, Mungu anatuahidi kwamba tutakuwa wa kwake mpaka siku Yesu atakaporudi. Ni muhimu kuelewa Mungu hakusema, "Mpaka siku utakapotenda dhambi." Yaani, kuwepo kwa Roho Mtakatifu ndani yetu ni uthibitisho wa kwamba hatuwezi kupoteza wokovu wetu na kwamba Mungu atati-

*Copyright © 2017 GMI Publications*

miza ahadi zake zote za kutufikisha mbinguni. Mungu hatauondoa muhuri wake, aliye Roho Mtakatifu, kabla Yesu hajarudi kutupeleka mbinguni.

***Roho Mtakatifu ni arabuni***

*Waefeso 1:14 – "Roho yule wa ahadi aliye Mtakatifu. Ndiye aliye arabuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya utukufu wake."*

Roho Mtakatifu pia ni "A*rabuni ya urithi wetu*." Arabuni ni nini? Kama mtu anataka kununua kitu fulani na hana hela ya kutosha, analipa kiasi fulani kama arabuni. Arabuni ni kitu ambacho mwenye kununua anatoa kama ahadi kwamba atarudi kuyamalizia malipo. Asiporudi kuyamalizia malipo yale, mwenye kuuza atabaki na hizo pesa alizoziweka. Mungu ametupatia Roho Mtakatifu kama arabuni ya urithi wetu. Maana yake ni kwamba Mungu anatuahidi kwamba tutarithi uzima wa milele. Kwa sasa katika maisha yetu hapa duniani Mungu ametupa Roho Mtakatifu, na kwa kuwa tumempokea Roho, tunaweza kuwa na uhakika kwamba siku moja tutaishi na Mungu mbinguni. Mungu ni mwaminifu. Ataitimiza ahadi yake! Mungu hatamwondoa Roho Mtakatifu. Mungu asipotimiza ahadi yake, kwa kawaida ingekuwa na maana kwamba sisi tungebaki na Roho Mtakatifu kama mali yetu. Jambo hilo haliwezekani kwa sababu Roho Mtakatifu ni Mungu; hatuwezi kummiliki Mungu. Lakini Mungu anapojitoa kama ahadi, anafanya hivyo kwa sababu yeye ana uhakika asilimia mia kwamba atatimiza ahadi yake ya kutufikisha mbinguni. Mungu hayuko katika hatari ya kumpoteza Roho Mtakatifu wake kwa kuwa ana uwezo wa kutimiza ahadi zake.

***Kazi za Roho Mtakatifu***

Roho Mtakatifu hakai bure ndani yetu. Anatusaidia sana katika maisha yetu ya kikristo. Hapo chini tumetaja baadhi ya kazi anazozifanya kwa ajili yetu wakati anakaa ndani yetu.

- Anatujaza (Efe 5:18)
- Anatuongoza (Rum 8:14)
- Anatupa uhakika wa wokovu wetu (Rum 8:16)
- Anatusaidia kuomba (Rum 8:26)
- Anatuwezesha kuzaa matunda ya kiroho (Gal 5:22,23)
- Anatuwezesha kutozitimiza tamaa za mwili (Rum 8:13; Gal 5:16).

***Tumshukuru Mungu kwa ajili ya Roho Mtakatifu***

Roho Mtakatifu ni zawadi kubwa yenye thamani sana! Tusiache kumshukuru Mungu kwa kutupatia Roho Mtakatifu.

**Maana ya kumpokea Roho Mtakatifu:** Tendo la Mungu la kumweka Roho Mtakatifu akae ndani ya kila anayemwamini Yesu.

**Matokeo ya kumpokea Roho Mtakatifu katika maisha ya Mkristo:** Mkristo atakuwa na uhakika kwamba ameokolewa na kwamba hawezi kupotea kamwe. Pia Roho Mtakatifu anasaida kila Mkristo kuishi maisha matakatifu.

**Mambo ya kutafakari:** Una uhakika na wokovu wako? Maisha yako yanaoneshaje unaye Roho Mtakatifu ndani yako?

## E. Tunapookolewa, Tunahesabiwa Haki.

*Warumi 3:24 –"Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu."*

Kabla hatujaokolewa, tulikuwa na hatia ya dhambi mbele ya Mungu. Tunapookolewa, Mungu anatuhesabia haki (Rum 3:24, 4:5). Katika kuhesabiwa haki na Mungu kuna sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ni kuondolewa hatia ya dhambi. Sehemu ya pili ni kuipokea haki ya Kristo.

***Kuhesabiwa haki ni kuifuta hatia tuliyo nayo***

Kwanza, Mungu anapomhesabia mtu haki, anasema kwamba yule hana hatia kutokana na dhambi zake tena. Mungu anatangaza mtu yule hataadhibiwa tena kwa sababu Yesu ameichukua adhabu ya dhambi zake zote. Amesamehewa dhambi zake zote kwa sababu deni la dhambi lililipwa kikamilifu kupitia damu ya Yesu Kristo.

***Kuhesabiwa haki ni kupewa haki ya Kristo***

Ya pili, Mungu anapotuhesabia haki, anatupa haki ya Kristo. Ni kusema, Mungu anaona haki ya Kristo kuwa haki yetu.

*2 Wakorintho 5:21 – "Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye."*

***Mungu anatuona tukiwa tumevaa haki ya Yesu siyo haki yetu***

Kuhesabiwa haki hakumaanishi kwamba Mungu ametubadilisha kwa ndani ili tuwe wenye haki. Yaani, Mungu hatubadilishi ili matendo yetu yote yawe ya haki. Kuhesabiwa haki kunahusu jinsi Mungu anavyotuona. Mungu anatuona bila hatia ya dhambi, na badala yake anaona haki ya Kristo kuwa haki yetu. Kutokana na matendo yetu sisi siyo wenye haki wala hatuwezi kustahili kuhesabiwa wenye haki. Bali, kwa neema ya Mungu, tunavalishwa haki ya Yesu Kristo na kwa sababu hiyo Mungu anatutangaza kuwa wenye haki.

***Kwa neema, wasio na haki (wala uwezo wa kuipata) wanahesabiwa haki na Mungu***

*Tito 3:6,7 – "…kwa njia ya Yesu Kristo Mwokozi wetu; ili tukihesabiwa haki kwa neema yake, tupate kufanywa warithi wa uzima wa milele, kama lilivyo tumaini letu."*

Lazima tuelewe kwamba mtu hahesabiwi haki kwa sababu ya haki yake mwenyewe. Sisi hatuna haki hata kidogo mbele ya Mungu, kwa sababu haki zetu ni chafu mbele ya Mungu (Isa 64:6). Mtu hahesabiwi haki kwa sababu amefanya cho chote kuziondoa dhambi zake. Mtu hana namna yo yote ya kuziondoa dhambi na kujisafisha (Rum 10:2-4). Sababu ya kuhesabiwa haki ni neema ya Mungu (Rum 3:24; Tit 3:7). Ni neema ya Mungu iliyomtuma Yesu kufa na kulipa deni la dhambi zetu.

***Aliyehesabiwa haki na Mungu hawezi kuwa na hatia tena hata akitenda dhambi***

Sisi Wakristo tunapotenda dhambi, Shetani anatushitaki (Ufu 12:10). Kwa sababu ya mashtaka ya Shetani Wakristo wengine wanajisikia kwamba hawastahili kuitwa Wakristo na wanaishi na hofu ya kupotea. Wanajisikia aibu na hatia mbele ya Mungu. Je, tunatakiwa kuishi na hofu, aibu na hatia kwa sababu ya kutenda dhambi? Hapana. Mkristo anayeishi hivyo, hawezi kuishi maisha ya ushindi juu ya dhambi, bali ataishi kama mtu aliyeshindwa dhidi ya Shetani. Hatakuwa na amani na Mungu kama impasavyo. Tena, anakana ukweli wa Warumi 5:1 inayosema kwamba kwa sababu ya kuhesabiwa haki tuna amani na Mungu! Mkristo anayeishi hivyo haamini kwamba Mungu amemsamehe dhambi zake zote, amempa haki ya Kristo na amemtangaza kuwa mwenye haki. Sisi Wakristo hatutakiwi kuishi na hofu kwa sababu ya dhambi tunazozitenda kana kwamba Mungu ataamua kutuhukumu. Hakuna dhambi zinazoweza kumfanya Mungu atuone tena kuwa na hatia ya dhambi. Mungu alipotuhesabia haki, aliziona dhambi zote tulizozitenda na dhambi zote tutakazozitenda na alitusamehe zote!

***Kutoweza kupata hatia tena hairuhusu Wakristo kutenda dhambi***

Kama hatutakiwi kuwa na hofu, aibu, wala hatia tunapotenda dhambi, tunatakiwa kufanya nini? Tunaweza kutojali dhambi au kufurahia dhambi? Hapana! Tu watumwa wa Mungu na kama watumwa wake tunapotenda dhambi, tunatakiwa kujisikia kama Mungu anavyojisikia. Tunapaswa kuchukia dhambi na kuhuzunika wakati tunapotenda dhambi. Mungu ni Mtakatifu na anataka sisi tuwe watakatifu katika matendo yetu. Tutawezaje kuishi katika dhambi wakati Yesu aligharimu maisha yake kwa ajili ya kutukomboa na dhambi? Kutotenda dhambi kwetu ni njia ya kuonesha shukrani yetu kwa Mungu aliyetuokoa. Kama Wakristo, tunapotenda dhambi, tunapaswa kuungama dhambi yetu. Hatufanyi hivyo kwa ajili ya kukwepa hukumu ya Mungu wala kwa ajili ya kuokoka. Mungu alishasamehe dhambi hizo na kutuahidi hatutahukumiwa naye tena na zaidi ameahidi hatuwezi kupoteza wokovu wetu. Bali kuungama dhambi zetu kama Wakristo ni kwa ajili ya kutengeneza uhusiano wetu na Mungu kama mwana na baba yake. Hatujapoteza uwana wetu lakini kuungama dhambi zetu kunatusaidia kuboresha uhusiano ule unaoendelea na Mungu. Pia kuungama dhambi zetu kama Wakristo kunapunguza uwezekano wa Mungu kutuadhibu kama wana (Ebr 12:5-11). Adhabu hiyo si ya hasira bali ni ya upendo (Ebr 12:6). Adhabu hiyo siyo hukumu ya kuangamiza bali ni yenye kusudi la kuwa faida yetu, *"ili tuushiriki utakatifu wake"* (Ebr 12:10).

**Maana ya kuhesabiwa haki**: Tendo la Mungu la kumtangaza kuwa mwenye haki yule anayemwamini Yesu Kristo kwa sababu Mungu ameiondoa hatia ya dhambi yake na kumpa haki ya Kristo.

Copyright © 2017 GMI Publications

**Matokeo ya kuhesabiwa haki katika maisha ya Mkristo:** Mkristo ataishi na amani bila hofu ya kupotea, wala hatia au aibu mbele ya Mungu.

**Swali la kutafakari:** Unapotenda dhambi, je, unaogopa utapoteza wokovu wako?

## F. Tunapookolewa, Tunatakaswa.

***Maana ya utakaso***

Neno "utakaso" au "kutakasa" linamaanisha "kufanya takatifu." Tunaposema kwamba tumetakaswa, tunasema kwamba tumefanywa watakatifu na ndiyo maana Biblia huita Wakristo watakatifu (2 Kor 1:1; Efe 1:1; Flp 4:21,22).

***Utakaso kamili siku ya kuokoka***

Biblia inafundisha kwamba kuna aina mbili za utakaso wa Mkristo. Aina moja inahusika na wokovu. Aina hii ni utakaso kamili unaotendeka wakati tunapookolewa.

*1 Wakorintho 6:11 – "Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu."*

Utakaso huo unakamilika mara moja, yaani ni tendo lilioisha.

***Mungu anawahesabu Wakristo kuwa Watakatifu***

Utakaso huo unafananishwa na kuhesabiwa haki na ni tangazo la Mungu kwamba huyu aliyemwamini Yesu anaonekana safi machoni pa Mungu, ndiyo sababu Mungu anaweza kuwaita Wakristo "watakatifu". Ingawa siyo hali halisi ya Wakristo katika maisha yao, ni tamko la Mungu kama hakimu katika mahakama yake.

Utakaso huo siyo mabadiliko ya ndani ya mioyo yetu kutufanya tuwe safi bali ni mabadiliko katika jinsi Mungu anavyotuona. Mungu hatuoni kuwa wachafu tena. Anatuona kuwa watakatifu. Si kwamba hatufanyi dhambi tena, lakini Mungu **anatuona** kama vile hatuna dhambi.

***Mungu anaweza kutuhesabu Watakatifu kwa kuwa alikufa kwa ajili ya dhambi zetu zote***

*Waebrania 10:10 – "Katika mapenzi hayo mmepata utakaso, kwa kutolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu."*

Je, Mungu anawezaje kutuona kuwa watakatifu ingawa tunaendelea kutenda dhambi? Tutaangalia tena mfano tuliotumia tulipoichunguza kazi ya Yesu msalabani. Tuliona kwamba Yesu alizichukua akiadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu na kwa njia hiyo akaondoa dhambi na hatia yetu akitupa msamaha wa dhambi zetu. Kwa sababu hiyo tumesafishwa dhambi zetu zote; dhambi tulizozitenda wakati uliopita, na dhambi tutakazozitenda wakati ujao.



*Mchoro#13 - Mchoro huu unaonesha dhambi tulizozitenda, tunazozitenda, na tutakazozitenda zimelipiwa na sasa machoni pa Mungu sisi ni watakatifu tusio na hatia ya dhambi.*

Tumesema Mungu kama hakimu anatamka katika mahakama yake kwamba wote wanaomwamini Yesu ni wenye haki, ni watakatifu, na ni waliotakaswa. Tamko hilo linawezeshwa na kazi ya Yesu kuwalipia deni la dhambi zao na kuwashirikisha katika haki, utakatifu, na usafi wake. Kumbe baada ya kuokoka Mungu anapotuangalia anaona haki, utakatifu, na usafi wa Yesu kana kwamba ni haki, utakatifu, na usafi wetu.

Hali hii inawezekana kwa sababu sisi Wakristo tumeunganishwa na Kristo. Tumo ndani ya Kristo na Kristo yumo ndani yetu. Mungu anapotuona, hatuoni peke yetu, bali anatuona pamoja na Kristo. Ndiyo maana anauona utakatifu wa Kristo kuwa wa kwetu.

*1 Wakorintho 1:30 – "Bali kwa yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi."*

*Wagalatia 3:27 – "Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo"*

***Mfano wa Wakorintho - Watakatifu wanaotenda dhambi***

Biblia inatumia neno "watakatifu" kueleza wale ambao wametakaswa na Mungu. Neno hilo linatumiwa kwa Wakristo wote na si kwa wale tu wanaofaulu zaidi katika kutotenda dhambi (2 Kor 1:1, Efe 1:1, Flp 4:21-22; Kol 1:22, Ebr 10:10). Mungu anawaita Wakristo watakatifu ingawa bado wanatenda dhambi kwa sababu wamesafishwa dhambi zao kwa damu ya Kristo na kwa sababu wamo ndani ya Kristo. Ndiyo sababu mtume Paulo aliweza kuwaita Wakorintho *"wale waliotakaswa katika Kristo Yesu"* (1 Kor 1:2). Je, Wakorintho walikuwa watu ambao waliishi maisha makamilifu bila dhambi? Hapana. Wengine kati yao walikuwa na tabia mbaya sana. Mtume Paulo aliwakemea mara nyingi kwa sababu walikuwa wanaishi maisha maovu. Kwa sababu ya uovu wao mtume Paulo aliwaita *"watu wenye tabia ya mwilini"* (1 Kor 3:1-3)! Kweli hawakuishi maisha makamilifu, lakini bado walikuwa watakatifu kwa sababu walisafishwa dhambi zao na walikuwa ndani ya Kristo. Ndiyo sababu Mungu aliwaona kuwa watakatifu.

***Mfano wako - Mtakatifu anayetenda dhambi***

Hatupaswi kuangalia Wakorintho kujua kwamba Wakristo (watu ambao wametakaswa) hawaishi maisha makamilifu kila wakati. Kila mmoja tunaweza kujiangalia wenyewe na kujua "kutakaswa" siyo kuishi bila dhambi. Mtakatifu ni Mkristo aliye safi machoni pa Mungu kwa sababu ya Kristo, si kwa sababu ya matendo yake mwenyewe kama Mkristo.

***Mtakatifu anaweza kushirikiana na Mungu***

Kumbuka kwamba mwanadamu anapaswa kuwa mtakatifu ili aweze kushirikiana na Mungu. Tunapookolewa, tunatakaswa (tunafanywa watakatifu) machoni pa Mungu. Ndiyo sababu Mungu anaweza kushirikiana na wote wanaomwamini Yesu na kuwa na uhusiano nao.

***Utakaso wa siku hadi siku katika maisha ya Mkristo***

*2 Wakorintho 7:1- "Basi, wapenzi wangu, kwa kuwa tuna ahadi hizo, na tujitakase nafsi zetu na uchafu wote wa mwili na roho, huku tukitimiza utakatifu katika kumcha Mungu."*

Aina ya pili ya utakaso ni utakaso unaoendelea muda wote katika maisha ya Mkristo. Unaeleza hali ya Mkristo anavyobadilika polepole katika maisha yake ili afanane na Yesu na aishi kwa namna inayompendeza Mungu. Mistari mingi sana inaeleza wajibu wa Mkristo kujitakasa kwa kuachana na dhambi (2 Kor 7:1, 1 Pet 2:11), kwa kujitoa kwa Mungu na kufanya nia yao upya (Rum 12:1-2), kwa kukua kiroho (1 Pet 2:2), kwa kufuata haki, utauwa, imani, upendo saburi n.k. (1 Tim 6:11-12), kwa kuishi kwa ajili ya Mungu (Gal 2:20), kwa kumfuata Mungu (Efe 5:1-2) kwa kumwiga Yesu (2 Kor 3:17-18; Rum 8:9; Efe 5:2; Flp 2:5-8) na mambo mengine mengi tusiyoweza kuyataja hapa.

Mungu anatusaidia kufaulu katika shughuli ya utakaso huo. Tulishaona jinsi tulivyopewa Roho Mtakatifu kukaa ndani yetu ili atusaidie kuishi jinsi Mungu anavyotaka, lakini hata Yesu anatusaidia na ataendelea kutusaidia mpaka siku ya mwisho.

*Wafilipi 1:6 – "Nami niliaminilo ndilo hili, ya kwamba yeye aliyeanza kazi njema mioyoni mwenu ataimaliza hata siku ya Kristo Yesu"*

Utakaso huo hautakamilika mpaka Mungu atakapowapa Wakristo miili ya utukufu siku ambayo Kristo atanyakua Kanisa lake. Siku ile tutafanana na Kristo kweli kweli na tutaitwa watakatifu kwa sababu kweli kweli tutakuwa watakatifu. Kwa sasa, sisi Wakristo hatujakamilika, lakini kwa uwezo wa Mungu tunabadilika siku hadi siku tukifuata maagizo ya Mungu.

**Maana ya kutakaswa:** Tendo la Mungu kumfanya mtakatifu, machoni pake, yule anayemwamini Kristo kwa sababu ya damu ya Kristo na muungano wa Mkristo na Kristo.

**Matokeo ya kutakaswa katika maisha ya Mkristo:** Mkristo anaweza kushirikiana na Mungu mtakatifu.

**Swali la kutafakari:** Maisha yako yanaoneshaje jinsi unavyoshirikiana na Mungu?

## G. Tunapookolewa, Tunafanywa Wana.

***Tunazaliwa tukiwa wana wa Shetani***

Tunapookolewa Mungu anatufanya kuwa wana wake. Watu wengine wanawaza kwamba sisi sote ni wana wa Mungu tangu kuzaliwa kwetu. Lakini Biblia inafundisha kwamba tulizaliwa tukiwa wana wa

Shetani (Yn 8:44) tena tukiwa na asili ya dhambi (Rum 5:12). Ni wakati tunapookolewa Mungu anatuingiza katika jamaa yake na kutufanya kuwa wana.

***Kuwa mtoto wa Mungu ni kuwa mrithi wake***

*Wagalatia 4:7 – "Kama ni hivyo, wewe si mtumwa tena bali u mwana; na kama u mwana, basi, u mrithi kwa Mungu."*

Kwa sababu tumekuwa wana wa Mungu, Biblia inatufundisha kwamba sisi ni warithi wa Mungu. Tunarithi nini? Urithi wetu ni wokovu, yaani uzima wa milele (Ebr 1:14; Tit 3:7). Kama warithi wa wokovu tutaishi na Mungu milele mbinguni. Urithi wa kidunia, kama mali au pesa, unaweza kuharibika na kupotea, lakini Mungu anatunza urithi wetu na hauwezi kuharibika (1 Pet 1:3,4). Utadumu milele (Ebr 9:15).

***Kuwa mtoto wa Mungu ina maana tunahusiana na Mungu bila hofu***

*Warumi 8:14,15 – "Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu. Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba."*

Kwa sababu tumekuwa wana wa Mungu, tuna uhusiano maalumu na Mungu. Hatutakiwi kumwogopa Mungu tena. Uhusiano wetu ni zaidi ya kuwa na ushirikiano na Muumba wetu, ni zaidi ya kuwa na ushirikiano na Mtawala mkuu, na ni zaidi ya kuwa na ushikiriano na hakimu mkuu. Uhusiano wetu na Mungu ni wa karibu sana kama uhusiano kati ya mtoto na baba yake. Ndiyo sababu tunaweza kumwita Mungu "baba". Tunaweza kustarehe katika upendo mkamilifu wa Mungu unaozidi hata upendo wa wazazi wetu hapa duniani.

**Maana ya kufanywa wana:** Tendo la Mungu la kumfanya kuwa mwana mrithi yule anayemwamini Kristo.

**Matokeo ya kufanywa mwana katika maisha ya Mkristo:** Mkristo atastarehe katika upendo wa Mungu, Baba yake, na kuufurahia uhusiano wa karibu na Mungu.

**Swali la kutafakari:** Je, unafurahia uhusiano wako na Mungu kama mtoto anayependwa naye?

### H. Tunapookolewa Tunasamehewa Dhambi Zetu

Wakati tunapookolewa Mungu anatusamehe dhambi zetu zote (Mdo 10:43; 13,38; 26:18; Efe 1:7; Kol 1:14; 2:13). Hatusamehewi dhambi zile tu tulizotenda kabla hatujazaliwa, bali tunasamehewa hata dhambi zile ambazo hatujazitenda bado. Katika kusamehe dhambi zetu Mungu anatangaza kwamba malipo yamelipwa na yamekubaliwa asilimia mia. Hatuwezi kuhukumiwa tena kwa ajili ya dhambi zetu kwa kuwa Mungu alishazisamehe zote.

Mungu anawezaje kusamehe dhambi zetu zote wakati tunapookolewa? Anaweza kuzisaheme zote kwa kuwa alishazihukumu katika Yesu msalabani.

**Maana ya kusamehewa dhambi zetu zote:** Tendo la Mungu kusamehe dhambi zote za Wakristo kwa sababu dhambi hizo ziliadhibiwa katika Yesu Kristo msalabani.

**Matokeo ya kusamehewa dhambi zote katika maisha ya Mkristo:** Wakristo wanaweza kuishi bila kuhofu kwa maana hawatahukumiwa kwa kuwa dhambi zao zote zimeshasamehewa (zilizotendeka, zinazotendeka, na zitakazotendeka).

**Maswali ya kutafakari:** Je, unaamini ahadi ya Mungu kwamba alishasamehe dhambi zako zote? Je, unamshukuru Mungu kwa zawadi hiyo ya ajabu?

## 16. Wokovu Unaleta Mabadiliko Gani Ndani Yetu?

**Tunapookolewa, tunazaliwa mara ya pili na kuhuishwa**

*Waefeso 2:4-6 – "Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhuisha pamoja na Kristo; yaani, tumeokolewa kwa neema"*

*1 Petro 1:23 – "Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyo-haribika; kwa Neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele."*

Kabla hatujaokolewa tulikuwa wafu kiroho. Tunapookolewa tunazaliwa mara ya pili. Kuzaliwa mara ya pili kunamaanisha kupata kuwa hai kiroho. Mtu anapozaliwa mara ya kwanza, anazaliwa kimwili. Yeye ni hai kimwili lakini ni mfu kiroho kwa sababu ya asili yake ya dhambi. Mtu anapozaliwa mara ya pili, anazaliwa kiroho, yaani anapata kuwa hai kiroho.

***Mungu hawezi kuhusiana na mfu kiroho***

Kama vile sisi hatuwezi kuwa na uhusiano na maiti, Mungu hawezi kuwa na ushirikiano na walio wafu kiroho. Ni lazima roho ya mtu, ambayo imekufa, ifanywe tena kuwa hai. Ndiyo sababu Bwana Yesu alisema, *"Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu"* (Yn 3:3).

***Roho Mtakatifu anafanya watu kuwa hai kiroho***

Hakuna mtu anayeweza kujifanya kuwa hai kiroho, kama vile hakuna maiti anayeweza kujifanya tena kuwa hai. Tendo hili la kuhuisha wafu ni tendo la Roho Mtakatifu tu (Tit 3:5). Watu wengine wanawaza kwamba wataokolewa kupitia matendo mema, lakini, je, matendo mema yanaweza kumfanya mfu kiroho awe hai? Hapana!

***Kuwa kiumbe kipya ni kuwa na moyo mpya***

*2 Wakorintho 5:17 – "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya."*

Mtu anapozaliwa mara ya pili, anakuwa kiumbe kipya. Ni badiliko kubwa ndani yetu. Tuna moyo mpya. Tunaposema "moyo", tunamaanisha utu wa ndani kabisa. Moyo ni jumla ya akili, nia, mawazo, na hamu ya mtu. Kuwa na moyo mpya ni kusema hamu kubwa ya maisha ya mtu imebadilika. Kabla mtu hajazaliwa mara ya pili, hamu kubwa yake ilielekea dhambi, faida yake mwenyewe au mambo ya kidunia tu. Mtu anapozaliwa mara ya pili, hamu yake kubwa inamwelekea Mungu. Anampenda Mungu kuliko mambo yote. Anataka kumpendeza Mungu kuliko mambo yote (2 Kor 5:9). Anataka kuyafanya mapenzi ya Mungu kuliko kuyafanya mapenzi ya ye yote mwingine.

***Hata kiumbe kipya anaweza kutenda dhambi***

Kuwa Mkristo aliye kiumbe kipya pamoja na moyo mpya, haimaanishi kwamba Mkristo hatatenda dhambi tena. Bali inamaanisha hatafurahia dhambi tena kwa sababu hamu yake inamwelekea Mungu. Anapotenda dhambi, atahuzunika kwa sababu amemkosea yule anayempenda. Kwa sababu anampenda Mungu na anataka kumpendeza Mungu, anaziungama dhambi zake na kujitahidi kuendelea katika njia inayompendeza Mungu.

**Maana ya kuzaliwa mara ya pili:** Tendo la Roho Mtakatifu la kumhuisha anayemwamini Yesu Kristo ili awe hai kiroho.

**Matokeo ya kuzaliwa mara ya pili katika maisha ya Mkristo:** Mkristo atakuwa na hamu mpya ya kumpendeza Mungu kuliko ye yote mwingine.

**Swali la kutafakari:** Maisha yako yanaoneshaje kwamba unataka kumpendeza Mungu kuliko mambo yote mengine?

# 17. Je, Mungu Aliwachagua Wote Watakaookoka?

*Matendo 13:48 – "Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza Neno la Bwana, nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini."*

Biblia inafundisha kwamba Mungu amewachagua wale watakaookolewa. Kuyaelewa yale Biblia inayofundisha kuhusu kuchaguliwa na Mungu, tutauliza maswali matatu:

## <u>A. Mungu Aliwachagua Lini Wale Watakaookolewa?</u>

Jibu ni kwamba aliwachagua kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Maana yake ni kwamba aliwachagua kabla hawajazaliwa na kabla hawajatenda tendo lo lote liwe zuri au baya. Kwa sababu hiyo tunajua

Wakristo hawajachaguliwa na Mungu kwa sababu ya matendo wala uzuri wo wote ulio ndani yao. Bali, aliwachagua kabla hawajaishi na kuonesha hali yao.

*Waefeso 1:4 – "Kama vile alivyotuchagua katika yeye kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake katika pendo."*

*2 Wathesalonike 2:13 – "Lakini imetupasa sisi kumshukuru Mungu sikuzote kwa ajili yenu, ndugu mliopendwa na Bwana, kwa kuwa Mungu amewachagua tangu mwanzo mpate wokovu, katika kutakaswa na Roho, na kuiamini kweli."*

## B. Mungu Aliwachagua Namna Gani?

*2 Timoteo 1:9 – "Mungu; ambaye alituokoa akatuita kwa mwito mtakatifu, si kwa kadiri ya matendo yetu sisi, bali kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele"*

Aliwachagua kufuatana na mapenzi yake na rehema yake. Hakuwachagua kufuatana na matendo yao wala wema wao (Rum 9:11-23).

***Mfano wa Yakobo na Esau***

Katika Warumi 9:11-23 mtume Paulo anatumia mfano wa Yakobo na Esau kuonesha jinsi Mungu anavyowachagua watu. Kabla hawajazaliwa, Mungu alikuwa amekwishamchagua Yakobo na kumkataa Esau. Kwa nini? Kwa sababu ya wema wa Yakobo na uovu wa Esau? Hapana, bado walikuwa hawajaishi ili wamwoneshe Mungu matendo yao. Mungu aliamua kumchagua Yakobo hata kabla Yakobo hajazaliwa kwa sababu Mungu ni Muumbaji na mtawala wa yote na ana haki ya kuamua anavyotaka. Mtume Paulo anaendelea kusema kwamba uchaguzi wa Mungu haulingani na uchaguzi wetu, lakini unalingana na rehema ya Mungu. Maana ya rehema ni nini? Kutoadhibu wale wanaostahili kuadhibiwa. Mungu alipowachagua watu, aliionesha rehema yake kwa sababu wale waliochaguliwa hawatapata adhabu wanayostahili. Habari za wale wasiochaguliwa? Watapata tu adhabu wanayostahili.

***Bado Mungu ana haki hata asipochagua wengine***

Mtume Paulo alijua suala hili litazaa maswali hivyo aliuliza na kujibu maswali mawili. Swali la kwanza ni: *"Kuna udhalimu kwa Mungu?"* (Rum 9:14). Jibu lake ni *"Hasha."* Sisi sote tunastahili hukumu ya Mungu. Kama Mungu angetuacha sisi sote tuadhibiwe, bado angekuwa na haki. Kama, kwa sababu ya rehema na huruma yake, anawachagua wengine kutopata adhabu yao, hajawakosea wale ambao hakuwachagua. Wao wanastahili adhabu yao.

***Si juu ya wanadamu kuyatathimini maamuzi ya Mungu***

Swali la pili ni "*Mbona angali akilaumu?*" (Rum 9:19) Jibu lake ni *"Wewe u nani umjibuye Mungu?"* (Rum 9:20). Kama Muumba wetu na mtawala mwenye haki, sisi hatuna haki ya kubishana naye.

## C. Kusudi la Kuwachagua ni Nini?

Ili wamtukuze Mungu.

*Waefeso 1:11-12 – "Na ndani yake sisi nasi tulifanywa urithi, huku tukichaguliwa tangu awali sawasawa na kusudi lake yeye, ambaye hufanya mambo yote kwa shauri la mapenzi yake. Nasi katika huyo **tupate kuwa sifa ya utukufu wake**, sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu."*

Mungu aliwachagua watu ili waokoke. Kwa sababu ya kuokolewa na kuwa huru kutoka dhambini, wanaweza sasa kuishi maisha yanayompa Mungu sifa.

***Akili yetu ndogo haielewi mambo yote ya Mungu***

Elimu ya kuchaguliwa na Mungu inaweza kuleta maswali mengi. Tusisahau kwamba Mungu ni mwenye haki; yaani, vyote anavyotenda ni sahihi. Pia, tukumbuke kwamba Mungu ni mwema. Labda hatuwezi kuielewa kikamilifu elimu hii, lakini Mungu daima anatenda haki.

Mistari mingine inayohusu kuchaguliwa na Mungu: Rum 8:28-30; Rum 11:28; 1 Pet 1:1; Rum 11:7; 2 Tim 2:10; Tit 1:1; 1 Thes 1:4-5; Ufu 13:7-8.

*Copyright © 2017 GMI Publications*

**Maana ya kuchaguliwa na Mungu:** Tendo la Mungu kabla ya kuumbwa kwa dunia la kuwachagua baadhi ya watu kuokolewa, si kwa sababu ya wema wao, lakini kwa sababu ya mapenzi yake, mema yake, na rehema yake.

# 18. Je, Mtu Anaweza Kujua kwa Uhakika Kwamba Ameokoka?

Biblia inafundisha kwamba Mkristo anaweza kuwa na uhakika wa wokovu wake.

***Biblia inaeleza Wakristo wameshaokoka***

Kwanza, Biblia inafundisha kwamba wokovu siyo kitu ambacho mtu atatumainia kupokea wakati ujao, bali ni kitu anachopata mara anapomwamini Yesu. Katika Waefeso 2:8 mtume Paulo aliandika, *"Kwa maana **mme**okolewa."* Na katika 2 Timotheo 1:8,9 na Tito 3:4,5 aliandika *"**ali**tuokoa."* Tunaona katika vifungu hivi kwamba wokovu ni tukio ambalo limeshafanyika kwa Wakristo wote. Pia, Yesu alisema katika Yohana 3:36, *"Amwaminiye Mwana **yuna** uzima wa milele."* Hakusema, "Amwaminiye Mwana **atapata** uzima wa milele." Tayari Mkristo anao uzima wa milele.

***Yohana anatuhakikishia kwamba tayari tunao wokovu***

Wakristo wengine wanaweza kuwa na shaka kuhusu wokovu wao. Ndiyo sababu mtume Yohana aliuandika waraka wa 1 Yohana. Katika 1 Yohana 5:13 anaandika, *"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili **mjue ya kuwa mna uzima wa milele**, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu."* Anahakikisha kwamba tunaweza kujua kwamba tumeokolewa.

***Wokovu hautambuliki kwa njia ya hisia zetu bali kwa ahadi ya Neno la Mungu***

Wengine wana shaka na wokovu wao wakisema hawajisikii kuwa watoto wa Mungu na wengine wana shaka kwa sababu wameambiwa Mkristo kweli hawezi kutenda dhambi. Inabidi tukumbuke kwamba msingi wa wokovu wetu siyo jinsi tunavyojisikia siku hadi siku, wala jinsi tunavyoachana na dhambi. Msingi wa wokovu wetu ni Mungu na neema yake. Mungu anasema kwamba tunaokolewa kwa sababu ya neema yake na kwa njia ya imani katika Yesu. Mungu ni mwaminifu na Neno lake linaweza kuaminika. Tunaweza kustarehe juu ya ahadi yake, ikiwa tuna imani ya kweli; yaani, ikiwa tumeiweka imani kamili katika kazi ya Yesu msalabani kwa ajili ya dhambi zetu zote.

***Mfano wa Wakorintho katika kuupima wokovu***

Mtume Paulo aliwaagiza Wakristo wa Korintho, *"Jijaribuni wenyewe kwamba mmekuwa katika imani; jithibithisheni wenyewe. Au hamjijui wenyewe, kwamba Yesu Kristo yu ndani yenu?"* (2 Kor 13:5). Katika swali la mwisho, mtume Paulo anategemea kwamba watajua kwa hakika kwamba Yesu ni ndani yao. Jinsi walivyoweza kujijaribu ni kujiuliza kama wameiamini Injili ya kweli; yaani, kukitegemea kifo cha Yesu tu ili kupata msamaha wa dhambi zao zote na kuamini kwamba Mungu alimfufua tena.

# 19. Uzima wa Milele Unadumu Muda Gani?

***Haiwezekani kuupoteza wokovu uliotolewa na Mungu***

Watu wengine wanadhani kwamba wataupoteza wokovu wao wakitenda dhambi. Lakini, Biblia inafundisha wazi kwamba wokovu ni zawadi ya milele na hatuwezi kuipoteza zawadi hiyo. Baadhi ya vifungu vinavyothibitisha umilele wa wokovu ni kama vifuatavyo: Yoh 3:16,36; Yoh 6:37; Yoh 10:28; Rum 8:1; Rum 8:35-39; Efe 4:30; Ebr 10:10-14.

***Kama tunaweza kuupoteza wokovu ina maana Yesu hajafa kwa ajili ya dhambi zetu zote (ndiyo kusema kifo cha Yesu kina mapungufu)***

Tumeona kwamba wakati Yesu alipokufa msalabani, alichukua dhambi zetu zote. Alijitoa mara moja tu kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu zote. Aliadhibiwa kwa ajili ya dhambi zetu zote. Aliziondoa dhambi zetu zote. Alitusafisha dhambi zetu zote ili tusamehewe dhambi zetu zote. Ndiyo sababu tunasoma katika Waebrania 10:12-14 kwamba kupitia dhabihu yake moja msalabani, ameshawakamilisha hata milele wale ambao wameokolewa. Kusema kwamba mtu anaweza kupotea tena, ni kusema kwamba mtu yule ataadhibiwa kwa ajili ya baadhi ya dhambi zake. Tukisema kwamba ataadhibiwa kwa ajili ya baadhi ya dhambi zake, tunasema kwamba dhabihu ya Yesu haikutosha kutusamehe dhambi zetu zote. Kama kifo cha Yesu hakikufaa kutusamehe dhambi zote, Yesu alikufa bure na hakuna wokovu.

***Mungu alilitumia neno milele kwa kuwa alimaanisha milele***

Mungu aliamua kuiita zawadi tunayopokea tunapomwamini Yesu nini? Uzima wa milele. Neno "milele" linamaanisha nini? Uzima usio na mwisho; unaodumu milele. Kama mtu angeweza kupoteza wokovu wake, ingekuwa bora kwa Mungu kuita zawadi yake "uzima wa muda" au "uzima mpaka utakapotenda dhambi" au "uzima mpaka ____?____." Asingeita zawadi yake "uzima wa milele". Kuona kwamba Mungu alichagua kuiita zawadi yake uzima wa milele, tunaweza kusema bila shaka kwamba uzima tunaopokea tunapookolewa utadumu milele. Kama mtu anaupokea uzima wa milele kutoka kwa Mungu halafu baadaye anaukuta uzima huo unaisha ina maana Mungu amekuwa mwongo. Mungu siyo mwongo hivyo akisema milele, ujue ni milele.

# 20. Kunamtokea nini Mtu Anapookolewa?

*Warumi 6:3-4 – "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."*

*Waefeso 2:10 – "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza ili tuenende nayo."*

Matokeo ya wokovu katika maisha ya Mkristo ni kuishi maisha mapya ya matendo mema. Ni namna gani Mkristo ataweza kuishi maisha haya mapya? Mungu alipotuokoa, alitupa uwezo wa kuishi maisha haya mapya (2 Pet 1:3). Tuyarudie na kukumbuka mambo Mungu aliyotujalia alipotuokoa:

- Mungu ametukomboa kutoka katika mamlaka ya Shetani na dhambi ili tuishi maisha yasiyo na dhambi kwa sababu hatutawaliwi na Shetani wala dhambi tena.
- Mungu ameturudisha chini ya utawala wake kama watumwa wake ili tumtii Mungu na kuishi maisha yanayolingana na mapenzi yake.
- Mungu ametuzaa mara ya pili ili tuwe na hamu mpya ya kumpendeza Mungu kuliko mambo yote.
- Mungu ametupatia Roho Mtakatifu ili tuwe na uwezo wa kuishi maisha matakatifu.
- Mungu ametuunga na Kristo ili tuwezeshwe kuzaa tunda la kiroho.

***Mungu ametuwezesha kuishi maisha yanayompendeza yeye***

Tunaona kwamba kupitia mambo yaliyo hapo juu, wakati Mungu alipotuokoa, kweli alitujalia uwezo wote wa kuishi maisha mapya ya kufanya matendo mema. Ametuweka huru na mamlaka ya Shetani na dhambi. Kwa hiyo hatupaswi kufanya dhambi tena. Ametupatia hamu mpya ya kuyafuata maagizo na mapenzi yake. Kupitia Roho Mtakatifu na kuungwa na Kristo tumepewa uwezo wa kuishi maisha matakatifu na kuyafanya matendo mema yanayompendeza na kumpa utukufu.

***Maana kwetu***

Basi, wajibu wetu ni nini? Ni kujua mambo haya, kuyaamini mambo haya na kuishi kufuatana na yale tunayoamini. Ndivyo jinsi wokovu wetu unavyotuwezesha kuishi maisha mapya.

**Tuishi sasa kwa uwezo tulio nao kutoka kwa Mungu kwa ajili ya utukufu wake.**